# Nipashe

Jumatatu Oktoba 24, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581108

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMI

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700

LIKE & FOLLOW




ESMA PLATNUMZ ATAFUTA MCHUMBA

UKURASA 27








**Rostam** asifia sera ya Samia kuvutia mitaji ya uwekezaji

UKURASA 4



Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili wa Baraza la Vyama vya Siasa, Doyo Hassan

# Vyama 14 siasa vyamwangukia Samia kuhusu demokrasia

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### RAIS TSHISEKEDI AWASILI NCHINI ZIARA YA SIKU 2

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Felix Tshisekedi Tshilombo...

UKURASA WA 3

### WAZIRI ATAKA VITENDO SERA MAHITAJI MAALUM

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, ametaka...

UKURASA WA 8

### JELA MIAKA 12 KWA KUMUUA MKEWE

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu...

## Ghala kuhifadhia mali za magendo lateketea kwa moto

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Félix Antoine Tshisekedi Tshilombo, baada ya kuwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Asimulia anavyopanda ukuta baada ya kuzibwa na majirani

UKURASA 2

**MICHEZO** | **ZUCHU ADAIWA KUIBA WIMBO** UK.27 | **KABWELA** UK.7



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (katikati), akikagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa uwekezaji wa jengo la Mzizima Tower jijini Dar es Salaam, linalomilikiwa na NSSF. **Habari UK 5. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vyama 14 vyamwangukia Samia kuhusu demokrasia

**Na Jenifer Gilla**

MUUNGANO wa vyama 14 vya upinzani nchini umemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kupitia haraka na kuifanyia kazi ripoti ya kikosi kazi ili kutatua mambo ya msingi ikiwamo ruhusa ya kufanya mikutano ya kisiasa.

Aidha, vyama hivyo vimemtaka Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kutekeleza maagizo yaliyo chini yake kuhusu ripoti hiyo itakayotolewa na Rais ikiwamo mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa ili viwe na uhuru wa kufanya shughuli zao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili wa Baraza la Vyama vya Siasa, Doyo Hassan, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu msimamo wa vyama kutokana na ripoti hiyo na kupongeza juhudi za serikali kukamilisha mchakato huo.

"Sisi tunamwomba Mheshimiwa Rais atufanyie haraka kidogo hasa katika masuala ya kanuni na sheria za mikutano ya hadhara na ruzuku za vyama vya siasa ili tuweze kujiendesha na huko mtaani muone kazi zetu na sera zetu kama vyama na vya siasa na tuisaidie nchi.

"Ukisoma mapendekezo manane yaliyotolewa katika muhtasari siku ile, kuna masuala ya mabadiliko ya vyama vya siasa kwa ajili ya kuweka miundombinu mizuri ya siasa na demokrasia nchini. Hili liko chini yake msajili," alisema.

Doyo ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC), alisema ripoti hiyo imesheheni masuala yote yanayohusu vikwazo vya kisiasa nchini, hivyo anaamini kama Rais ataifanyia kazi na kuitolea maagizo, itarudisha uhuru wa demokrasia nchini.

Aidha, mwenyekiti huyo alisema ameshangazwa na kitendo cha baadhi ya viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuipinga ripoti hiyo ilhali hawajui kilichoandikwa ndani kwa kuwa bado haijawekwa hadharani.

"Tulitaraji kuona Watanzania tunajipa muda wa kusoma kwa kina yale yaliyowasilishwa kwa Rais na wajumbe wa kikosi kazi badala ya kukimbilia kupinga yale yaliyosomwa kama sehemu ya muhtasari katika ripoti ile," alisema Boyo.

Alisema vyama vya siasa vina uhuru wa kutoshiriki kutoa maoni na ni sehemu ya uhuru wa kikatiba lakini kutoshiriki kwao kusionekane kama jambo hilo halifai kwa sababu wako waliokubali kushiriki.

Maoni ya chama hicho ya kukosoa ripoti hiyo na kuwataka wananchi kupinga yale yaliyowasilishwa na kikosi kazi, alisema ni mambo ya kupuuzwa kwa sababu walihusishwa viongozi mbalimbali wa nchi wakiwamo wa dini, wanasiasa na wanazuoni.

"Huwezi ukapuuza maoni na mawazo ya viongozi waliolisukuma taifa letu mpaka hapa tulipo kwa sababu zako binafsi. Tumeona hili jambo si sawa, mawazo ya chama kimoja hayawezi kuharibu jambo liliofanywa na watu wengi kwa kutumia pesa nyingi," alisema.

Katibu Mkuu wa Democratic Party (DP), Felix Makua, alisema kuundwa kwa kikosi kazi hicho kulitokana na mkwamo wa kisiasa hasa katika upande wa mikutano ya hadhara na katiba. Katika vikao vyao, CHADEMA waligoma kushiriki jambo wanalolitafsiri kama ni ubinafsi.

Muungano huo unaundwa na vyama vya African Democratic Alliance (ADA-TADEA), ADC, ACT-Wazalendo,Tanzania Labour (TLP),Demokrasia Makini (MAKINI) na DP.

Vingine ni Sauti ya Umma (SAU), Alliance for African Farmers Party (AAFP), Chama cha Kijamii (CCK), United Peoples' Democratic Party (UPDP) na National Reconstruction Alliance (NRA) na National League for Democracy (NLD).

Ripoti hiyo ilikabidhiwa Oktoba 22, mwaka huu, ikiwa na mapendekezo 18 yaliyogusa maeneo mbalimbali kwa ustawi wa demokrasia nchini.

# Asimulia anavyoruka ukuta baada kuzibiwa njia na majirani zake

**Na Halfani Chusi**

NI majira ya saa 5:00 asubuhi maeneo ya Mwapemba Kata ya Toangoma, Kigamboni mkoani Dar es Salaam, anaonekana mjane, Amina Ali (75), akipanda juu ya ukuta wa jirani kuingia kwenye nyumba yake. Hapo ndipo Nipashe inajiuliza kulikoni?

Nipashe inajaribu kumdadisi mama huyo, ambaye baada ya kutambua anayemdadisi ni mwandishi wa habari, haiba yake inabadilika na kuelekea kwenye simanzi na kuanza kutoa machozi huku akisimulia kwa machungu.

"Nilinunua nyumba hapa kipindi cha nyuma kidogo. Nilikuwa peke yangu baadaye majirani wakaanza kuuza maeneo yanayonizunguka. Wakaja matajiri wakanunua na kuanza kujenga bila mpangilio. Baadaye nyumba yangu ikazungukwa mpaka nikajikuta nakosa kwa kupita kuingia kwangu.

"Wakati hawa watu wanajenga nilikuwa nawafuata na kuwaeleza kuwa hii sehemu ni njia ya kuingilia kwangu lakini hawakutaka kunisikiliza. Walidai hata serikali ya mtaa inafahamu kwamba wao wamenunua eneo hilo na hawajaelekezwa kama hii sehemu ya mimi kupita," alisema.

Mama huyo aliendelea kusimulia kwa uchungu huku katika malalamiko yake akimtaja jirani aliyepakana naye mwenye jina la Mama Stomu kuwa amejenga ukuta ulioziba njia ya kuingilia kwenye nyumba yake na ameweka geti ambalo hataki kutumia na mtu mwingine.

"Huyu jirani yetu hapa anaitwa Mama Stomu, amejenga ukuta ambao unaziba nyumba yangu, lakini ametengeneza geti kwenye njia ya kuingilia nyumbani kwangu na analitumia peke yake na funguo anakaa nazo mwenyewe sisi hajatupa. Fikiria mimi na umri wangu huu kweli niwe naingia kwenye nyumba yangu kwa kupanda kwenye ukuta?

Tukiomba funguo anasema anaogopa wezi. Swali la kujiuliza sisi ndio tumemkaribisha na ndio majirani zake sasa inakuwaje atuone wezi. Yote hiyo anatumia mabavu ili sisi tukose pa kupita.

Kutokana na adha hiyo, alisema amelazimika kuihama nyumba yake kwa sababu hana njia ya kuingia kwake.

"Nimeshafikisha jambo hili katika vyombo mbalimbali vya serikali ikiwamo kwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa, diwani pamoja na baraza la ardhi la kata lakini na kote huko imeshindikana," alisema.

Nipashe ilipomfuata Mama Stomu kujibu tuhuma hizo, alisema eneo aliloweka geti ni sehemu ya kuingilia kwenye nyumba yake na si kama majirani hao wanavyodai.

"Mimi hii njia ya kwangu peke yangu na tangu nahamia hapa nilikuwa naitumia peke yangu wao walikuwa wanatumia njia ya huko juu ya kutokea kwa muuza genge baada ya kuuzwa kiwanja cha mbele yake. Hao walionunua walipojenga wakaziba njia yake na sasa hivi amerudi tena kwangu kwa sababu ananiona mimi mnyonge," alisema.

"Waulize wakati mimi nahamia hapa wenyewe walikuwa wanatumia njia gani mpaka mimi nikatengeneza geti langu la kutumia peke yangu. Kwa nini wasimzuie yule aliyejenga mbele ya nyumba yao tangu mwanzo kama hiyo ni njia? Hapa mimi ni kwangu na siko tayari kutumia nao njia pamoja.

"Niko tayari kwenda kokote lakini si kuruhusu njia hii tutumie pamoja. Fikiria uchochoro wenyewe ni mwembamba hadi gari langu linashindwa kuingia humu ndani. Kwa hiyo nimeamua niwe nalilaza sehemu za kulipia wakati nyumba ninayo lakini shida nafasi ya kuingilia kwangu ni ndogo tena mtu anataka hiyo hiyo tutumie wote kwa kweli hilo hapana," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, Shabani Mkambala, alithibitisha kupokea malalamiko hayo huku akibainisha kuwa alishamwita ofisini kwake lakini aligoma kutii wito, hivyo kushauri suala hilo kulipeleka mbele.

Diwani wa Kata hiyo, Mohamedi Mketo, naye anaungana na mwenyekiti kuwa analifahamu juu ya kulifahamu sakata hilo.

"Nilipokea malalamiko kutoka kwa familia hiyo nikaenda hadi hapo kuona nini kinaendelea. Baada ya kufika hapo nikawaita nikaongea nao tena nilikuwa na mwenyekiti wa baraza la ardhi nikawashauri hayo mambo wayamalize.

"Nilikuwa tayari kutumia hata gharama zangu kutenganisha mpaka ili kuumaliza huo mgogoro lakini baada ya kuona kuna utata, maelewano madogo, nikashindwa kujua namna ya kuwasaidia," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Kata, Hassan Ligire, alithibitisha kuwapo kwa malalamiko hayo japo alipomwita malalamikiwa (Mama Stomu) na aligomea wito wake.

"Malalamiko hayo kweli yapo na yalikuja ofisini kwangu nikampeleka barua ya wito mara ya kwanza hakuja nikamwita tena na mara ya pili hakuja. Mlalamikaji alipoona kimya wakaamua kulipeleka suala hili kwa diwani wa kata na wakati anaenda kwa ajili ya kukagua, aliniita kwenda kushuhudia.

"Baada ya hapo diwani akasema suala hilo atalishughulikia mwenyewe kwa hiyo tangu hapo sijui suala liliishaje lakini kwangu mimi aligoma nilipomwita kwa ajili ya mahojiano," alisema.

# Waziri ataka vitendo sera mahitaji maalum

**Na Golden Kisapile, TUDARCo**

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, ametaka kutumika kwa sera ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu kuwasaidia kutimiza ndoto zao.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa sera ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu wakati wa maadhimisho miaka 60 ya Chuo Kikuu cha Dar er Salaam (UDSM) Shule Kuu ya Elimu.

"Nimefarijika kwamba UDSM imetengeneza sera kwa ajili ya wanafunzi na wenye mahitaji maalumu ambayo itaongeza hamasa ya watu wenye mahitaji maalumu kupata elimu nchini.

"Sera hii itakuwa na dira kwa wanafunzi watakaojiunga katika chuo hiki kwa miaka ijayo na maadhimisho haya yatapata mafanikio makubwa na kujenga jamii jumuishi," alisema. Hongereni mnahudumia zaidi ya wanafunzi 150,000 mnawawezesha kutimiza ndoto zao. Nataka niwahikishie serikali itaunga mkono juhudi za UDSM katika kuwezesha wenye mahitaji maalumu," alisema.

"Serikali inataka elimu itolewe kwa ubora na usawa bila ada ngazi ya elimu ya msingi hadi sekondari kwa kuzingatia wenye makundi maalumu. Bajeti ya elimu imegusa makundi mbalimbali ya kisekta na inawapa kipaumbele watoto wa kike na wenye mahitaji maalumu, hivyo serikali inatazama kwa jicho la pekee wanafunzi wenye mahitaji maalumu," aliongeza.

Awali, Makamu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye, alisema chuo kimeongeza udahili wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kwamba wanawatia moyo kuwa wanaweza kufikia hatua kubwa kielimu.

"Pia UDSM imefanikiwa kuanzisha sera ya elimu ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na niipongeze serikali kwa kujali watu wenye mahitaji maalumu," alisema.

Naye Mkuu wa Shule Kuu ya Elimu, Dk. Eugenia Kafanabo, alisema kongamano hilo limewaleta wadau mbalimbali wakiwamo wanafunzi wenye uhitaji maalumu na watalaamu wa mahitaji maalumu.

# Ghala kuhifadhia mali za magendo lateketea

**Na Oscar Assenga,** TANGA

GHALA lililokuwa limehifadhi shehena ya bidhaa za magendo zilizoshindwa kulipiwa ushuru na wafanyabiashara limeteketea kwa moto katika Bandari ya Tanga.

Ghala hilo linalomilikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Tanga, lilikuwa na vitu mbalimbali yakiwamo mabalo ya vitenge 370, sukari, mchele, mafuta ya kupikia na pikipiki, ambavyo vilikamatwa vikiingizwa kwa njia ya magendo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika eneo la tukio, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omar Mgumba, alisema alipata taarifa kuwa ghala hilo linateketea kwa moto saa 8:30 usiku na kufika eneo la tukio.

Alisema mkazo mkubwa ni kuhakikisha wanazima moto huo ili kuanza uchunguzi wa kubaini chanzo kilichosababisha moto huo.

"Kwa sasa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kuzima moto huo ndipo waendeleea kufanya uchunguzi ili kubaini sababu za moto huo.

"Kwa sasa tunahakikisha usalama wa mali zilizobaki katika eneo hilo baada ya hapo tutaunda tume maalumu ya kufanya uchunguzi wa kina wa chanzo cha tukio hilo na sababu za kuzuka kwa moto huo kabla ya kuchukua hatua zaidi," alisema Mgumba.

Aidha, alisema alitoka eneo hilo Oktoba 17, alipokwenda kukagua shehena ya mabelo 370.

Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Tanga, Fatma Ngenya, alisema majira ya saa 8:30 usiku walipokea taarifa za moto kutoka Mamlaka ya Bandari Tanga na walifika wakavunja geti na kufanikiwa kudhibiti moto huo.

Meneja wa Bandari ya Tanga, Masoud Mrisha, alisema walipata taarifa za moto huo kupitia ofisa ulinzi mwandamizi wa Bandari.

Oktoba 2, mwaka huu, shehena ya magendo ya sukari na mafuta ya chakula, iliyokuwa imeingizwa nchini kupitia Bandari Bubu ya Kasera iliyoko nje kidogo ya jijini Tanga, iliripotiwa kutoroshwa na watu wasiojulikana katika mazingira ya kutatanisha.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa huo, Omari Mgumba, bidhaa hizo zilitoroshwa muda fupi, baada ya kufika bandarini hapo, huku majahazi yaliyoubeba mzigo huo yakitelekezwa.

# Rais Tshisekedi awasili nchini

**Na Jenifer Gilla**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Felix Tshisekedi Tshilombo, amewasili jijini Dar es Salaam jana na kupokewa na mwenyeji wake Rais Samia Suluhu Hasan, kwa ziara ya kikazi ya siku mbili nchini.

Rais Tshisekedi na mwenyeji wake walikagua gwaride lililoandaliwa kwa ajili yao kisha kuelekea Ikulu kwa ajili ya kuendelea na ratiba ya leo ikiwamo kutia saini mikataba ya makubaliano ya kibiashara na kuongea na waandishi wa habari.

Rais Tshisekedi anatarajiwa kutembelea Bandari ya Dar es Salaam pamoja na mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) na anatarajiwa kuondoka nchini Oktoba kesho. Kabla ya kuwasili Dar es Salaam, Rais huyo na ujumbe wake walitembelea Zanzibar na kufanya mazungumzo na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kisha kutembelea vivutio vya utalii.

Ujio wa rais huyo ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ni wa kwanza katika uongozi wa Rais Samia tangu nchi hiyo iingie Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na ya pili tangu achaguliwe kuwa rais wa nchi hiyo mwaka 2020.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe MJini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi Na...75/2022**
**Katika shauri la mirathi ya**
**MOHAMED ISSA ATHUMANI.........................Marehemu**
**Wa MJIMWEMA**
**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa na**
**FATUMA KALENJA.......Mwombaji**

## TANGAZO KWA UMMA

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombajihajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.

**Imetolewa leo tarehe 4 mwezi 10 mwaka 2022**

HAKIMU MKAZI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Muleba**
**Kituo cha Muleba Mjini Mkoa wa Kagera**
**TShauri la Madai no 15/2022**
**Jina la Mdai SUZUNA J TUMBO**
**Jina la Mdaiwa VICTOR KILASARA KYARA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TALAKA KATIKA FAMILIA**

Unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 25/10/2022 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo.Kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO**:Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini.Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20/10/2022

**HAKIMU**

## CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA (IFM)

## MAREJESHO YA MALIPO YA BIMA YA AFYA KWA WAHITIMU WA IFM

CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA (IFM) KINAWATANGAZIA WANAFUNZI WALIOHITIMU AMBAO HAWAJAOMBA KUREJESHEWA FEDHA WALIZOLIPA KWA AJILI YA KUPATIWA VITAMBULISHO VYA BIMA YA AFYA WAKATI TAYARI WALIKUWA NA KADI HIZO, KUWASILISHA MAOMBI YA KUREJESHEWA FEDHA ZAO. TANGAZO HILI LINAWAHUSU PIA WAHITIMU AMBAO WANASTAHILI KURUDISHIWA FEDHA HIZO KUTOKANA NA SABABU NYINGINEZO.

UNAPOFANYA MAOMBI YA KUREJESHEWA MALIPO HAYO UNATAKIWA KUAMBATANISHA VITU VIFUATAVYO:

1. **MAJINA YAKO KAMILI KAMA ULIVYOJISAJILI CHUONI,**
2. **AKAUNTI NAMBA NA JINA LA BENKI,**
3. **NAMBA YAKO YA SIMU.**

MAREJESHO YATAFANYIKA KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA TOKEA TAREHE YA TANGAZO HILI. BAADA YA MUDA HUO KUPITA HAKUNA ATAKAYEREJESHEWA MALIPO HAYO.

MAJINA YA WANAOSTAHILI KUREJESHEWA YANAPATIKANA KATIKA TOVUTI YA CHUO: **http://www.ifm.ac.tz**

**IMETOLEWA NA;**
**NAIBU MKUU WA CHUO.**
**MIPANGO,**
**FEDHA NA UTAWALA.**

217110202

## KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA



**Ndugu JUMA MTANGI KHATIB** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE367941** iliyotolewa na idara ya Uhamiaji Tanzania tarehe 26/10/2020. Ametoa taarifa polisi na kupewa No. **KAG/BUK/RB/412329/2022,** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0753318665 au 0621328665.**

217110702

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**GABRIEL FAIDA SAID**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS** yenye usajili namba **MC882 DCS**, CHASSIS NAMBA: **MD625AF46M1H14706** na ENGINE NAMBA: **0F4HM1914781**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA : KBA/RB/4603/2022**

# ROSTAM: Sera ya Samia inavyovutia mitaji katika uwekezaji kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA na Mbunge wa zamani wa Jimbo la Igunga, Rostam Aziz, amepongeza juhudi zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kuchochea mitaji kutoka nje.

"Tangu ameingia madarakani Rais Samia Suluhu Hassan na vile vile Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wamekuwa mstari wa mbele kushawishi mitaji kutoka nje kuingia nchini. Katika kipindi cha mwaka mmoja tangu Machi 2021 mpaka Machi 2022, mitaji kutoka nje iliyoingia nchini iliongezeka kwa asilimia 300 kutoka Dola za Marekani bilioni 1.13 mpaka bilioni 4.144," alisema.

Rostam, alikuwa akizungumza juzi katika mkutano wa pili wa kuenzi urithi wa Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, aliyefariki dunia Februari, mwaka jana.

Alisema, maendeleo ya kiuchumi hususan uimarishaji wa uchumi mpana, unapaswa kuwa kipaumbele cha serikali yoyote makini kwa kuwa kukua kwa shughuli za uchumi ndio kunazalisha ajira na hatimaye maisha ya wananchi kuwa mazuri na bora zaidi.

"Ninaweza kutamka kwa ushahidi wa kisayansi kuwa katika historia fupi ya nchi yetu tangu Uhuru wa Tanganyika, Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wa Tanzania, kila Jamhuri yetu inapopata viongozi wakuu kutoka Zanzibar kumekuwa na mafanikio makubwa ya mageuzi ya kiuchumi. Tuliona hivyo wakati wa uongozi wa Rais Ali Hassan Mwinyi na tunaona hivyo hivi sasa wakati wa Rais Samia Suluhu Hassan."

"Kama alivyosema Rais Samia Suluhu Hassan katika mazungumzo yake na Rais William Ruto wa Kenya hivi karibuni, tusipoimarisha uwezo wa watu wetu kushiriki katika uchumi, tutajikuta tunagawana umasikini badala ya kugawana utajiri. Ni kwa sababu watu wetu hawana elimu na ujuzi, ndiyo maana tunapata "wawekezaji" uchwara ambao wanakuja kuchukua fursa za Watanzania mithili ya mtu anayeona kwa mbali ameingia kwenye eneo la watu vipofu."

**MKOMBOZI HALISI**

Alisema Rais Samia amejitoa na kujipambanua kuwa mkombozi halisi wa wanyonge na masikini wa nchi. Ni mtetezi au mkombozi wa wanyonge sio anayepiga piga kelele kusema bali ni yule anayewapa vituo vya



Rostam Aziz



Hayati Maalim Seif Sharif Hamad

afya, kuwajengea shule, kuwajengea masoko, kuwafungulia fursa za biashara na ujasiriamali na kuifungua Tanzania kimataifa ili kuongeza fursa kwa Watanzania. "Unaiona dhamira yake hasa ya kuwafanya Watanzania wawe wachezaji, na sio watazamaji tu wa maendeleo ya wengine. Anataka kuona Watanzania kuwa washiriki na sio waimba mapambio."

Akimzungumzia Maalim Seif, alisema licha ya kuwa hakuwahi kuwa kiongozi mkuu wa nchi, lakini katika wadhifa alioshika serikalini alionyesha juhudi za ujenzi wa uchumi. Alipokuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Mipango na Uchumi miaka ya themanini, katikati ya utaifishaji wa mali za watu, Maalim alizuia baadhi ya utaifishaji kwa sababu aliamini kuwa uchumi unajengwa na sekta binafsi. "Maalim Seif anahadithia mwenyewe kuwa alipotembelea kiwanda cha kuchakata mafuta ya kula cha Rajani kule Shinyanga na kukutana na wamiliki na kuelezwa namna biashara ile inafanya kazi, alizuia utaifishaji wa kiwanda kile. Hata sera za kufungua milango ya biashara ambazo Rais Mwinyi alifanya baada ya mwaka 1985 zilitokana na kazi ambayo Maalim Seif alifanya na Rais Mwinyi wakati wawili hao wakiendesha Serikali ya Zanzibar mwaka 1984."

Alisema alikuwa miongoni mwa viongozi mahiri wenye maono, dira na nia ya kuipeleka Zanzibar na Tanzania katika uchumi wa juu zaidi kwa manufaa ya watu wake.

"Uchumi endelevu ni unaoshirikisha wananchi vya kutosha. Wananchi hawawezi na hawapaswi kuwa watazamaji tu au wafanyakazi tu wa wageni. Ni lazima elimu na juhudi za makusudi za kisera zielekezwe kuhakikisha ushiriki wa wananchi katika uchumi. Tusibaki kufurahia takwimu tu za ongezeko la mitaji, kukua kwa GDP n.k. Kama watu hawaoni mabadiliko hizo takwimu hazitakuwa na msaada wowote.

**MFUMO WA ELIMU**

Alisema Zanzibar, wananchi wengi wapo katika sekta ya huduma kwa sababu ya aina ya uchumi wake. Ni lazima mfumo wa elimu Zanzibar uhakikishe kuwa Wazanzibari wanakuwa na ujuzi wa kutosha kushiriki katika sekta kuu ya utalii lakini sekta zinazounganika na sekta hiyo kama vile sekta ya huduma za usafiri wa baharini, angani na nchi kavu, huduma za fedha na benki, uhasibu, ukaguzi, uanasheria, uzalishaji wa bidhaa zinazohitajika katika utalii zikiwamo zinazotokana na kilimo cha mboga na matunda, ufugaji na uvuvi, uendeshaji wa migahawa ya kisasa, na biashara za vito vya thamani. Zanzibar sio tu itoe wafanyakazi wazuri wa hoteli bali mameneja bora na wabunifu wanaoweza kusimama na kuhesabika katika huduma zote muhimu zinazoendesha uchumi wa visiwa hivyo.

Alizitaja sekta mpya zinazoibuka Zanzibar ni pamoja na gesi asilia na mafuta, nishati inayotokana na vyanzo visivyomalizika kama jua na upepo (renewables) na kilimo cha matunda, viungo (Zanzibar kumekuwa na uzalishaji wa muda mrefu wa kienyeji) na mboga. Uzalishaji wa viungo na mboga unahusiana moja kwa moja na ukuaji wa sekta ya utalii.

"Zanzibar leo inapokea watalii chini ya 600,000 kwa mwaka na tayari tunaona sehemu kubwa ya vyakula hata mboga vikiagizwa kutoka nje ya Zanzibar. Hivi wakifika watalii milioni mbili kwa mwaka tutajenga terminal ya kuingiza mchicha, nyanya, vitunguu pale Bandarini?"

Alisema kuna umuhimu wa hatua mahsusi kuchukuliwa kuwajengea uwezo wa elimu Wazanzibari ili wawe na ujuzi wa kuzalisha kwa tija bidhaa hizo ndani ya ardhi yao.

Alisisitiza kuwa elimu inayotoa ujuzi itasaidia kujenga mtaji wa umma wa ndani ili kuwezesha wananchi wa Zanzibar na Tanzania kufaidika kwa pamoja.

**SEIF ALIKUWA KIONGOZI**

"Ulipokuwa unakaa na Maalim Seif Sharif Hamad ulikuwa unahisi hasa kuwa umekaa na kiongozi. Hakuhitaji hata kusema chochote. Uwepo wake popote alipokuwapo ulidhihirisha uwapo wa kiongozi, tena kiongozi kwa maana hasa ya kiongozi. Haiba, bashasha, utulivu, maarifa, weledi na muhimu kuliko yote, hekima na busara - vyote hivi ulikuwa ukivihisi na kuviona kila alipokuwapo."

"Hayo si ya kuhadithiwa na wengine, nimeyaishi na kuyaishi mimi mwenyewe nilipokuwa nikikutana na Maalim Seif. Pengine wengi mnaweza kustaajabu kuwa ni kweli Rostam alipata kukaa pamoja na Maalim Seif kiasi hicho hadi kuweza kumjua na kumzungumza hivi ninavyomzungumza hapa leo? Jibu lake ni ndiyo. Nilibahatika na namshukuru Mungu kwa kunipa bahati hiyo, kwamba sio tu nilikuwa nakutana na Maalim Seif bali tumefanya kazi pamoja kufanikisha jambo moja kubwa sana katika nchi hii - jambo la 'Maridhiano' yaliyozaa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) Zanzibar."

Alisema uchaguzi wa 2005 ambao Rais mstaafu Jakaya Kikwete aliteuliwa kuwa mgombea urais wa Jamhuri ya Muungao kupitia CCM, waliona kuna fursa nzuri ya kulifanikisha hilo. Na ulikuwa ndiyo msingi wa mazungumzo ya Mwafaka wa Tatu ambayo yalikwaa kisiki na hatimaye yakaja kukawamuliwa na mazungumzo ya maridhiano kati ya Rais mstaafu Amani Karume na Maalim Seif hapo mwaka 2009. Kamati ya Maridhiano ikaundwa Zanzibar, kura ya maoni ikafanyika, Katiba ya Zanzibar ikabadilishwa na hatimaye Serikali ya Umoja wa Kitaifa ikaanzishwa Zanzibar.

"Nimeamua kuyasema haya ili kukumbusha tu kwamba mtu ambaye ndiye sababu ya kukusanyika kwetu hapa hakuwa mtu wa kawaida. Ni mtu aliyejitoa nafsi yake na akaukataa ubinafsi kwa kujali nchi yake na watu wake. Huyo ndiye Maalim Seif. Ni aina ya viongozi ambao ni nadra sana kutokea katika nchi. Huwa ni zawadi kutoka kwa Mungu na huchukua miaka mingi na vizazi kadhaa kabla ya kuja mwengine. Kwa nguvu ya kisiasa aliyokuwa nayo angeweza kuamrisha lolote na wafuasi wake wakatekeleza, lakini yeye mara zote alijali maslahi mapana ya nchi yake na watu wake."

HABARI KITAIFA

# Ndalichako: Kitega uchumi cha NSSF Mzizima Tower chadhihirisha juhudi za serikali kwenye uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amepongeza kazi inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ya kufungua fursa mbalimbali zikiwamo za uwekezaji nchini.

Profesa Ndalichako alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa jengo la kitega uchumi la Mzizima Tower linalomilikiwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

"Tunafahamu namna ambavyo Rais wetu Samia Suluhu Hassan anafungua fursa za uwekezaji, kwa hiyo na nyie NSSF mnatengeneza mazingira ambayo wawekezaji watakapokuja nchini watapata sehemu ya kuishi na sehemu ya kufanya biashara zao," alisema.

Alisema kupitia uwekezaji huo wa mradi wa Mzizima Tower inadhihirisha kuwa NSSF inaunga mkono juhudi ambazo zinafanywa na serikali.

Kadhalika, alisema kukamilika kwa mradi huo kutaendana na kazi kubwa anayoifanya Rais Samia ya kufungua uchumi wa nchi, kuweka mazingira mazuri kwenye sekta binafsi na kukaribisha wawekezaji nchini.

"Tumeshuhudia kazi kubwa inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ambavyo imefungua fursa na hivi sasa wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali wanakuja nchini, hivyo bado tunahitaji majengo mengi zaidi ya biashara ikiwamo hoteli ya namna hii," alisisitiza.

Aliwasihi NSSF kuendelea kufanya kazi kwa wakati ili serikali iweze kuona matunda ya mradi huo, pia fedha za wanachama ambazo zimewekezwa kupitia mradi huo zianze kurejeshwa na kutengeneza ajira kwa vijana na kwamba mradi huo ukianza utatoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja 1000.

Pia Ndalichako aliipongeza Bodi ya Wadhamini, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba na menejimenti kwa kazi kubwa mnayofanya hasa ya kuondoa changamoto mbalimbali zilizokuwa zimejitokeza katika mradi huo ambao utakapokamilika utachagiza maendeleo ya taifa na wananchi kwa jumla.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba alisema ujenzi wa mradi huo unaendelea vizuri.

Kwa upande wake, Msanifu wa Majengo ya Mzizima Tower, Kaisi Kalambo, alimweleza Waziri Ndalichako kuwa maendeleo ya mradi huo yamefikia asilimia 88 na kuwa jengo hilo likikamilika litatumika kwa matumizi ya ofisi, hoteli na makazi.

## Mradi kilimo biashara kunufaisha vijana Tarime

**Na Faustine Feliciane,**
TARIME

KAMPUNI ya uchimbaji dhahabu ya Barrick mkoani Mara, imewawezesha vijana 100 wilayani humo kuanzisha mradi wa kilimo cha mboga na kupata soko la uhakika.

Mradi huo wa mwagiliaji ulihusisha vijana walioanza na ekari 10 za kilimo cha mboga zitakazonunuliwa na Barrick kwa ajili ya kulisha wafanyakazi wa mgodi wa North Mara.

Akizungumza mbele ya Naibu Waziri wa Madini, Steven Kiruswa, Kaimu Ofisa Kilimo wa wilaya hiyo, Stanley Kibula, alisema mradi huo umeanzishwa na mgodi huo wa North Mara kuwawezesha vijana wa Kijiji cha Matongo Kata ya Nyamongo wanaozunguka mgodi huo kupata kipato cha kujikimu.

"Huu mgodi umezungukwa na vijiji 11 na kijiji hiki cha Matongo ni kimoja wapo, awali kulikuwa na matukio ya vijana kuvamia mgodi na kuleta mvutano, lakini baada ya kuanzishwa kwa mradi huu na kukabidhiwa kwa vijana, matukio ya migogoro kati ya vijana wa kijiji hiki na mgodi yataondoka," alisema Kibula.

Alisema vijana wanaolima kwenye mradi huo wamepata uhakika wa soko na Barrick kupitia kampuni ya Ako watanunua mazao yote yatakayozalishwa.

Kiongozi wa vijana hao, Chacha Machori, alisema mradi huo umewafanya vijana kuona wanathaminiwa.

"Baada ya Barrick kutupa uhakika wa soko, sisi vijana kwa pamoja tumekubali kupambana na mradi huu na kushirikiana na mgodi katika kila fursa watakayotupa, tumeona litakuwa na manufaa makubwa kuendesha mradi huu ambao naamini baadaye utapanuka zaidi," alisema Machori.

Aliuomba uongozi wa mgodi huo kupanua wigo zaidi kwa kuwasaidia pia kuanzisha ufugaji wa kisasa wa kuku.

Msimamizi wa Kampuni ya Ako wanaolisha wafanyakazi wa migodi yote ya Barrick, Michael Ndolechi, alisema wameamua kuwapa kipaumbele vijana hao kwa kununua mazao yote watakayozalisha kwenye mradi huo.

Mbuge wa Jimbo la Tarime, Mwita Waitara, aliushukuru mgodi huo kwa kuwasaidia vijana wa maeneo hayo kuwaingizia kipato.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Kiruswa, aliwataka wananchi wa Tarime kuendelea kushirikiana na mgodi huo kusaidia maendeleo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**
**BODI YA MICHEZO YA KUBAHATISHA TANZANIA**

## TAARIFA KWA UMMA

## UFAFANUZI KUHUSU TAARIFA ZA ELIMU YA MICHEZO YA KUBET KUFUNDISHWA NCHINI

Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) inapenda kutoa ufafanuzi wa taarifa iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii hivi karibuni kuhusiana na madai ya GBT kutaka Elimu ya Michezo ya Kubet kufundishwa katika taasisi za Elimu ya juu/Vyuo hapa nchini.

Kwanza kabisa tunapenda kuufahamisha Umma kuwa taarifa hiyo ni potofu na imetolewa kinyume na maelezo halisi. Ufafanuzi ni kuwa, **suala la Elimu ya michezo ya kubahatisha (siyo ya Kubet) lilielezwa wakati wa Semina ya Elimu ya ukusanyaji kodi kwa wadau wanaosimamia *uendeshaji na ukusanyaji kodi zinazotokana na michezo ya Kubahatisha nchini na siyo elimu ya Uchezaji.***

GBT ndiyo chombo pekee cha Serikali chenye mamlaka na utaalamu wa kusimamia uendeshaji wa michezo ya kubahatisha nchini. Hata hivyo, katika kutekeleza wajibu wake, GBT inafanya kazi kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali zingine za Serikali. Hivyo GBT ina wajibu wa kutoa Elimu kwa Mamlaka hizo inayoshirikiana nazo ili kuziwezesha kuifahamu michezo hii vizuri na hivyo kuhakikisha kuwa sekta ya Michezo ya Kubahatisha inasimamiwa na kudhibitiwa ipasavyo ikiwemo katika ukusanyaji wa kodi na mapato ya Serikali.

Tunatumai kuwa **Taarifa hii itaondoa Mkanganyiko uliojitokeza** na kuiwezesha sekta ya michezo ya kubahatisha kuendelea kuchangia mapato ya Serikali na maendeleo ya jamii.

Pia tunaomba kutoa wito kwa Waandishi wa Habari nchini (hasa wa mitandaoni) kutoa taarifa kwa weledi ili kuepuka kuleta taharuki isiyo ya lazima kwa jamii.

Kwa maelezo au maswali yoyote kuhusiana na usimamizi wa uendeshaji wa Michezo ya Kubahatisha nchini, tafadhali wasiliana nasi kupitia anuani hapo chini.

**Imetolewa na;**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania**
**Mtaa wa Mission/Sokoine Drive,**
**Ghorofa ya 27, PSSSF Twin Towers, Wing 'A'**
**S. L. P. 1717 Dar Es Salaam, Simu: 022 2124703/4/0800 1100 51**
**Barua pepe: info@gamingboard.go.tz Tovuti: www.gamingboard.go.tz**

217109702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serengeti Girls imeiheshimisha nchi, TFF mulikeni vipaji zaidi

**TIMU** ya Taifa ya Wanawake wenye umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), imeaga Fainali za Kombe la Dunia zinazoendelea nchini India baada ya kuishia hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Serengeti Girls ambayo tofauti na ilivyotarajiwa ilionyesha kiwango cha kuvutia katlka fainali hizo zilizoshirikisha mataifa 16, imeishia hatua hiyo baada ya kutolewa na Colombia kwa mabao 3-0 juzi hivyo kuwashuhudia wapinzani wao hao wakiungana na Nigeria, Ujerumani pamoja na Hispania hatua ya nusu fainali itakayopigwa keshokutwa, Jumatano.

Kabla ya kipigo hicho dhidi ya Colombia, Serengeti Girls ambayo ilikuwa Kundi D, ilipoteza mechi moja tu dhidi ya Japan kwa mabao 4-0, kisha ikashinda 2-1 dhidi ya Ufaransa na kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Canada.

Matokeo hayo yaliifanya Serengeti Girls kumaliza nafasi ya pili kwenye Kundi D, nyuma ya bingwa mtetezi Japan, ambaye alishinda mechi zote tatu kabla ya kukutana na kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Hispania hatua ya robo fainali.

Kwa ujumla hatuna tunachopaswa kuidai Serengeti Girls ambayo ilishiriki fainali hizo kwa mara ya kwanza katika historia yake, lakini ikiungana na timu ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu (Tembo Warriors), kuwa timu pekee kutoka Tanzania zilizofanikiwa kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa mpira wa miguu.

Ikumbukwe Tembo Warriors nayo imetoka kushiriki Fainali za Kombe la Dunia mwaka huu kwa Watu wenye Ulemavu nchini Uturuki na kuishia hatua ya robo fainali, jambo ambalo ni mwanzo mzuri kwa timu hizo za Tanzania.

Kwa mantiki hiyo, japo tulitamani kuona Serengeti Girls ikifika mbali zaidi na hata kutwaa ubingwa huo, kwa ilipoishia tuna kila sababu ya kuipongeza kwani tunatambua haikuwa michuano rahisi hata kidogo.

Tunaamini hivyo hasa tukizingatia timu Serengeti Girls ilizokutana nazo katika fainali hizo, ni nchi ambazo zinautaratibu mzuri wa kulea vipaji katika akademi maalum za soka tangu wakiwa wadogo zaidi ya umri huo, tofauti na Tanzania, ambapo ni vigumu kujua wachezaji hao walitokea wapi kisoka hapo kabla.

Ni wazi vipaji vya wachezaji wa Serengeti Girls vimeonekana wakiwa na umri huo ama wakiwa na miaka 14, hivyo kwa uwezo walionyesha, upambanaji mwanzo mwisho na hatua waliyofikia, tuna kila sababu ya kusema kongole kwao kwa kazi kubwa waliyofanya.

Lakini pamoja na kongole zetu hizo, tuna kila sababu pia kulitaka Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuhakikisha inavilinda vipaji vya watoto hawa kwa kuviendeleza visipotee ili baadaye kuwa msaada mkubwa kwa timu ya Taifa ya U-20, U-23 na hatimaye ya wakubwa, Twiga Stars.

Tunachotamani kwa wachezaji hao ni kuendelea kuwaona wakiwika zaidi katika michuano ijayo ya U-20 na U-23 kwa kiwango cha juu na hilo litawezekana tu kama TFF itakuwa na utaratibu mzuri wa kuwaita mara kwa mara na kuwaandalia mechi mbalimbali za kirafiki ili kuendelea kuwa na muunganiko mzuri.

Tunaamini kwa kiwango walichoonyesha wapo watakaopata timu kubwa Afrika na nje ya bara hili, hivyo kwa kulitambua hilo ni wakati sasa kwa TFF kuelekeza nguvu zaidi katika soka la wanawake kwa kuwa wameonyesha wanaweza zaidi katika mchezo huo pendwa duniani.

Aidha, ni wakati sasa kwa wadhamini kujitokeza zaidi kuzidhamini klabu za soka za wanawake pamoja na Ligi Kuu na ile ya Daraja la Kwanza, ili kuongeza hamasa na ushindani zaidi jambo litakalochochea kukua na kuongezeka kwa vipaji katika soka la wanawake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kongole TFF kwa hili la timu za taifa nchini

Na Adam Fungamwango

**KAMA** una sababu binafsi ndiyo unaweza kuona Shirikisho la Soka nchini (TFF), halifanyi kitu chochote kwa ajili ya kuendeleza soka nchini, lakini endapo utasimama kama mwanasoka halisi, utagundua vinginevyo.

Kwa miaka ya hivi karibuni hasa utawala huu wa Rais Wallace Karia, kumekuwa na mapinduzi makubwa kwenye soka la Tanzania.

Kabla ya kuingia madarakani, tulishuhudia Tanzania ikishiriki michuano michache tu ya soka kama vile timu ya Taifa, Taifa Stars na timu ya soka ya wanawake, Twiga Stars. Kuna wakati timu ya Serengeti Boys nayo ilikuwa inapata nafasi ya kushiriki michuano, ingawa kuna kipindi ilibidi wadau watoe michango.

Tunakumbuka jinsi Redio One na ITV zilivyokuwa mstari wa mbele kipindi hicho kwa ajili ya kuisaidia timu ya vijana chini ya miaka 17, Serengeti Boys, pamoja na kuhamasisha wanamichezo na wadau wote kutoa misaada ya hali na mali kwa ajili hiyo. Na kweli kwa kupitia michango ile Serengeti Boys ilifanya vema sana na kuwa gumzo kila kona nchini na nje ya nchi.

Unaweza kusema wakati huo ni timu tatu zilikuwa zikiangaliwa zaidi na TFF, huku Serengeti Boys ikibebwa zaidi na misaada.

Lakini tangu aingie Karia madarakani, kumekuwa na timu nyingi za soka za taifa ambazo zinashiriki michuano mbalimbali ya Afrika na Dunia. TFF imekuwa ikiziwezesha timu zote hizo kujiandaa, kukaa kambini, kusafiri, kutoa posho kwa wachezaji na makocha.

Kuwapo na timu nyingi za wanaume na wanawake na zote zikiwezeshwa, kumeifanya hata serikali sasa nayo kuweka mkono wake na kuisaidia TFF. Kwa bahati nzuri pia ni kwamba timu hizo si tu zinashiriki kwa kusindikiza, bali zinafanya vizuri na kutoa ushindani mkali sana kwenye anga la soka kimataifa.

Mfano timu ya soka la wanawake chini ya miaka 17, ambayo kwa namna isiyotarajiwa imeishangaza dunia kwa kuweza kufika hatua ya robo fainali kabla ya kutolewa juzi na Colombia.

TFF kwa sasa inaziandaa na kuzitunza timu za taifa kama Taifa Stars, kuna timu ya wanaume chini ya miaka 23 ambayo juzi imecheza mechi ya kusaka tiketi ya AFCON chini ya umri huo dhidi ya Nigeria na kutoka sare ya bao 1-1, lakini kuna kikosi cha timu ya Taifa chini ya miaka 20 ambacho kimeingia kambini juzi kujiandaa na michuano ya kusaka tiketi ya kucheza AFCON, ikiwa ni kwa Ukanda wa CECAFA.

Kwenye timu za wanawake bado wana timu ya Twiga Stars ya wakubwa wanawake, halafu ina timu ya chini ya miaka 20 na ile ya miaka 17 iliyokuwa nchini India.

Kama vile haitoshi bado kuna timu ya taifa ya soka la ufukweni ambayo nayo inashiriki michuano mbalimbali ya kimataifa.

Mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni, TFF chini ya Rais ya Karia imeonekana kulipa soka la nchini mafanikio kwenye nyanja mbalimbali za klabu na timu ya taifa.

Chini ya TFF hii ndiyo taifa kwa mara ya kwanza limepata nafasi nne za klabu kuiwakilisha nchi ambapo huko nyuma tulikuwa tunashangaa tu kwa wenzetu kiasi kwamba hata baadhi walikuwa hawajui ni kwa nini baadhi ya nchi zinatoa timu mbili mbili kwenye michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.

Binafsi, naipongeza TFF, na iendelee kushirikiana na serikali bega kwa bega kwa ajili ya kuendeleza michezo ambapo kwa sasa Tanzania imeanza kuwa moja ya nchi tishio kwenye soka ngazi ya klabu na timu za taifa zote za wanawake. Kwa wanaume pamoja na kwamba bado kuna changamoto nyingi, lakini Stars hii si kama ile ya miaka ya 2000.

Kama nilivyotangulia kusema, wanaoisema vibaya TFF hii wana ajenda zao, pamoja na mambo yao binafsi, lakini kwa takwimu na hali soka ilivyo nchini ukilinganisha na tulipotoka, kama kweli ni mpenzi wa michezo, inastahili sifa lukuki kwa kuuinua mchezo huu nchini, kongole nakupa Karia na jopo lako la uongozi.

# Burundi yaipongeza Tanzania kuhusu lishe

**Na Pascal Mayalla,**
BUJUMBURA

RAIS wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, ameipongeza Tanzania kwa ushirikiano unaoipatia katika nyanja mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Pia amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa salamu zake alizotoa kupitia kwa Salma Kikwete, mke wa Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, wakati wa kufunga kongamano la tatu la kimatatifa la wake wa viongozi barani Afrika (OAFLAD) liliofanyika hivi karibuni jijini hapo.

Ndayishimiye alisema Burundi kama nchi zingine za Afrika, inakabiliwa na changamoto mbalimbali za afya na lishe kwa wanawake, mama na mtoto, watoto wachanga, vijana na vijana balehe.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hizo, Burundi ilizindua kampeni ya "Zero Utapiamlo" Oktoba 2020 kwa lengo la kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha ustawi wa raia wa Burundi.

Rais huyo alitaja hatua kadhaa zilizochukuliwa kuwa ni pamoja na kampeni ya uhamasishaji wa kinamama kuwachanja watoto katika wiki maalum ya afya ya mama na mtoto iliyoandaliwa tangu mwaka 2002. Kupitia kampeni hiyo, hivi sasa karibu kila mtoto anapozaliwa hospitalini, anachanjwa.

Pia Rais Ndayashimiye aliyezungumzia kampeni za uhamasishaji kuzuia magonjwa ya utapiamlo na kukuza afya na lishe bora ikiwa ni pamoja na kuanzisha mpango wa chakula shuleni na kuzuia na kudhibiti fistula, mipango ambayo Tanzania ilishaanza nayo kitambo.

Alisema lengo la kampeni na hatua hizo ni kuhamasisha makundi yote ya jamii kutekeleza wajibu wao katika kukuza afya ya mama na mtoto na katika mapambano dhidi ya utapiamlo, kutoa chakula na lishe bora, kushauriana na wafanya uamuzi kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya na lishe kwa watu walio katika hatari zaidi, hasa wanawake na watoto chini ya miaka mitano.

Mke wa Rais wa Burundi, Angelina Ndayishimiye, alisema kaulimbiu ya mwaka huu ni: "Afya na Lishe ya Wanawake, Watoto na Vijana" na lengo kuu la kongamano hilo lilikuwa kubadilishana, kutafakari na kujitolea kwa hatua endelevu zinazoweza kuchangia kuboresha afya na lishe ya watoto, wanawake na vijana kupitia ushirikishwaji wa viongozi wanawake kuelekea kufikia Lengo la Tatu la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG3).

Mama Salma kwa upande wake, aliwasilisha kwenye mkutano huo, salamu za Rais Samia na kusema Tanzania imepiga hatua kubwa katika masuala ya afya ya mama na mtoto na sasa juhudi zinaelekezwa kwa vijana.

Alisema hivi karibuni Tanzania imeanzisha mpango wa kuendelea kuwasomesha watoto wa kike, waliopata ujauzito wakiwa shuleni, wakati huko nyuma walifukuzwa shule.

Salma aliwakaribisha wajumbe kutoka mataifa mengine ya Afrika kutembelea Tanzania na kujifunza uzoefu na maendeleo ya Tanzania yaliyofikiwa nchini Tanzania ili kutumika kama shamba darasa kwa nchi zingine za Afrika na kuhimiza ushirikiano wa kimataifa katika kukuza afya na lishe ya wanawake, watoto wachanga, watoto na vijana.

Mama Salma ambaye alihutubia kongamano hilo kwa lugha ya Kiswahili, alipongeza mjadala wa mkutano huo na kushauri maazimio ya kongamano hilo kutumika kwa nchi zote za Afrika kukabiliana na changamoto za lishe zinazoikabili Afrika kufikia malengo ya SDG katika nyanja za afya na lishe.

OAFLAD ni Taasisi ya Wanawake Wake wa Marais wa Afrika kwa Maendeleo iliyoanzishwa mwaka 2002 kwa wake wa marais wa Afrika kuunda taasisi hiyo kwa lengo la kuwa na sauti ya pamoja, kusaidia wananchi wa Afrika kwa wake hao kutumia nguvu yao ya ushawishi na nafasi zao.

Lengo lingine ni kusaidia huduma za afya na uwezeshaji wa wanawake na vijana kwa kukusanya rasilimali na kuendeleza ushirikiano na wadau wote katika ngazi zote.

Mama Salma na ujumbe wake walirejea Tanzania mwishoni mwa wiki.



Mke wa Rais mstaafu, Salma Kikwete ambaye ni Mbunge waMchinga (kushoto), akiwa katika maonyesho ya wajasiriamali wa Burundi kwenye Kongamano la 3 la Viongozi Wanawake barani Afrika, ambao ni wake wa marais lililoandaliwa na Taasisi ya OAFLAD jijini Bujumbura, Burundi, kujadili changamoto za afya na lishe kwa wanawake, watoto na vijana balehe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Meya Mnyonge: Uko umuhimu kutolewa elimu ya mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

MEYA wa Manispaa ya Kinondoni, Songolo Mnyonge, ameeleza umuhimu wa kutolewa elimu ya uwekezaji kwa makundi maalum hasa wanawake wanapochukua mikopo ili waweze kuendelea kiuchumi.

Alisema kinamama wengi wanapochukua mikopo ya asilimia 10 hawazingatii mambo ya msingi badala yake wanapeleka kwenye biashara ya kutunzana na kununua vijora.

Meya huyo alitoa mfano katika manispaa yake ambayo imekopesha kinamama jumla ya Shilingi bilioni mbili, lakini wanapokwenda kuwatembelea kuona mitaji waliowekeza wanagundua wengi fedha hizo zinaishia kwenye mambo yasiyo na msingi.

"Mkopo haurudishwi, biashara aliyotaka kufanya haifanywi, anazidi kudidimia kiuchumi," alisema Myonge.

Alisema hayo juzi wakati akizindua Bodi ya Wajumbe wa Taasisi ya Waandishi wa Habari Wanawake wanaotetea haki ya Mwanamke na Mtoto (TAWOJAC).

Taasisi hiyo ilisajiliwa rasmi mwaka 2021 ikiwa na lengo la kutetea haki ya mtoto, msichana na mwanamke katika kupambana na ukatili wa aina zote.

Meya Mnyonge, alisema taasisi hiyo ina uwezo wa kuwasaidia wanawake haki ya usawa katika jamii na siasa ili wasukume gurudumu la maendeleo kwa taifa.

Aliwakumbusha wanaume kuwashika mkono kinamama ili kuwasaidia mapambano ya kumlea mtoto wa kike dhidi ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

Alisema mambo yanayotokea katika jamii hayawezi kufumbiwa macho, lazima yakemewe na wa kuyakemea ni mwanamke mwenyewe.

"Ukienda kwenye bendi utaona wanaume wamevaa nguo nzuri za kujisitiri, lakini mwanamke anavalishwa nguo zisizo staha, hili lazima wanawake wenyewe walikatae na kulikemea. Mwanamke kataa kujidhalilisha ili usidhalilishwe," alisisitiza.

Akizungumzia taasisi hiyo, Mkurugenzi Mwezeshaji, Neema Nchimbi, alisema pamoja na kulinda na kutetea haki ya mtoto na mwanamke, inajishughulisha na miradi ya kusaidia jamii kwa kushirikiana na mashirika mengine yanayofanya shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii.

Bodi ya TAWOJOC inaongozwa na Mwenyekiti wake, Nicholas Mgaya, Makamu Mwenyekiti, Asha Mtwangi na wajumbe katika bodi hiyo ni Evarist Mwitumba, Benjamin Mwandete, Dk. Flora Minja, Wallace Mfuko na Beatrice Bandawe.



# Jela miaka 12 kwa kumuua mkewe

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu mkazi wa Mtaa wa Kilimahewa Katoro, Frack Salvatory (30) kifungo cha miaka 12 jela kwa kosa la kumuua mke wake, Elizabeth Paul.

Mshtakiwa huo alifikishwa mahakamani kwa madai ya kunyonga mke wake kwa kutumia kitenge na kufariki dunia papo hapo kisha akamchukua na kwenda kumtupa pembeni mwa mto.

Hukumu hiyo ilitolewa Ijumaa iliyopita na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Bukombe mwenye mamlaka ya ziada, Ainawe Moshi, baada ya mshtakiwa kukiri kosa la kumuua mke wake bila kukusudia.

Baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa, Hakimu Moshi alimwambia Wakili wa Serikali Flora Massawe amsomee maelezo ya awali.

Akisoma maelezo hayo, Massawe alidai kuwa Januari 12, 2021 katika mtaa wa Kilimahewa Katoro, mshtakiwa alikuwa anadai hati ya kiwanja chake ambacho mke wake alikuwa amekificha.

Massawe alidai kuwa baada ya mke wake kudaiwa hiyo hati, alimfukuza mshtakiwa ambaye alikuwa anaishi kwa mke wake ambaye kwa sasa ni marehemu na kwenda kuishi sehemu nyingine.

Alidai kuwa siku ya tukio hilo, mshtakiwa alimwita mke wake sehemu ya pori ili wazungumza juu ya hati ya kiwanja na baada ya kufika, alimvamia na kumvua nguo zote kisha akachukua sketi na sidiria na kumfunika mdomo.

Mwanasheria huyo alidai kuwa baada ya hapo alichukua kitenge na kumnyonga shingoni na kufariki dunia papo hapo na baada ya kuona mke wake amefariki dunia, alimburuza hadi pembeni mwa mto na kumtupa.

Pia alidai kuwa baada ya kumtupa, aliondoka na kwenda nyumbani kwa mke wake na muda mfupi baadaye alikwenda kituo cha polisi kutoa taarifa ya kupotea kwa mke wake.

Polisi baada ya kupata taarifa hizo, alidai kuwa walianza kufanya uchunguzi wa tukio hilo na baada ya siku mbili walikuta mwili wa marehemu ukiwa pembeni mwa mto. Waliuchukua mwili wa marehemu pamoja na mshtakiwa hadi kituo cha polisi na mshtakiwa huyo alipohojiwa alikiri kumuua kwa kumnyonga na kitenge alichokuwa amevaa mke wake.

Alidai kuwa baada ya kukamatwa kwa mshtakiwa, polisi waliendelea na uchunguzi wa tukio hilo na baada ya kukamilika walimpeleka mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Baada ya Wakili wa Serikali kumaliza kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali, Hakimu Moshi alisema mahakama inamtia hatiani kwa kukiri kosa bila ya kulazimishwa na mtu.

Kabla ya Hukumu kutolewa, Hakimu Moshi alimtaka mshtakiwa ajitetea ili mahakama impunguzie adhabu.

Mshtakiwa huyo akiongozwa na Wakili wa Kujitegemea, Elizabeth Msechu, aliomba mahakama hiyo impunguzie adhabu kwa madai kuwa bado ni kijana mdogo na ni nguvu kazi ya taifa.

Msechu pia alidai kuwa mteja wake alikuwa akidai hati yake ambayo ni mali yake na pia alikuwa baba mzuri wa watoto wa marehemu na ana watoto wawili wanamtegemea.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Masawe aliomba mahakama itoe adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili kukomesha vitendo vya kikatili na vya kinyama dhidi ya wanawake.

Hakimu Moshi alitupilia mbali utetezi huo na kusema kitendo ulichokifanya mshtakiwa ni cha kikatili, hivyo mahakama inamhukumu kutumikia kifungo cha miaka 12 jela ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia kama yake.

Hata hivyo, Hakimu Moshi alisema kuna upande ambao haujaridhika na hukumu hiyo, rufani iko wazi.



Mafundi wakijenga njia ya waenda kwa miguu inayopita pembeni mwa daraja la magari eneo la Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam juzi ili kuepusha kuingiliana na vyombo vya moto. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TCB yaagizwa kuzalisha miche milioni 20

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeiagiza Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), kuhakikisha inazalisha miche 20,000,000 ya kahawa kwa mwaka kwa ajili ya kukuza uzalishaji wa zao hilo nchini.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki mkoani Kagera na Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, wakati akizindua ugawaji wa miche 800,000 ya kahawa aina ya Robusta katika Kijiji cha Karenge, Wilaya ya Kyerwa. Miche hiyo imezalishwa na Kampuni ya JJAD Kagera Farmers na lengo la kampuni hiyo ni kuzalisha miche milioni tatu ya kahawa aina ya Robusta kwa mwaka.

Naibu Waziri aliwataka wakulima watakaonufaika na miche hiyo itakayotolewa bure, waipande kwa njia za kisasa na kuisimamia kwa karibu ili kutoa mavuno bora na kufanikisha malengo yaliyokusudiwa na bodi ya kahawa na serikali.

"Bodi tumewapa malengo ya kuzalisha miche milioni 20 kwa mwaka nashukuru kwa kuishirikisha sekta binafsi leo hii mko na JJAD Kagera Farmers mnayefanya naye kazi hapa. Tunataka kuona matokeo chanya baada ya miaka mitatu tukija tuone uzalishaji wa kahawa umeongezeka," alisema.

Mavunde pia aliitaka TCB kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji kwa wakulima wote wanaopewa miche bora ili kuongeza tija na uzalishaji.

Alisema dhamira ya serikali ni kuona mkulima wa kahawa ananufaika na kilimo anachokifanya na kuchangia katika upatikanaji wa ajira na kuongeza pato la nchi.

"Mfano mzuri wa hili ni manufaa ya mfumo mpya wa kuuza kahawa kwa njia ya mnada mkoani Kagera ambao umeleta ufanisi mkubwa ikiwa ni pamoja na kuongeza bei na kipato kwa mkulima.

Hakuna jambo la muhimu sana kwenu ambalo litarahisisha sana serikali na wadau wote kutoa huduma kwenu kama tukiwatambua hivyo ninawaomba mtoe ushirikiano ili muweze kusajiliwa, mtambulike mpo wangapi ili kupewa huduma stahiki kulingana na mahitaji yenu," alisema.

Pia Mavunde aliiagiza Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na sekretarieti za mikoa kuhakikisha wanaandaa mwongozo wa ugawaji wa miche kwa wakulima ambao utaonesha vigezo vya nani atagawiwa miche na kuainisha majukumu ya wadau wote wanaohusika katika zoezi la uzalishaji, ugawaji na usambazaji wa miche.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa JJAD, Dk. Albert Katagira, alisema ili kufikia malengo shughuli mbalimbali zinatekelezwa ikiwamo kuzalisha miche bora ya kahawa, kuimarisha ugani na kwamba kampuni hiyo kwa msimu wa mwaka 2021, ilizalisha miche 11,300,000 na kusambazwa kwa wakulima.

Estavia Henry ambaye ni mmoja wa wakulima hao alizishukuru JADD Kagera Farmers na Bodi ya Kahawa kwa kutoa miche hiyo kwani itawapa wakulima motisha wa kuboresha kilimo.

"Hili zao linatusaidia sana kiuchumi tunasomesha watoto na kupata mahitaji yetu mbalimbali kwa hiyo uamuzi huu ni wa kupongezwa," alisema.

# Madereva wa serikali waonywa kuhusu ulevi

**Na Said Hamdani,** LINDI

KATIKA kuhakikisha ajali za barabarani zinapungua, madereva wa serikali mkoani hapo wameonywa kuhusu tabia ya kutumia kilevi wakiwa kazini na kutakiwa kuacha vitendo hivyo mara moja.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Madereva Wilaya ya Kilwa, Bakari Maulidi, alipopewa nafasi ya kutoa neno wakati wa ufungaji wa utoaji huduma ya upimaji afya kwa madereva 300 wa mkoa uliofanyika katika Hospitali ya Rufani ya Sokoine, mjini hapo.

Akiwasilisha changamoto zinazowakabiri mbele ya mgeni rasmi, Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi, Ngusa Samike, Maulidi alisema kutokana na majukumu waliyo nayo ya kuendesha vyombo vya moto barabarani ni vyema wakajiepusha na utumiaji kilevi hasa pombe na uvutaji sigara.

Maulidi alisema itakuwa busara kwa madereva wenzake wakiachana na matumizi ya kilevi ili kulinda majukumu yao wanapokuwa barabarani na usalama wa watu na vyombo wanavyoviendesha.

"Mimi mwenzenu nimeacha vyote hivyo, yaani pombe na sigara. Baada ya siku moja kukaa na kufikiri sana, nikaona hakuna faida ninayoipata zaidi ya upuuzi tu," alisema Maulidi.

Alisema siku aliyoamua kuachana na kilevi, alikwenda bar na kununua bia tatu na pakiti moja ya sigara na kumwomba Mungu kuwa kuanzia siku hiyo, hataki kushiriki tena ulevi kisha kuchukuwa chupa na kuzivunja na sigara kuzifinya.

Tangu achukue uamuzi huo, alisema huu ni mwaka wa tatu hajaonja pombe wala sigara na sasa anafanya majukumu yake bila shida na hakuna kero ya harufu ya sigara kwa anaowabeba.

Awali, ilielezwa na Mkuu wa Usalama Barabarani mkoani Lindi, Peter Magayane, kuwa kuanzia Januari, mwaka jana, hadi Oktoba 13, mwaka huu, ajali 21 zinazohusisha madereva wa serikali zimetokea, huku magari ya halmashauri yakitajwa kuongoza.

# TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA USAFIRI WA NDEGE KWA WAFANYAKAZI KUMBUKUMBU NA: 10007995

Kampuni ya Mafuta Ghafi ya Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, ambayo ni Kampuni ya mafuta na gesi, inaalika kampuni au taasisi zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma ya usafiri wa ndege kwenda kwenye Mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika mashariki.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka mashariki mwa pwani ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa waTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Huduma za Usafiri wa Ndege:

- Sifa Husika za ndege: Ijulikanayo kitaalamu kama fixed wing, Marubani 2, Injini pacha, Iwe na injini yenye turubo ya kusukuma propela , iwe inazingatia vigezo vya Mamlaka ya Kimataifa ya Usafirishaji wa Anga.
- Viwanja vya Ndege: Dar-es salaam/Tanga au mahali pengine penye kiwanja cha ndege (Kiwanja chenye moramu).
- Ratiba: Safari 2 za Kwenda na kurudi kwa wiki kwenye viwanja vya ndege vilivyotajwa. Safari za kawaida za ndege za abiria zinaweza kuruhusiwa baadae.
- Ratiba ya kuanza: Inakadiriwa kuanza tarehe 1 Desemba 2022.
- Mshahara: Unajumuisha viwango vyote vya malipo kwa kila saa ya kuruka angani.
- Muda: Mwaka mmoja ingawa unaweza kuongezeka

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zanaalikwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kanzi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa konesha nia.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa makampuni ya ndani.
- Uzoefu, utendaji na uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu katika kiwango kikubwa nchini Tanzania, kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za mwaka husika.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi hii.
- Leseni ya biashara kutoka nchii husika inayothibitisha kufanya kazi hii.
- Vyeti vya ubora wa ndege.
- Wasifu wa marubani na marubani wasaidizi pamoja na wahudumu wengine watakaohusika katika kutoa huduma, ikiwa ni pamoja na vyeti vya lazima vya kila mhudumu, viwango vya elimu, ushahidi wa mafuzo ya mara kwa mara.
- Uthibitisho mwingine wowote wa Kampuni, vibali na leseni.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Haki za Binandamu.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**) mnamo au kabla ya Tarehe **1 Novemba 2022** saa **12:00 jioni** saa za Afrika Mashariki (EAT). Kichwa cha Barua pepe kiwe **1007995.**

Maombi yote yakuonesha nia yasizidi kurasa **10 hadi 20.**

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni) ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA).

217107202

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
### TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI

## TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'

**1. UTANGULIZI:**

Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Makao makuu ya Taasisi yapo katika Manispaa ya Morogoro kilipokuwa Chuo cha Ujenzi. Taasisi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha kozi maalum ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe kwa vikundi vya Wanawake na Vijana kuanzia Tarehe 21 Novemba hadi Tarehe 17 Disemba, 2022. Mafunzo haya yatafanyika katika Tawi la Taasisi lililopo Mkoani Mbeya Wilaya ya Rungwe.

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi maalumu ya vikundi vya Wanawake na Vijana ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Kumi (4)**<br>21/11/2022 – 17/12/2022 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya) Wilaya ya Rungwe** |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**

Washiriki watajifunza maada mbali mbali kuhusu ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Kozi imelenga kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kufanya ukarabati na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hususani matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent maintenance'. Aidha, itahusisha mafunzo ya Ujenzi wa Makalvati, Teknolojia ya Udongo na Teknolojia ya Zege. Aidha, maada shirikishi kuhusu utaratibu wa kufungua kampuni kwa makundi maalum, utaratibu wa kujaza vitabu vya zabuni zitafundishwa.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**

Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) kwa wiki moja (1) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site') kwa muda wa wiki tatu (3).

**4. MALENGO YA KOZI**

Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO :**

a) Makundi maalum ya Vijana na Wanawake,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
d) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**

Lugha itakayo tumika katika kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**

Kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana

i. Mshiriki atakaye jitegemea huduma za chakula na malazi, atalipa ada kiasi cha Tsh. 350,000.00; na
ii. Mshiriki atakayepata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo atalipa ada kiasi cha Tsh. 500,000.00

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia 'control number' itakayotolewa kwa mtu yeyote atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Aidha, ada ilipwe kabla ya wiki mbili ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**

Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi hii hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI**
**MKUU WA CHUO**

| | |
|---|---|
| **Institute of Construction Technology**<br>**ICoT,**<br>**S.L.P 1957, MBEYA.**<br>**Simu : 025 295 7484/5**<br>**: 0764775354/0769317404**<br>**Nukushi : 025 295 7486**<br>**Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com** | **Institute of Construction Technology**<br>**ICoT,**<br>**S.L.P 963,**<br>**MOROGORO.**<br>**Simu : 023- 2935229/023- 2935226**<br>**: 0787059555 /0753035348**<br>**Nukushi : 023-2935227**<br>**Barua pepe : mwti@morogoro.net** |

217109402

# Mbunge ataka shule binafsi kuacha kupandisha holela ada

**Na Joseph Mwendapole**

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Dk. Thea Ntara, amezitaka shule binafsi kuacha tabia ya kupandisha ada holela kwa kuwa kufanya hivyo ni kuwanyima fursa watoto wengine wa Kitanzania kupata elimu.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 12 ya kidato cha nne ya Shule ya Brilliant iliyoko Mbezi kwa Msuguri, Dar es Salaam.

Alimpongeza Mkurugenzi wa Shule hiyo ambaye ni Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Dk. Jasson Rweikiza, kwa uwekezaji mkubwa alioufanya kwenye sekta ya elimu, hivyo kusaidia jitihada za serikali katika kuinua elimu.

"Nimeambiwa kwamba pamoja na kupanda kwa gharama za maisha, ninyi kwa miaka minne mfululizo hamjapandisha ada hata kidogo. Nawapongeza sana lakini nataka shule zingine ziige mfano wa Brilliant kwa sababu mnatoa huduma zaidi kuliko kuangalia biashara," alisema.

Aidha, mbunge huyo alisema mbali na kusaidia serikali kuboresha kiwango cha elimu lakini uwekezaji huo mkubwa umesaidia pia kupunguza tatizo la ajira kwa kuwa amefanikiwa kuajiri wafanyakazi wengi kuanzia watumishi walimu, wapishi, walinzi madaktari na wauguzi.

"Kwenye risala nimesikia kwamba mlikuwa na nidhamu na mmefanya vizuri sana kwenye mitihani ya ustahimilifu kwa kupata daraja la kwanza 49, daraja la pili 40 na watatu daraja la tatu sasa kwa matokeo haya ni imani yangu kwamba mtafanya vizuri sana kwenye mtihani wa mwisho mnaotarajia kuufanya hivi karibuni," alisema.

Mbunge huyo alimpongeza Ofisa Elimu Manispaa ya Ubungo na Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwa usimamizi wao ndio umeiwezesha shule hiyo kuendelea kufanya vizuri kitaaluma na kupanda madaraja kiwilaya, kimkoa na kitaifa.

Pia aliwakumbusha wazazi na walezi kutimiza wajibu wao wa kulipa ada kwa wakati ili kuiwezesha shule hiyo kuendelea kufanya vizuri kwa kupata mahitaji muhimu.

Dk. Rweikiza kwa upande wake aliahidi kuwa shule hiyo itaendelea kutoa elimu bora kwa gharama nafuu ili kuwawezesha Watanzania wengi kumudu kuwapeleka watoto wao shule.

"Ingawa gharama za maisha zimepanda zikiwamo gharama za uendeshaji lakini hatujapandisha ada kwa miaka minne mfululizo na tutaendelea kutopandisha ada ili Watanzania wengi wamudu kupata elimu bora," alisema Dk. Rweikiza.

Naye Mkuu wa Shule hiyo, Edrick Philemon, alisema kwenye matokeo ya kidato cha nne mwaka 2020 wanafunzi 13 walipata daraja la kwanza, wanafunzi 26 daraja la pili na wanafunzi 27 daraja la tatu.

Alisema kwa mwaka 2021 wanafunzi 18 walipata daraja la kwanza, wanafunzi 38 daraja la pili, wanafunzi 18 daraja la tatu ambayo ni mafanikio makubwa kwa shule.




Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Barrick Gold Corporation, Mark Bristow, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu mipango ya kampuni hiyo kupanua shughuli zake nchini, North Mara mwishoni mwa wiki, (katikati) Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mara, Yahya Nawanda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafariki katika matukio tofauti

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WATU wawili wamefariki dunia katika matukio tofauti mkoani Ruvuma likiwamo la Johari Makunguru, maarufu kwa jina la Kaburu (42), Mkazi wa Mtaa wa Londoni Manispaa ya Songea, kuuawa kwa kushusiwa kipigo kisha kuchomwa moto kwa tuhuma ya wizi wa vitu mbalimbali, yakiwamo magodoro.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Amini Mahamba, alisema juzi kuwa katika tukio la kwanza, Oktoba 20, mwaka huu, majira ya saa 3.30 asubuhi eneo la Mtaa wa Londoni, Makunguru aliuawa baada ya kupigwa sehemu mbalimbali za mwili kisha kuchomwa moto kwa kutumia tairi la gari na kundi la watu wenye hasira kali.

Mahamba alisema siku hiyo kabla ya tukio, majira ya saa 1.30 asubuhi Ephraim Mikao (33) mkazi wa Lizaboni, akiwa nyumbani kwake ghafla alimwona Makunguru akiwa amebeba panga huku akiwa na subufa aina ya Aborder pamoja na twitter mbili.

Alisema baadaye Mikao aliamua kumsogelea Kaburu kwa lengo la kutaka kumwuliza vitu hivyo amevitoa wapi na anavipeleka wapi na ghafla Kaburu alipomwona, alitoa panga kisha alianza kumtishia na baadaye kukimbia huku akiwa amebeba vitu hivyo.

Mikao, alisema baada ya kuona Makunguru anakimbia alipiga kelele za mwizi ndipo kundi la watu lilijitokeza na kuanza kumkimbiza kisha kumkamata na kumshushia kipigo na kumkatakata na vitu vyenye ncha kali. Baada ya hapo walichukua gurudumu na kumvalisha kisha kuwasha moto na kumsababishia kifo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Londoni, Joseph Zawamba, alikiri kuwa Makunguru kwa muda mrefu alikuwa akilalamikiwa kuwa ni mwizi na alikuwa na mtandao wa wezi katika manispaa ya Songea.

Alisema ofisi yake baada ya kupata taarifa ya tukio hilo, waliwasiliana na kituo kikuu cha polisi mjini Songea na baadaye askari walifika eneo la tukio wakiwa wameongozana na daktari toka Hospitali ya Rufani ya Mkoa ambaye alithibitisha kuwa Makunguru alikuwa ameshafariki dunia baada ya kuwa na majeraha makubwa ya moto mwilini.

Katika tukio lingine, Kamanda Mahamba alisema Oktoba 20, mwaka huu, majira ya saa 2:00 asubuhi katika kitongoji cha Jabali Kijiji cha Mbungulaji wilayani Tunduru, Issa Selemani (76) alifariki dunia baada ya kuvamiwa na kundi la tembo ambao walimkanyaga hadi kusababisha kifo chake papo hapo.

Alisema Selemani akiwa anatoka nyumbani kwake kwenda shambani, alipofika eneo la Mbungulaji alikutana na kundi tembo ambao walimvamia na kumjeruhi tumboni kabla ya kufikwa na mauti.

# VETA, Uholanzi zaingia mkataba mafunzo ufundi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Singida, Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) na Shirika la Dusabikane la Uholanzi, wameingia makubaliano ya kuanzisha mafunzo ya kozi mpya ya umeme wa jua kwa wanafunzi wa vyuo hivyo. Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Fihili Challange, akizungumza jana kwenye mahafali ya kwanza ya wahitimu wa kozi hiyo, alisema VETA Singida ndiyo itakuwa kitovu cha kuandaa wawezeshaji wa kozi ya mafunzo ya umeme wa jua ndani na nje ya VETA.

Alisema katika kuhakikisha mafunzo hayo yanafanikiwa, Busabikane/CCHO imetoa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 136 na VETA imetoa Sh. milioni 15.3 ambapo Chuo cha Arusha Technical College watatoa utaalamu na ushauri.

Challange alisema hadi sasa chuo kimefanikiwa kutoa mafunzo kwa wawezeshaji 13 ambao ni walimu waliotoa mafunzo kwa wanafunzi 20 ambao wamehitimu kwa mara ya kwanza na kutunukiwa vyeti katika Chuo cha VETA Singida.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Muragili, alisema programu hiyo imefika wakati mwafaka na sasa hivi dunia nzima inazungumzia suala la nishati ya umeme wa jua ambao unasaidia sana kutunza mazingira.

"Katika mipango ya umeme serikali yetu imeshatangaza programu ya kuhakikisha katika miaka michache tunakuwa na umeme wa jua na umeme wa upepo ambao utaingizwa katika gridi ya taifa," alisema.

Muragili alisema bahati nzuri katika tafiti zote zilizofanyika mkoa wa Singida umeonekana kuwa upepo mwingi na jua linalowaka muda mrefu hivyo kuweza kuzalisha umeme wa kutosha. Alisema kutokana na hali hiyo tayari serikali ilishatangaza mchakato wa kutafuta watu wa kuwekeza kwenye uzalishaji wa umeme wa upepo na umeme wa jua na zipo kampuni kadhaa zilizoomba zabuni hiyo na Halmashauri ya Manispaa ya Singida ilishatenga eneo maalum la kuzalisha umeme wa jua.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ambaye alikuwa mgeni rasmi alisema matumizi ya umeme wa jua yanasaidia sana kutunza mazingira kwa sababu haina vitu vinavyotembea na hivyo kutoharibu hewa ya ukaa kama nishati nyingine.

Serukamba alisema umeme wa jua pia utasaidia kupunguza bili za umeme kwa wateja kwasababu baadhi ya vifaa kama taa na redio vinaweza kutumia umeme wa jua na jiko na pasi vikatumia umeme wa gridi.

Mkuu wa Mkoa aliwataka wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao katika vyuo vya VETA ili wakafundishwe mafunzo ya kozi ya umeme wa jua ambao utatoa ajira kwao.



# Watu wenye ulemavu 261 wanufaika na ajira mpya

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amesema watu wenye ulemavu wamenufaika na ajira mpya 261, kati ya ajira 9,800 zilizotolewa hivi karibuni.

Amesema Ofisi ya Waziri Mkuu iliwapa upendeleo kundi hilo kwa kuwa inatambua na kuthamini mchango wao.

Aliyasema hayo katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Fimbo Nyeupe Duniani, ambayo kitaifa kwa mwaka huu ilifanyika Wilaya ya Babati, mkoani Manyara. Katambi alimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

"Chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, ajira hizo nilizozitaja ndizo zilizotolewa kwa wenzetu wenye ulemavu. Na kati ya hizo, ajira 61 zilitolewa kwa walemavu wasioona, ambapo wanaume ni 48 na wanawake 13,"alifafanua Katambi.

Alizikumbusha taasisi za serikali zinapotangaza ajira, zihakikishe wana waajiri watu wenye ulemavu, kwa kuwa ni takwa la kisheria ambalo lipo kwenye Sheria ya Walemavu Namba 9 ya Mwaka 2010, ambayo inawataka kila watu wanaowaajiri waajiri asilimia tatu ya watu wenye ulemavu.

"Hivi sasa uko wepesi wa kupata vifaa vya wenye ulemavu, kwa sababu kodi ya vifaa hivyo imepungua na mkitaka kuamini hilo, muulizeni Mwekezaji wa Kiwanda cha Malt Super Brands Limited kinachozalisha bidhaa mbalimbali, David Mulokozi, ambaye ametuunga mkono serikali na wadau mbalimbali wa haki za binadamu, baada ya kuchangia fimbo nyeupe 500,"alisema.

Kutokana na utashi huo wa Mulokozi, Naibu Waziri Katambi, alimshukuru mwekezaji huyo akisema alichokifanya ni jambo zuri kwa kuwa ametoa sadaka kwa Mungu, akitambua na kutoa mahitaji kwa watu wasioona.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda hicho, David Mulokozi, alisema wao hawana mengi wanafanya kwa vitendo, ndiyo maana waliona kilele cha maadhimisho hayo, jamii ya watu wenye ulemavu wa kutokuona, wasiondoke bila kitu.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wasioona nchini (TLD), Deodageja Manonga, alisema maadhimisho ya siku hiyo ni utambulisho kwa wasioona huku akiomba wazazi kuwapeleka watoto shule wasioona kwa kuwa kutokuwapeleka ni kuwanyima haki yao ya elimu.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Sightsavers, Godwin Kabalika, alisema wanasaidia kupambana na upofu unaoweza kuzuilika na wanatetea haki za watu wenye ulemavu, wanafanya kazi mikoa ya Manyara, Lindi, Ruvuma, Singida na Dodoma.

# Ahukumiwa miaka 30 jela kwa kumbaka kikongwe

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, imemhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 jela mkazi wa Kijiji cha Endadosh, Paschal Niki (26), baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka kikongwe mwenye umri wa miaka 87.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario, baada ya kupitia mwenendo wa shauri hilo na kisha kusikiliza ushahidi wa upande wa mashtaka na ule wa upande wa utetezi.

"Mshtakiwa ametiwa hatiani baada ya mahakama hii kujiridhisha pasipo shaka kwamba ushahidi ulitolewa na mashahidi wa upande wa mashtaka katika kesi hii wameweza kuunganisha na kuijenga kesi nzima.

Bila shaka yoyote, nimeridhika kwamba mshtakiwa alikutwa akifanya mapenzi na bibi huyo, wakati akiwa anachunga mifugo na bibi akikata majani,"alisema.

Aidha, Hakimu Kimario, alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 130 (1), (2) (e) na kifungu 131 (1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2019. Kwa mujibu wa Hakimu Kimario, mshtakiwa alifanya kosa la kisheria kwa makusudi kwa kumlazimisha kikongwe huyo kufanya naye mapenzi kichakani, bila ya kuridhiana.

Alisema wakati mshtakiwa akiendelea kufanya ukatili huo, ndugu yake mmoja na kikongwe huyo aliwafumania na ndipo alipokwenda kutoa taarifa kwa ndugu zake wengine ambao walishirikiana na wananchi kumkamata mshtakiwa huyo.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi sita ambao wote walithibitishia mahakama kuwa mshtakiwa alimbaka bibi huyo na upande wa utetezi ulikuwa na shahidi mmoja ambaye ni mshtakiwa.

Katika hati ya mashtaka, ilidaiwa na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Emmanuel Jumbe, kwamba mshtakiwa Niki, alitenda kosa hilo Machi 30, mwaka huu, huko Endadosh, majira ya saa 5:00 asubuhi.

Kabla ya kusomwa kwa hukumu hiyo, Mwendesha Mashtaka huyo, aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine katika jamii wanaofanya vitendo hivyo kwa ukatili dhidi ya wengine.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Patrobas Katambi (kulia), akipokea moja kati ya fimbo nyeupe 500 za watu wasioona zilizotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Malt Super Brands Ltd, David Mulokozi, kwenye maadhimisho ya Siku ya Fimbo Nyeupe Duniani Mjini Babati mkoani Manyara juzi, (wa pili kulia) Mkuu wa Mkoa huo, Charles Makongoro Nyerere. **PICHA: GIFT THADEY**

# EWURA yaanza kuwasajili kidijitali mafundi umeme

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeanza kutekeleza mkakati wake maalum wa kuwatambua na kuwasajili kidijitali mafundi umeme mitaani.

Pia imeanza kuwapa leseni za kufanyia kazi ili kuwakabili watu waliovamia fani hiyo bila ya kuwa na taaluma.

Meneja wa EWURA wa Kanda ya Kaskazini, Lorivii Long'idu, alisema mkakati huo unalenga pamoja na mambo mengine kukutana na kutoa elimu kwa wanafunzi wanaosomea fani ya umeme katika vyuo ili kuwakumbusha wajibu wao watakapohitimu mafunzo yao, kuifahamu vyema mamlaka hiyo.

Long'idu alikuwa akizungumza mwishoni mwa wiki na wanafunzi wa Chuo cha Ufundi cha Arusha, ikiwa ni mwendelezo wa mkakati wa EWURA kutekeleza mkakati huo wa utoaji wa leseni na kuitangaza mamlaka hiyo.

"Sisi tumewafuata hawa mafundi wa mjini kuwaelimisha wajue utaratibu wa kupata leseni na watakapomaliza masomo yao, waingie mtaani na kuanza kufanya kazi na tutaendelea kufanya shughuli hii kwa kuvifikia vyuo vingi zaidi.


"Tathimini yetu kama mamlaka inaonyesha kuwa, kwa sasa nchini kuna uhitaji mkubwa wa mafundi umeme kutokana na wingi wa ujenzi wa miradi ya umeme inayoendelea kutekelezwa na serikali kwenye maeneo mbalimbali."

Alisema serikali imewekeza nguvu kuhakikisha huduma ya umeme inafika katika vijiji vyote nchini, hivyo kutakuwapo na uhitaji wa mafundi hao watakaokwenda kufanya kazi sehemu hizo.

"Tumekuja kuwapa elimu mfahamu matakwa ya kisheria, ikiwamo namna ya kuomba leseni ambazo tunatoa kwa watu wote, wanaofanya kazi ya kufunga mifumo ya umeme ili waweze kutoa huduma hizo kwa wananchi. Tunatoa leseni kwa mafundi, kwa ajili ya kuhakikisha kazi hiyo inafanywa na waliosomea taaluma hiyo,"alisisitiza.

"Natoa onyo kwa vishoka wote kuacha mara moja kujishughulisha na kazi ambazo hawajazisomea, rai yangu waende kwenye vyuo vya ufundi vilivyoko karibu yao, wakajisajili kwa lengo la kujifunza kwa kuwa nchi inaongozwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na utaratibu hivyo wanapaswa kuzingatia,"alisema.

Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha, Musa Chacha, akizungumza katika mafunzo hayo alisema chuo hicho ni miongoni mwa vyuo nchini vinavyozalisha vijana waliobobea katika sekta ya umeme.





## UNICEF: Vita dhidi ya vitendo vya ukatili kijinsia bado mbichi

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF), limesema vita dhidi ya ukatili wa kijinsia nchini ina safari ndefu ya kupata suluhisho, kwa kuwa mifumo haijaweka sawa mkakati wa kuikabili, ikiwamo kuitishwa kwa mjadala wa kitaifa.

Mtaalamu wa ulinzi na usalama wa mtoto kutoka UNICEF, Victoria Mgonela, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye Jukwaa la Haki za Mtoto kutoka taasisi za serikali na sekta binafsi waliokutana jijini Arusha.

Alisema kuendelea kukithiri kwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa watoto ni ishara kwamba ufumbuzi wa tatizo hilo bado haujapatikana na nguvu zaidi zinahitajika.

"Haya matukio ya unajisi kwa ujumla kama ulawiti na ubakaji, naona kabisa kwamba kuna haja ya kufanyika kwa mijadala zaidi. Pia nguvu kubwa ya ushirikishaji na utoaji wa elimu katika jamii juu ya vitendo hivyo inapaswa kufanywa.

"Kuna mambo mengi ya kufanya kwa ushirikiano ili kuhakikisha kuwa ufumbuzi wa tatizo hili la ukiukwaji wa haki za watoto unapatikana. Wapo wadau wengi wanaoweza kushiriki, kimsingi kuna rasilimali watu ya kutosha ikiwamo jamii yenyewe, wataalamu na wadau ambao sitaki kuamini kuwa wote hawa wameshindwa. Lazima tujiulize tunakwama wapi?"

Mkurugenzi anayeshughulikia Msaada wa Kisheria katika Wizara ya Katiba na Sheria, Felister Joseph, alisema ni kweli vita hiyo bado ni mbichi, lakini serikali na wadau wa haki za binadamu wamechukua hatua mbalimbali.

Aidha, alitaja baadhi ya hatua zilizoanza kuonyesha tija kuwa ni pamoja na kuanzishwa kwa majukwaa ya haki za watoto yanayowakutanisha pamoja wadau wengi wanaoshughulikia tatizo hilo.

Alisema jambo ambalo kwa sasa linahitaji kufanyiwa kazi zaidi na serikali na wadau, ni kiini cha tatizo ambacho kiko kwenye jamii yenyewe kukosa utashi na kushiriki zaidi kuongeza ukatili badala ya kuvitokomeza.

"Taarifa nyingi na hata matukio yanaonyesha kuwa watoto wengi wanafanyiwa ukatili na watu wa karibu wakiwamo ndugu, wazazi na watu wa karibu. Hili ni tatizo kubwa ambalo kama halitapata ufumbuzi, basi itakuwa vigumu sana kumaliza tatizo hili,"alisisitiza Felster.

Mratibu wa Mtandao wa Wasaidizi wa Kisheria Tanzania, Tollbati Mmasi, alisema ushirikishaji wa makundi muhimu katika jamii wakiwamo viongozi wa dini, mila na wengine wenye ushawishi katika jamii bado ni mdogo.

# Hospitali ya Kibong'oto yaanza kuwakinga madaktari wake

**Na Anjela Mhando,** SIHA

HOSPITALI ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto iliyoko Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, imeanza kuchukua hatua za kuwalinda wataalamu wake na watumishi wengine dhidi ya magonjwa ambukizi.

Hivyo imeanza kwa kuwabana kuchanjwa chanjo ya homa ya ini na kuwapima magonjwa mengine yanayoweza kuhatarisha maisha yao wakiwa kazini.

Mpango huo wa kuwafanyia uchunguzi wa afya na kisha kuwapa kinga ya magonjwa yasiyoambukiza na yale yanayoambukiza unatekelezwa kwa siku tano.

Akizungumzia mpango huo jana, Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Leornad Subi, alisema wameamua kuchukua uamuzi huo kwa sababu wataalamu wengi hasa madaktari na wauguzi huathirika na hata wengine kupoteza maisha wakiwa kazini kutokana na kukosa kinga.

"Homa ya ini ni miongoni mwa magonjwa yanayoenea kwa kasi kubwa, huku yakihatarisha maisha ya watu duniani kote. Ndio maana unaona tunapambana kuwalinda watumishi wa sekta ya afya," alisema.

Katibu wa hospital hiyo, Rose Shawa, alisema wanatarajia kutoa vipimo kwa watumishi 300, ambao tayari wameanza kufanya vipimo.

"Lengo ni kuhakikisha usalama wa watumishi wetu katika maeneo ya kazi. Mpango huu wa upimaji ni wa lazima ili kujua afya zao na kujikinga, kwa sababu watumishi wanafanya kazi katika mazingira ambayo sio salama kwao.

"Serikali imeliona hilo la kuwalinda watumishi hawa, ikasema ni lazima wapimwe na kupewa chanjo. Ili wakati wa kumuhudumia mgonjwa asipate maambukizi, tumeona maeneo mengine watumishi hao wamehudumia wagonjwa na wakapata maambukizi na kufariki. Hatutaki tufike huko, lazima tuwalinde serikali imekubali kuingia gharama," alisema Shawa.

Mratibu wa Huduma za Afya ya Jamii wa Hospitali hiyo, Dk. Alexndra William, alisema kwa kuwa serikali imegharamia malipo yote ya vipimo na chanjo kwa watumishi wa hospitali hiyo, hakuna mtumishi wala mtaalamu atakayekwepa mpango huo.



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji Mkoa wa Tanga wakizima moto kwenye ghala ya kuhifadhi bidhaa katika Bandari ya Tanga jana, ambalo lilikuwa na bidhaa za magendo zilizokamatwa hivi karibuni. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

## Halmashauri Arusha yavuka lengo ukusanyaji wa mapato

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha imevuka lengo la ukusanyaji mapato ya robo ya kwanza ya mwaka kwa kukusanya Sh.bilioni 7.598 ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita, ambao walikusanya Sh. bilioni 6.129. Kwa mujibu wa Meya wa Jiji hilo, Maxmillian Iraghe, sehemu ya fedha hizo zitatumika katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Wilaya.

"Halmashauri ya Jiji la Arusha tumevuka lengo baada ya kuwapo ongezeko la Sh. bilioni 1.3, ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita katika robo ya kwanza na mafanikio yote haya yanatokana na sisi kufanya kazi kama timu moja," alisema.

Aidha, alisema Sh. bilioni nne zimeshaanza kutumika, kwamba Sh. bilioni 1.2 zimeelekezwa kwenye jengo la wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Wilaya ya Arusha, jengo hilo litakuwa la kuhudumia watalii.

"Katika fedha hizo tumeshapeleka kiasi cha Sh. milioni 500 kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), ili barabara zipitike muda wote, ujenzi wa vyumba vya madarasa ya Shule ya Msasani pamoja na kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu,"alisema.

Alisema pia wamejipanga kuongeza vyanzo vya mapato ili kupaisha mapato ya halmashauri hiyo kwa kujenga soko la kitalii eneo la kwa Mrombo.

"Soko hili litakuwa ni mahali ambako watalii watapata huduma na tutalijenga kwa ustadi wa hali ya juu, watalii watakwenda soko hilo kununua bidhaa mbalimbali lakini kula nyama choma pamoja na vyakula vya asili na sisi tutapata mapato mazuri kutoka kwenye soko hilo," alisema.

Kadhalika aliwaonya baadhi ya watu wanaotumia mitandao ya kijamii kuchafua taswira ya Jiji la Arusha juu ya ukusanyaji wa mapato kwa kutoa taarifa za uongo na kwamba wakiendelea watawachukulia hatua kali za kisheria.

"Natumia fursa hii kuwaonya baadhi ya watu wanaochafua taswira ya Jiji la Arusha kwa kuweka taarifa za uongo kwenye mitandao ya kijamii kuhusu ukusanyaji wetu wa mapato ya Jiji kwa maslahi yao binafsi.

"Watu hawa wanachokifanya siyo sahihi. Watambue kuwa Jiji ni taasisi inayotambulika kisheria na hakuna mtu mwenye mamlaka ya kuzungumzia taarifa za ukusanyaji wa mapato zaidi ya waliopewa dhamana ya kuzungumzia masuala yanayohusu Jiji hilo," alisema.

NIPASHE JUMATATU OKTOBA 24, 2022

Nipashe

# Spotika



SABABU LIVERPOOL KUANZA VIBAYA EPL MSIMU HUU EPL UK.16



## ISIKUPITE

MOHAMED Salah alihitaji dakika sita na sekunde 12 tu kufunga bao la kwanza hadi la tatu (hat-trick) wakati wakishinda 7-1 dhidi ya Rangers wiki iliyopita, hivyo kuweka rekodi ya kufunga hat-trick ya mapema zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuipiku ile ya nyota wa zamani wa Bayern Munich, Robert Lewandowski, ambaye alitumia dakika 11 na sekunde saba Novemba 2019 dhidi ya Red Star Belgrade.

## 'GUU IKULU!!!'...

Kiungo wa Liverpool, Thiago Alcantara, akimchezea rafu mbaya eneo nyeti 'Ikulu', mshambuliaji wa Manchester City, Erling Braut Haaland, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Oktoba 16, mwaka huu katika Uwanja wa Anfield na wenyeji kushinda 1-0. **PICHA: MTANDAO**




# NYOTA WA5 WANAOWEZA KUKOSA KOMBE LA DUNIA

**DOHA,** Qatar

KOMBE la Dunia ndio mashindano makubwa zaidi ya soka. Kila baada ya miaka minne, mataifa yote ulimwenguni hushindana kuwania taji kubwa na linalotamaniwa zaidi katika soka la kimataifa.

**Kwa sababu hii, ndoto ya kila mchezaji wa soka ni kuvaa jezi za taifa lake na kuwakilisha kwenye mashindano hayo.**

Kombe la Dunia la mwaka huu litaanza Novemba 20 nchini Qatar. Wachezaji ambao nchi zao zimefuzu kwa michuano hiyo wote macho yao yapo kwenye kuunda vikosi vya taifa lao.

Hata hivyo, baadhi ya wachezaji wamekuwa na bahati mbaya kwa kushindwa kuzichezea nchi zao. Makala haya inawaangalia wachezaji nyota watano ambao wanaweza kukosa Kombe la Dunia kutokana na majeraha, wafahamu hapa...

**#5. PAULO DYBALA**

Paulo Dybala ni mmoja wa wachezaji nyota wakubwa ambao huenda wasionekane kwenye Kombe la Dunia. Nyota huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 28, alipata jeraha ambalo limemfanya kuwa nje kwa kipindi cha wiki nne hadi sita.

Alipata pigo dakika chache tu baada ya kuifungia Roma bao la pili katika ushindi wao wa 2-1 dhidi ya Leece mnamo Oktoba 9, mwaka.

Dybala amekuwa katika kiwango kizuri tangu ajiunge na Klabu ya Roma kutoka Juventus kwa uhamisho wa bure. Amefunga mabao saba na asisti mbili katika mechi 11 katika mashindano yote kwa kikosi cha Jose Mourinho msimu huu.

Kukosekana kwake kutakuwa pigo kubwa kwa Timu ya Taifa ya Argentina kule Qatar.

**#4. REECE JAMES**

Beki wa Chelsea na England, Reece James ni mmoja wa mabeki wa kushoto wenye viwango vya juu zaidi duniani kwa sasa. Tangu aanze kujulikana na klabu hiyo ya London mwaka 2019, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amejidhihirisha kuwa mmoja wa wachezaji bora katika nafasi yake.

James amekuwa katika kiwango kizuri msimu huu, akifunga mabao mawili na kutengeneza pasi mbili za mabao katika mechi 11 alizoichezea Chelsea. Hata hivyo, nafasi yake ya kucheza Kombe la Dunia inaweza isiwapo.

Jeraha la goti la James ni baya zaidi kuliko ilivyotarajiwa na anaweza kukosa Kombe la Dunia. Nyota huyo alipata jeraha la goti wakati Chelsea ilipomenyana na AC Milan Oktoba 11 katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#3. PAUL POGBA**

Paul Pogba amekuwa nje ya uwanja tangu majira ya joto. Julai, wiki chache baada ya kukamilisha uhamisho wa bure wa kurejea Juventus, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa aliumia goti lake la kulia na tangu wakati huo amekuwa nje ya uwanja.

Alikuwa mchezaji muhimu kwa Ufaransa wakati ikitwaa taji la dunia kule Urusi miaka minne iliyopita. Kwa bahati mbaya, nafasi ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, anaweza asiichezea timu hiyo.

Hata kama atarejea kabla ya michuano hiyo kuanza, Pogba atakuwa anahitaji muda wa kuwa fiti.

**#2. N'GOLO KANTE**

Kiungo nyota wa Chelsea N'Golo Kante ni mchezaji mwingine bora ambaye pengine hatutamwona akiwa kazini kwenye Kombe la Dunia. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa kwa sasa anauguza jeraha la msuli wa paja.

Kante alipata pigo hilo wakati Chelsea ilipocheza na Tottenham Hotspur kwenye Ligi Kuu England Agosti 14, mwaka huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, hajaichezea Chelsea tangu wakati huo, na anatarajiwa kukaa nje kwa miezi michache zaidi.

Alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wakati wa ushindi wa timu yake nchini Urusi mnamo 2018, akisajili jumla ya dakika 595 katika michezo saba ya Ufaransa ikitawazwa mabingwa.

**#1. MARCO REUS**

Maisha ya soka ya Marco Reus yamekumbwa na majeraha mara kwa mara. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani hajatimiza uwezo wake kamili kutokana na jeraha moja au jingine katika miaka michache iliyopita.

Alikosa ushindi wa Kombe la Dunia la Ujerumani mnamo 2014 kutokana na jeraha la kifundo cha mguu na anaweza kukosa kucheza Qatar 2022 kwa sababu hiyo hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, alipata jeraha baya la kifundo cha mguu Septemba 17, mwaka huu dhidi ya Schalke 04. Reus alitolewa nje ya uwanja na hajaicheza Borussia Dortmund tangu wakati huo.

Ingawa uchunguzi ulibaini kuwa jeraha hilo halikuwa kubwa kama inavyodhaniwa, inabaki kuonekana kama Reus anaweza kupona kwa wakati na kurejesha kiwango chake katika timu hiyo ya Hansi Flick kwenye Kombe la Dunia.

## MICHEZO

FATUMA ISSA 'FETTY DENSA'



# NA CHANZO CHA HIJAB UWANJANI

• Aanika pia soka lilivyomtoa kimaisha

**Na Hadija Mngwai**

WACHEZAJI wa soka wengi hupenda kuwa na alama zao zinazowatambulisha kirahisi ama kuwatofautisha kimwonekano na wenzao, kama kunyoa mtindo fulani wa nywele, kuchora tatoo na hata namna ya uvaaji wa jezi uwanjani, hivyo ndivyo ilivyo pia kwa mshambuliaji wa Simba Queens na Timu ya Taifa ya Tanzania ya Wanawake (Twiga Stars), Fatuma Issa 'Fetty Densa'.

**Fetyy Densa, ambaye huwezi kuacha kutaja jina lake pindi unapozungumzia soka la wanawake nchini, yeye amejizolea umaarufu mkubwa si tu uwanjani, bali pia kutokana na uvaaji wake wa hijab akiwa anatandaza soka dimbani.**

Fetty Densa ambaye ni nahodha wa Simba Queens iliyopo mkoani Iringa ikijiandaa na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, anasema awali alikuwa hacheze na hijab na kwa kwamba mara ya kwanza alipoamua kuanza kuvaa ilikuwa shida, lakini kwa sasa haoni tatizo lolote.

"Kwangu haina shida yoyote kucheza nikiwa nimevaa ushungi ni kawaida na ninaamini kupitia mimi kuna watu wengine watajifunza kupitia hichi ninachokifanya kwa kuona ni kitu kizuri."

**LIGI YA MABINGWA**

Fetty Densa ambaye alikiongoza kikosi hicho kutwaa ubingwa wa Cecafa mapema mwezi wa nane kwa kuifunga She Corporate FC ya Uganda kwenye mechi ya fainali na Simba Queens kuweka rekodi ya kushiriki michuano ya Ligi Mabingwa Afrika ikiwa timu ya kwanza ya wanawake kutoka Tanzania kufanya hivyo, anasema wamejipanga vema kufanya makubwa katika michuano hiyo.

Katika michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Oktoba 30 hadi Novemba 13, mwaka huu, Simba Queens imepangwa Kundi A na Green Buffaloes ya Zambia, Determines ya Liberia pamoja na wenyeji, ASFAR ya Morocco.

**ALIPOANZIA SOKA**

Fetty Densa ambaye ni mzaliwa wa Morogoro, anasema alianza kucheza soka tangu akiwa mdogo wakati huo akisoma shule ya msingi na kisha kucheza mitaani kabla ya kuanza kucheza soka la kulipwa baada ya kuja Dar es Salaam.

"Nilikuja Dar es Salaam mwaka 2010, kisha nikajiunga na timu ya Eva Green ya Temeke ambayo niliichezea kwa kipindi cha miaka tisa kabla ya kujiunga na Simba mwaka 2019," anasema.

**SAPOTI KWA WAZAZI**

"Kwa upande wa wazazi wangu walinisapoti kwa kiasi kikubwa hadi kufikia hapa nilipo, ila kipindi cha nyuma bibi yangu alikuwa na mashaka kuona mimi nacheza soka.

"Ilikuwa tabu sana kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa akinilea, siunajua tena malezi ya bibi? Lakini baadaye alikuja kunielewa baada ya kuona kuna kitu nakitafuta na kukihitaji, hivyo akaona si mbaya kuniachia kupambana katika soka la wanawake.

"Kwa hiyo nimeendelea kupambana hadi leo na ndio maana wazazi wangu wameona kuna matunda yanaonekana na kuendelea kunitia moyo jambo ambalo linanifanya daima nipambane zaidi kwa sababu wao ndio wanaonipa nguvu sana."

**CHANGAMOTO NDANI YA SIMBA**

"Nimekutana na changamoto nyingi baada ya kutua Simba kwa kuwa hii ni timu kubwa kila mmoja anataka kupambana ili kuweze kupata namba.

"Ninaamini kila mmoja anacheza kwa kujituma ili apate namba na kufikia malengo yake na ya timu kwa jumla, changamoto ni za kawaida ambazo kila mmoja anazipitia ila naamini kila mmoja anapambana ili kuipeleka mbali timu yetu."

**CHANGAMOTO KATIKA SOKA**

"Changamoto zipo nyingi, wengi wanaamini mpira huu wa miguu ni kwa wanaume tu na si kwa watoto wa kike, lakini nakabiliana nazo hivyo hivyo kwa sababu ndio kipaji changu na mpira ndio kazi yangu ninayoipenda.

"Nafanya hivyo kwa kuwa nina malengo ya kufika mbali, hivyo naendelea kupambana ili nitimize ndoto yangu licha ya baadhi kuuona mpira wa miguu kwa wanawake ni kama ni uhuni."

**MAFANIKIO KATIKA SOKA**

"Mafanikio niliyoyapata hadi sasa kwanza ni kujuana na watu mbalimbali, pili makombe niliyofanikiwa kuyapata nikiwa katika timu ya Taifa, Twiga Stars na Simba Queens.

"Pia napata pesa kupitia kipaji changu cha mpira vilevile nasaidia familia yangu kupitia kazi hii, kuna mafanikio yangu binafsi niliyoyapata ambayo sipendi kuyaweka hadharani, ni kitu kikubwa sana kwangu ambacho kila mtu anatamani kukipata katika maisha yake.

**USHINDANI LIGI YA WANAWAKE**

Anasema kwa sasa umekuwa mkubwa na ligi hiyo imekuwa na mvuto tofauti na huko nyuma.

**AHADI KWA WANASIMBA**

Fetty Densa anasema kufanya vizuri katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ndicho kitu anachowaahidi.

**USHAURI KWA WAZAZI**

"Naomba wazazi na walezi kuwaruhusu watoto wao kwani mpira ni ajira pale wanapoona wanavipaji na si kuwafungia ndani.

"Mpira wa miguu ni mchezo kama michezo mingine, wasiwabeze watoto wao naupenda kwa kuona uhuni, waendelee kuwaunga mkono ili tuweze kulifikisha soka la wanawake mbali zaidi."

**NJE YA UWANJA**

Mshambuliaji wa zamani wa Brazil, Ronaldo Nazario: "Je, Messi anastahili (kushinda Kombe la Dunia? Bila shaka, anastahili – lakini mimi simsapoti, labda kama uraia wake ungekuwa ni Muhispania. Brazil na Argentina ni mahasimu wa jadi, ninampenda na ataelewa na ninauhakika atajisikia hivyo hivyo".






# SABABU LIVERPOOL KUANZA VIBAYA EPL MSIMU HUU

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL wamepata mwanzo mbaya zaidi katika Ligi Kuu England msimu huu. Kocha Jurgen Klopp amefanikiwa kuwafanya 'Wekundu' hao kufanya vizuri kwa misimu kadhaa, lakini haijawa hivyo hadi sasa msimu huu.

**Liverpool walipewa nafasi kubwa ya kuwania taji la Ligi Kuu baada ya kumaliza pointi moja nyuma ya mabingwa, Manchester City msimu uliopita.**

Makala haya yanaangalia mambo matano yaliyoifanya Liverpool kutokuwa na kiwango kizuri msimu huu, twende sasa...

#5. Kutobadilika kwa Jurgen Klopp

Tangu awasili Anfield Oktoba 2015, Jurgen Klopp ameigeuza Liverpool kuwa timu ambayo inaweza kugombea kila taji katika soka la nyumbani. Kwa kweli, pia ameshinda kila taji, ukiondoa Ligi ya Europa ambayo Liverpool haijashiriki tangu kupoteza katika fainali ya mwaka 2016 na Sevilla.

Klopp ametumia mbinu fulani ambazo zimefanya kazi vizuri kwake na kwa wachezaji wake. Mchanganyiko wa nguvu ya juu katika maeneo muhimu imekuwa siri ya mafanikio yao. Hata hivyo, kuna wakati wa kushikamana na itikadi za mtu na wakati wa kukabiliana na hali iliyopo.

Tangu aanze kuinoa klabu hiyo, Klopp amechagua mabeki wanne na hajawahi kufanya majaribio zaidi ya hapo.

Zaidi ya hayo, kudumisha kiwango cha juu cha nguvu haiwezekani kila wakati, lakini kocha huyo wa Ujerumani hajajitolea kwa msimamo huo. Matatizo yao ya safu ya ulinzi yameifanya Liverpool kufungwa mabao 12 kwenye ligi katika mechi nane.

Klopp hajajaribu kuzoea na kubadilisha mbinu zake kuja kwenye timu zilizo na mpango tofauti wa mchezo. Hii imeruhusu kila timu barani Ulaya, pamoja na Ligi Kuu kupunguza vitisho vyao, kwa sababu tu hakuna mpango B kwa Liverpool.

Ni wakati tu ndio utakaoamua kama kocha huyo mwenye umri wa miaka 55, anaweza kuzoea kabla ya timu yake kupata misukosuko zaidi katika wiki zijazo.

### #4. UMRI WA WACHEZAJI

Klopp amekuwa na msingi thabiti wa wachezaji kwenye kikosi ambao ameweza kuwategemea pindi hali inapokuwa ngumu.

Lakini kundi hili kuu, ambalo linajumuisha wachezaji kama James Milner, Jordan Henderson, Virgil Van Dijk, Roberto Firmino na Mohamed Salah, umri umeanza kuwatupa mkono.

Ingawa watatu wa mwisho wako katika miaka yao ya mapema ya 30, kiwango chao kimeshuka msimu huu.

Liverpool, chini ya Klopp, wanasifika kwa kucheza soka la kuvutia, lakini hilo linahitaji nguvu nyingi na damu changa.

Wakati Darwin Nunez, Diogo Jota, Harvey Elliot, Trent Alexander-Arnold ni vijana, lakini bado hawakofiti. Zaidi ya hayo, Thiago Alcantara, ambaye anategemewa, ana majeruhi na pia yupo kwenye umri wa miaka 30.

Kwa hiyo, timu ambayo haikuwa na wachezaji waliokuwa na umri wa miaka 30, miaka mitano iliyopita sasa ina wachezaji wengi.

Klabu ina wachezaji wapatao sita hadi saba pekee wenye umri wa miaka 24 hadi 28. Jambo la kusikitisha kwa Liverpool ni kwamba rundo la wachezaji wake kwa sasa ni majeruhi.

### #3. MABADILIKO YA JUKUMU LA SALAH

Mohamed Salah amekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio ya Liverpool tangu ajiunge na klabu hiyo akitokea AS Roma mwaka 2017.

Nyota huyo wa Misri ameshinda Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England mara tatu kati ya misimu mitano iliyopita huku pia akifunga mabao muhimu katika mashindano ya Ulaya. Amefunga mabao 164 na asisti 67 katika mechi 267 za Wekundu hao.

Lakini msimu huu ameanza taratibu na mchezo pekee aliopata uhai ulikuwa ushindi wa 7-1 dhidi ya Rangers katika Ligi ya Mabingwa Ulaya Oktoba 12. Salah alifunga hat-trick ya haraka zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akitokea benchi.

Mambo yamebadilika msimu huu, kwa sababu tu jukumu la Salah limebadilika pia.

Hii imesababisha nafasi ya kuanzia ya Salah kuwa mbali zaidi na goli huku pia akilazimika kuunda mfumo mpya na Luis Diaz na Darwin Nunez.

Ingawa wawili hao ni wazuri sana kwenda mbele na kimbinu wako tofauti na Sadio Mane na Roberto Firmino. Kwa hiyo, haishangazi kwamba Mmisri huyo anapata tabu kufika katika nafasi za kupachika mabao, lakini badala yake anafanya vema katika kutengeneza nafasi.

### #2. UKOSEFU WA VIUNGO

Liverpool imekuwa na sera nzuri ya uhamisho katika kipindi cha muongo mmoja hivi uliopita. Isitoshe, mapungufu yoyote yamefunikwa na mbinu za Klopp.

Aurelien Tchouameni alikuwa akitajwa kusajiliwa msimu huu wa majira ya joto, lakini Mfaransa huyo badala yake akachagua kusaini Real Madrid.

Jude Bellingham pia anaripotiwa kuwa mlengwa wa muda mrefu. Hata hivyo, hakuna uhakika wa kumsajili msimu ujao wa majira ya joto.

Arthur Melo alimaliza kujiunga kwa mkataba wa mkopo kutoka Juventus siku ya mwisho. Hata hivyo, tayari amepata jeraha ambalo linaweza kumuweka nje kwa miezi mitatu, na kupoteza nafasi yake ya kufanya vizuri katika kipindi kigumu kwa klabu hiyo.

Kwa hiyo, Liverpool sasa wana Henderson, Thiago, Milner, Fabinho, Jones, Keita, Carvalho na Elliott kama chaguo lao la kiungo.

Carvalho, Jones na Elliot bado wanajifunza, huku Keita akiripotiwa kutofurahishwa na Klopp. Kombinesheni yoyote ya Fabinho, Milner, Henderson na Thiago haitoi nguvu ya kutosha kucheza soka la hali ya juu ambalo Liverpool wanahitaji ili kuwashinda wapinzani wao.

### #1. TRENT ALEXANDER-ARNOLD

Trent Alexander-Arnold bila shaka ni kipaji cha kizazi hiki na namba zake za miaka mitano iliyopita zinajieleza zenyewe.

Ingawa ustadi wake wa kushambulia umezidi mapungufu yake kwenye safu ya ulinzi katika kipindi cha nusu muongo uliopita, hiyo haiwezi kusemwa kuhusu kampeni ya sasa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ana majukumu madogo ya ulinzi kuliko wachezaji wengine wa nyuma.

Ingawa hawezi kulaumiwa, Alexander-Arnold amekuwa na wakati ambao ameonekana akirudi nyuma kwa uvivu.

Ikizingatiwa kwamba amekuwa hayuko karibu na ubora wake wa kusonga mbele, Alexander-Arnold anahitaji kupata kiwango kizuri hivi karibuni.

Hata hivyo, baada ya kupata jeraha dogo hivi majuzi, huenda ikamchukua muda hadi baada ya Kombe la Dunia lijalo la FIFA kuimarisha kila awamu ya mchezo wake.

## Nukuu

"Usipoifunga Inter nyumbani [kwako] hustahili kuendelea. Sasa haitegemei tena upande wetu, hatustahili kuendelea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ni pigo gumu, gumu sana. Neno hili linaweza kuwa la kikatili," **Kocha Mkuu wa Barcelona, Xavi baada ya timu yake kulazimishwa sare ya mabao 3-3 nyumbani dhidi ya Inter wiki iliyopita.**



"Kama ningekuwa mkurugenzi wa michezo, ningemsajili Messi [Lionel] Barcelona. "Tumekuwa tukifanya naye kazi kwa muda. Hapo mwanzo ilikuwa ngumu kidogo, kwa sababu anakuja na mawazo mapya, na mambo ambayo yalikuwa hayafanyiki miaka ya karibuni hapa," **Beki wa Barcelona, Ronald Araujo akitamani kuungana na nyota wa Paris Saint-Germain, Lionel Messi.**



"Timu nzuri; wanacheza soka la kisasa, wanashambulia wakiwa 11 na kulinda wakiwa 11. Wakati mwingine, inaonekana kama wanaweza kuwa uwanjani wakiwa wamefumba macho. Wanakuja pamoja kwa urahisi wa ajabu na haya ni matokeo ya ukarimu, ushirikiano uliopo kikosini. Bravo kwa Spalletti, kwa sababu hapa unaweza kuona, na mengi, mkono wa kocha. Nadhani wanaweza kufika mbali [kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya]. Nani ajuaye, labda hata nusu fainali ikiwa droo haitakuwa mbaya sana. Kwa vyovyote vile, hadi sasa kazi ya vijana wa Spalletti ni 10 kati ya 10," **Kocha wa zamani wa Milan na Italia, Arrigo Sacchi akiimwagia sifa Napoli.**





# HAWA NDIO CLUB AFRICAIN WAPINZANI WA YANGA SC CAF

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga watakwenda kucheza mechi ya mtoano ya Kombe la Shirikisho Afrika kabla ya kutinga hatua ya makundi dhidi ya Club Africain ya Tunisia.

**Kwa mujibu wa droo iliyopangwa wiki iliyopita jijini Cairo, Misri yalipo Makao Makuu ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), Yanga itaanzia nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Novemba 2, kabla ya kwenda Tunisia kumalizia mechi ya mkondo wa pili itakayopigwa Novemba 9, mwaka huu.**

Yanga itacheza na timu hiyo, baada ya kusukumizwa nje ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan kwa jumla ya mabao 2-1, ikitoka sare nchini kwenye mechi ya kwanza na kufungwa bao 1-0 mchezo wa marudiano.

Club Africain inakumbukwa vema msimu huu kwa kuiondosha timu ya Tanzania, Kipanga ya Zanzibar kwa mabao 7-0 kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Hii ni timu kongwe ambayo mashabiki wengi wa kizazi cha sasa hawaijui vizuri, lakini kwenye miaka ya 1980 hadi 1990 ilikuwa moja kati ya timu tishio nchini Tunisia na barani Afrika, hapa tunaimulika kwa undani zaidi...

## TIMU YA TATU KWA UBORA TUNISIA

Kwa sasa inatajwa kama ni timu ya tatu kwa ubora nchini humo baada ya Esperance na Etoile du Sahel ambazo ndizo zinazotamba nchini Tunisia kwa sasa na kupata nafasi za kuiwakilisha nchi hiyo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Club Africain na CS Sfaxien zikipaswa kukita kambi kwenye Kombe la Shirikisho.

## BINGWA WA AFRIKA MWAKA 1991

Ilitwaa ubingwa wa Afrika mara moja, ambapo mwaka 1991 ikiuchukulia kwenye Uwanja wa Nakivubo, Kampala nchini Uganda.

Ilifanikiwa kuingia fainali na kucheza dhidi ya SC Villa, ambapo kwenye mechi ya kwanza nchini Tunisia, Uwanja wa El Menzah ilitoa kipigo cha mabao 6-2 Novemba 23, na kwenye mechi ya marudiano timu hizo zikatoka sare ya bao 1-1 nchini Uganda, Desemba 14, 1991, Club Africain ikakabidhiwa kombe lake nchini humo kwa ushindi wa jumla ya mabao 7-3.

## FAINALI SHIRIKISHO 2011

Mafanikio mengine makubwa ya timu hiyo ni kucheza fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika 2011 dhidi ya Maghreb de Fes ya Morocco na kupoteza kwa mikwaju ya penalti 6-5.

Ikiwa nyumbani Novemba 19, mwaka huu, ilishinda bao 1-0, lakini ikaenda kupoteza kwa idadi kama hiyo nchini Morocco, Desemba 4, hivyo timu hizo zikalazimika kuingia kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti na ndipo ilipolikosa kombe hilo.

## MAKUNDI LIGI YA MABINGWA MARA MOJA

Club Africain imefanikiwa kuingia hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika mara moja tu. Nayo ilikuwa ni msimu wa 2018/19 na haikufanikiwa kabisa kutinga hatua ya robo fainali, yaani kushika nafasi mbili za juu.

Ikiwa kwenye Kundi C, timu hiyo ilishika nafasi ya tatu ikimaliza na pointi 10 sawa na CS Costantine ya Algeria, lakini ikizidiwa mabao ya kufunga, hivyo wenzao wakashika nafasi ya pili na kwenda robo fainali, TP Mazembe akiliongoza kundi kwa pointi 11, Ismailia ya Misri ikishika mkia kwa pointi mbili.

## MAKUNDI MARA TATU KOMBE LA SHIRIKISHO

Timu hiyo inawania kuingia kwenye hatua ya makundi Kombe la Shirikisho Afrika kwa mara ya nne. Imeshafanya hivyo mara tatu, kuanzia 2008, 2011 ilivyokwenda mpaka hatua ya fainali na 2017 ilipoingia na kuishia hatua ya nusu fainali ilipochapwa jumla ya mabao 4-1 dhidi ya Super Sport United ya Afrika Kusini, baada ya kutoka sare nyumbani bao 1-1, kabla ya kwenda kufa nchini Afrika Kusini kwa mabao 3-1.

## KIKOSI CHA BILIONI 21 ZA KIBONGO

Club Africain imepitia kipindi kigumu kwa siku za karibuni kutokana na kuyumba kiuchumi, na kama haitoshi kuwa adhabu ya kutoruhusiwa kusajili wachezaji katika madirisha matatu.

Hii ilitokana na kushindwa kumlipa Mchezaji Mghana Nicholas Opoku baada ya kuvunja naye mkataba. Hali hiyo ya ukata ilisababisha kuondokewa na nyota wao kadhaa akiwamo kinara wa mabao msimu uliopita, Yassine Chamack aliyejiunga Al Ahly Tripoli ya Libya.

Hata hivyo, kwa sasa wanaonekana kujipanga kwani ina kikosi chenye thamani ya Dola za Marekani milioni 9.29 zaidi ya Sh. bilioni 21 za Tanzania.

**NDANI YA 18**



Mshambuliaji wa Barcelona, Robert Lewandowski, ana bao moja kutoka katika kila mashuti mawili aliyopiga yakalenga goli msimu huu. Mashuti 18 mabao tisa.

# SOKA




## MKALI WA WIKI

**JINA KAMILI:** Kylian Mbappe Lottin
**KUZALIWA:** Desemba 20, 1998 (miaka 23)
**ALIPOZALIWA:** Paris, Ufaransa
**KIMO:** 1.78 m (5 ft 10 in)
**NAFASI:** Mshambuliaji
**KLABU:** Paris Saint-Germain
**JEZI NAMBA:** 7
**MABAO:** 10 (Kinara Ligue 1)

LIVERPOOL wamepata mwanzo mbaya zaidi katika Ligi Kuu England msimu huu. Kocha Jurgen Klopp amefanikiwa kuwafanya 'Wekundu' hao kufanya vizuri kwa misimu kadhaa, lakini haijawa hivyo hadi sasa msimu huu.

Uk. 16-17



AARON RAMSDALE

# MAGOLIKIPA WA5 BORA ZAIDI KWA SASA EPL

**LONDON, England**

MSIMU wa Ligi Kuu England (EPL), unazidi kushika kasi na timu kadhaa zinafanya vema hadi sasa. Arsenal ndio vinara wa ligi wakiwa na pointi 27 baada ya kucheza michezo 10 kabla mechi yao ya jana, huku Nottingham Forest wakiwa mkiani mwa msimamo wa ligi wakiwa na pointi tano katika mechi 10 za mwanzo.

**Hadi sasa, kumekuwa na makipa kadhaa kwenye ligi ambao wamefanya vizuri. Makala haya yanaangalia magolikipa watano waliofanya vizuri kwenye Ligi Kuu hadi sasa msimu huu, hawa hapa...**

**#5. JOSE SA (WOLVERHAMPTON WANDERERS)**

Licha ya mwenendo mbaya wa timu yake kwenye ligi, mchezaji huyo wa Ureno amekuwa na wakati mzuri kwenye lango la Wolverhampton Wanderers.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, amecheza mechi nne bila kuruhusu bao kati ya 10 kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Sa anabaki kuwa mchezaji muhimu kwa Wolverhampton Wanderers katika msimu wa 2022-23 na uthabiti wake katika goli bado ni muhimu kwa timu.

**#4. ALISSON BECKER (LIVERPOOL)**

Licha ya Liverpool kuanza vibaya msimu huu, utendaji wa Alission langoni umekuwa mzuri. Mbrazil huyo amesajili pasi moja ya goli na amecheza mechi tatu kati ya tisa bila kuruhusu bao msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ndiye mlinda mlango aliyehusika kwenye idadi kubwa ya mabao katika historia ya Ligi Kuu.

Alisson anabakia kuwa mchezaji muhimu kwa 'Wekundu' hao na uwapo wake langoni umekuwa muhimu kwa kocha Jurgen Klopp msimu huu.

**#3. NICK POPE (NEWCASTLE UNITED)**

Nyota huyo wa England alijiunga na Newcastle United kutoka Burnley kwa pauni milioni 10 na uwapo wake langoni umeboresha kiwango cha timu hiyo msimu huu. Pope amecheza mechi nne kati ya 10 bila kuruhusu bao msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, katika suluhu ya Manchester United Oktoba 16 ilikuwa ni mechi yake ya 50 bila kufungwa bao kwenye Ligi Kuu.

Zaidi ya hayo, ni makipa wanne pekee ambao wametoa pasi za mabao kuliko Pope tangu alipoanza mechi yake ya kwanza ya ligi mnamo Septemba 2017.

Pope amekuwa mmoja wa wachezaji bora wa Newcastle United msimu huu na uwapo wake langoni ni muhimu kwa kocha, Eddie Howe.

**#2. AARON RAMSDALE (ARSENAL)**

Nyota huyo wa England ni mmoja wa wachezaji bora wa 'Washikabunduki' kwenye ligi na uwapo wake umekuwa muhimu kwa kikosi hicho.

Ramsdale amecheza mechi nne bila kuruhusu bao katika mechi 10 za ligi msimu huu.

Ramsdale mwenye umri wa miaka 24, anabakia kuwa mchezaji muhimu kwa Arsenal na uthabiti wake unahitajika ili timu hiyo iweze kuibuka washindi wa taji la ligi.

**#1. EDERSON (MANCHESTER CITY)**

Mlinda mlango wa Manchester City bila shaka ni mmoja wa makipa bora kwenye ligi. Ederson amecheza mechi tano kati ya 10 za Ligi Kuu bila kuruhusu bao na hii ndiyo idadi kubwa zaidi kwa golikipa kwenye ligi msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, anabakia kuwa mchezaji muhimu kwa kocha Pep Guardiola na itafurahisha kuona kama anaweza kuibuka mshindi wa golikipa bora wa msimu.

**JE, WAJUA?**




Kiungo wa Manchester United, Antony ni mchezaji wa kwanza katika klabu hiyo kuweza kufunga mabao mfululizo katika mechi zake tatu za mwanzo wa msimu wa Ligi Kuu England. Mabao matatu katika mechi tatu za mwanzo.



# Aahidi tofali 15,000 ujenzi maabara 3 Sekondari Mbalizi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MDAU wa maendeleo mkoani Mbeya, Ndele Mwaselela, ameahidi kutoa matofali 15,000 kwa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya ujenzi wa maabara tatu za Shule ya Sekondari Mbalizi.

Pia ameahidi kuchimba kisima cha maji ili kuwasaidia wanafunzi wa shule hiyo kuondokana na tatizo la ukosefu wa huduma hiyo na kuepuka kukumbwa na magonjwa ya mlipuko.

Alitoa ahadi hiyo juzi kwenye mahafali ya kidato cha nne katika shule hiyo.

Alisema ameamua kutoa msaada huo kama sehemu ya shukrani kwa jumuiya hiyo kwa maelezo kuwa ndiyo iliyomsomesha baada ya familia yake kukosa fedha za kumlipia ada.

Alisema ili kuhakikisha ujenzi wa miundombinu hiyo inaanza ni lazima uongozi wa shule hiyo kwa kushirikiana na bodi ya shule kutafuta vifaa vingine vya ujenzi ikiwamo saruji, mawe na mchanga.

Alisema atakaa kikao maalumu na viongozi wa shule hiyo pamoja na wadau wengine wa elimu mkoani humo ili kuangalia namna bora ya kutekeleza mradi huo na kwamba ujenzi huo utaanza Juni mwakani.

"Mimi nimesomeshwa na Jumuiya ya Wazazi ya CCM kwa hiyo ninatoa vitu hivi kama shukurani zangu, wazazi wangu walikosa ada ya kunilipia kwenye shule niliyokuwa nimepangiwa lakini jumuiya hii ilinichukua na kunisomesha kwenye shule zake," alisema Mwaselela.

Mwaselela alisema shule hiyo ni miongoni mwa shule chache za jumuiya hiyo ambazo zinafanya vizuri kitaaluma kwa maelezo kuwa imekuwa ikiongoza katika Mkoa wa Mbeya kwa miaka ya karibuni.

Mkuu wa Shule hiyo, Marco Shija alisema shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa maabara kutokana na vyumba vilivyoko kuwa vidogo, havikidhi mahitaji ya wingi wa wanafunzi waliopo kwa sasa.

Alisema kwa sasa shule hiyo ina zaidi ya wanafunzi 600 wa kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha sita na kwamba kuna uwezekano wakaongezeka zaidi mwakani baada ya kuwapokea wa kidato cha kwanza ambao wanaendelea kufanyiwa usahili.

Alisema wamekuwa wakishindwa kukarabati miundombinu hiyo pamoja na kujenga mipya kutokana na baadhi ya wazazi kutowalipia watoto wao ada kwa wakati.

# Serikali, wananchi wamaliza mgogoro uliodumu miaka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO uliodumu kwa miaka mingi kati ya wananchi wa Kijiji cha Kikondo kilichoko Kata ya Ilungu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na serikali umemalizika na wananchi hao kuruhusiwa kuendelea kuishi katika eneo hilo.

Wananchi hao wamekuwa na mgogoro na serikali kutokana na eneo wanaloishi kuingiliana na shughuli za Hifadhi ya Taifa ya Kitulo pamoja na vyanzo vya maji vya Mto Ruaha Mkuu na Mto Lufilio, wakitakiwa kuhama.

Mgogoro huo umemalizika baada ya juzi Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka pamoja na wahifadhi wa Hifadhi ya Kitulo walifika katika kijiji hicho kwa ajili ya kuwasikiliza wananchi hao na kutoa maamuzi. Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mtaka alisema kwa muda mrefu wananchi hao wamekuwa wakipata huduma mkoani Mbeya na hakuna sababu ya mikoa hiyo kuendelea kuwagombea kwa sababu eneo walilopo lipo ndani ya Tanzania.

Alisema wananchi hao hawawezi kuondolewa kwenye eneo hilo kwa sababu wanapata huduma zote za kijamii ambazo zimepelekwa na serikali na hivyo wataendelea kuishi hapo na wataendelea kuhudumiwa kama ilivyokuwa awali.

"Sisi viongozi wa Mkoa wa Njombe, tutakuwa wa mwisho kusema tulete tingatinga tuvunje nyumba zenu, mmeishi kwa muda mrefu hapa, serikali imewaletea umeme, imewaletea shule, imewaletea kituo zahanati na huduma zingine kwahiyo hamtaondoka kwa sababu huduma hizi zililetwa kwa ajili yenu," alisema Mtaka.

Hivyo, alimshauri Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera kuwashirikisha wananchi wa kijiji hicho kutunza vyanzo vya maji kwa maelezo kuwa wamekuwa wakihifadhi mazingira kwa muda mrefu.

Homera alikubali wananchi hao waendelee kuhudumiwa na mkoa wake kwa maelezo kuwa tangu awali walikuwa wanahudumiwa na mkoa huo.

Alisema anakusudia kumshauri Rais Samia Suluhu Hassan ili awaruhusu wananchi hao kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kuepuka mwingiliano wa shughuli mbalimbali zikiwamo za uhifadhi pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji.

Hata hivyo alisema pamoja na kwamba wananchi hao wameruhusiwa kuishi katika eneo hilo, bado kuna baadhi ya nyumba zitatakiwa kuondolewa kutokana na kujengwa karibu na vyanzo vya maji ambavyo vinatakiwa kuhifadhiwa.

"Kwa hiyo zile nyumba 19 ambazo zipo karibu na vyanzo vya maji itabidi tuwahamishie kwenye maeneo mengine ambayo tutaona ni sahihi ili kulinda chanzo hicho," alisema Homera.

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Kitulo, Theodora Batiho, alisema uhusiano wa wahifadhi na wananchi wa kijiji hicho umeimarika hivi karibuni baada ya kuzungumza nao kupitia wazee wa mila.

Alisema kwa miaka ya nyuma walikuwa maadui na maofisa wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) walikuwa wanaogopa kupita kwenye kijiji hicho lakini kwa sasa wanashirikiana kwenye shughuli mbalimbali za kijamii.

Baadhi ya wakazi wa kijiji hicho waliishukuru serikali kwa kuwaruhusu waendelee kuishi kwenye eneo hilo kwa maelezo kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wakiishi kwa wasiwasi wakiamini kwamba wangeondolewa.

Mmoja wa wananchi hao, Stella Seme alisema watahakikisha wanashirikiana na maofisa wa serikali kuhakikisha wanaendelea kulinda vyanzo vya maji pamoja na maeneo mengine ambayo yamehifadhiwa.



Wakazi wa Kijiji cha Kikondo, Kata ya Ilungu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wakiwasikiliza wakuu wa mikoa ya Mbeya, Juma Homera na Njombe, Anthony Mtaka waliotembelea kijijini hapo mwishoni mwa wiki kwa ajili ya kutatua mgogoro wa mipaka ulikuwa unasumbua muda mrefu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kampuni 8 zajitosa zabuni barabara Igawa-Tunduma

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMPUNI nane za makandarasi zimejitokeza kuomba zabuni ya utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa barabara ya Igawa-Tunduma yenye urefu wa kilomita 218.

Watendaji wa kampuni hizo kwa kushirikiana na viongozi wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) wa mikoa ya Mbeya na Songwe, waliikagua barabara hiyo mwishoni mwa wiki kuanzia Tunduma mpaka Igawa.

Lengo la ukaguzi wa barabara hiyo ilikuwa ni kuwaonyesha makandarasi hao walioomba zabuni pamoja na kuyapa nafasi kampuni hizo kuangalia sehemu za kupata baadhi ya vifaa vya ujenzi ikiwamo mawe, mchanga na maji ili kupanga gharama za ujenzi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kampuni zilizoomba zipo nane na hakuna kampuni yoyote ya kizawa iliyoomba na kwamba zabuni itafunguliwa rasmi Novemba mwaka huu.

Alisema miongoni mwa kampuni hizo itateuliwa kampuni moja ambayo itaonekana ina vigezo ili kuanza utekelezaji wa mradi huo mapema kwa ajili ya kusaidia kuboresha miundombinu hiyo.

Homera aliwapongeza wananchi wa Jiji la Mbeya kwa kujenga makazi yao na kuacha nafasi ya kutosha kwa ajili ya hifadhi ya barabara hiyo kwa maelezo kuwa katikati ya Jiji hilo barabara itakuwa ya njia nne pamoja na barabara ya mchepuko.

"Anahitajika mkandarasi mmoja kwahiyo maofisa wa TANROADS kutoka makao makuu, watakuja hapa kwa ajili ya kufanya 'evaluation' (upembuzi), kwa hiyo sisi tunaishukuru serikai yetu kwa kuamua kuiboresha barabara hii," alisema Homera.

Alisema barabara hiyo ni muhimu kwa ajili ya kuiunganisha Tanzania na mataifa ya ukanda wa SADC na kwamba ikikamilika itapunguza usumbufu ambao umekuwa ukitokea hasa katikati ya Jiji la Mbeya ambalo linakuwa na msongamano wa magari.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Matali Masige alisema barabara hiyo ilijengwa mwaka 1978 na hivyo imechoka, kwamba inahitajika kujengwa upya ili iendane na mahitaji ya sasa.

Alisema katika barabara hiyo yamekuwa yakitokea matatizo mbalimbali ikiwamo ajali za barabarani kutokana na miundombinu kuharibika na kutoendana na mahitaji ya sasa.

"Hii barabara imekuwa ikipitisha magari yenye mizigo mizito kwa hiyo inahitaji kuimarishwa zaidi, tunaishukuru serikali kwa kuamua sasa tuipanuwe, tunaamini sasa baadhi ya matatizo yatapungua," alisema Masige.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Songwe, Mhandisi Suleiman Mshanga, alisema kampuni hizo zilionyeshwa maeneo yote muhimu kwa ajili ya kupata baadhi ya vifaa na kuwaelekeza mahitaji halisi ya mradi.



# Bunge lashindwa kuihoji h'shauri kisa hoja za CAG

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imeshindwa kuihoji Halmashauri ya Korogwe kutokana na hesabu zake kuwa na kasoro nyingi ikiwamo kushindwa kujibu hoja 91 za muda mrefu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Maimuna Mtanda, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza kuzihoji Halmashauri za Mkinga na Korogwe.

"Halmashauri ya Mkinga tumekutana nao, tumewahoji tumetoa maagizo yetu mambo hayakuwa mabaya sana lakini tulipofika kwa Halmashauri ya Korogwe imebidi tuwarudishe tusiwahoji hesabu zao, kwa sababu zinamatatizo mengi kwanza hawajajibu hoja za CAG wana hoja 91 ambazo hawajajibu na ni hoja za muda mrefu," alisema na kuongeza:

"Zipo hoja chache za mwaka 2020/21 lakini nyingi ni za nyuma lakini hawatekelezi maagizo ya Kamati ya Bunge wana maagizo matano na mengine ni ya muda mrefu bado hawajatekeleza hadi leo kwa hiyo tuliona hakuna sababu ya kuendelea kuhojiana wakati hawajatekeleza chochote," alisema Mtanda.

Alisema halmashauri hiyo imeshindwa kutekeleza maagizo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan, aliyatoa wakati akipokea ripoti ya ukaguzi iliyotolewa na CAG ya mwaka 2020/2021, alisisitiza sana halmashauri kuenda kujibu hoja za mkaguzi.

"Lakini mbaya kuliko ukienda kwenye vitabu vyao kuna mambo mengi yapo kwenye miradi kuna miradi imetelekezwa, mingine ya ujenzi wa wodi za wanaume na wanawake ni ya muda mrefu imetelekezwa kwa hiyo ni halmashauri ambayo tayari katika miaka tisa imeshaitwa mbele ya Kamati ya Bunge mara nne tukajua tayari wameshajifunza lakini bado," alisema.

Kadhalika, alisema kutokana na hali hiyo wameamua kuirudisha na kuikabidhi kwa Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI),waende kuisimamia kwa sababu kuna mambo ambayo yapo ndani zaidi yanahitaji watu vyombo vya dola wayapitie.

Hata hivyo, alisema pamoja na uwapo wa hoja nyingi za CAG, lakini bado vitabu vinaonyesha halmashauri hiyo imeshindwa kukusanya mapato ambayo ndiyo uhai wake, kuna mwaka takwimu zinaonyesha ilishindwa kukusanya kwa asilimia 60.




Wasamaria wema wakimwokoa mwendesha bodaboda uvunguni mwa gari baada ya kugongwa na kutumbukia kwenye mtaro wa barabara ya Meriwa jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wizara ya Kilimo, Vodacom wasajili wakulima mil. 1.8

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Kilimo kwa kushirikiana na Kampuni ya Teknolojia na Mawasiliano ya Vodacom Tanzania PLC na Benki ya CRDB imesajili wakulima milioni 1.8 kupitia programu ya kidijitali ya M-Kulima.

Programu hiyo ni maalumu kwa kuwawezesha wakulima kupata taarifa mbalimbali za kilimo ikiwamo mbolea ya ruzuku.

Taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano Vodacom ilimnukuu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, katika andiko lake aliloliweka katika moja ya kurasa zake za kijamii akieleza kuwa idadi hiyo ni sawa na asilimia 25 ya wakulima wote nchini.

"Kwa siku hizi 60, tumefanikiwa kusajili asilimia 25 ya wakulima, huku lengo letu likiwa ni kusajili kidijitali wakulima wote nchini, ifikapo Desemba mwaka huu, inakadiriwa kwamba jumla ya wakulima wote nchini ni milioni saba, mpaka mwisho wa mwaka huu lazima tuwe tumewasajili wakulima wote nchini," alisema Bashe.

Bashe alifafanua kwamba usajili huo mbali na kuwapa unafuu wakulima kwa kupewa mbolea ya ruzuku, lakini utaisaidia serikali kufahamu tabia za matumizi ya wakulima pamoja matumizi ya pembejeo kwa wakulima.

Alisema katika suala la umiliki wa ardhi, wanaume wanaongoza kumiliki ardhi kwa asilimia 59, huku wanawake wakimiliki ardhi kwa asilimia 41.

Aidha, aliwashukuru Vodacom na CRDB kwa kuiamini Wizara ya Kilimo na kushiriki katika kufanikisha malengo yake ya kusajili wakulima wote nchini.

M-Kulima ni mfumo unaolenga sekta ya kilimo nchini, ikiwa ni njia bora na rahisi ya kuwasiliana na kufanya miamala na wakulima.

M-Kulima inahakikisha kuwa malipo hufanywa kwa wakulima kupitia huduma ya M-Pesa na hivyo matokeo yake huunda uwazi na kupunguza hatari ya ulaghai ama kuibiwa.

Pamoja na faida za malipo, mfumo huu uliobuniwa na Vodacom sasa unatumika na serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Mfuko wa Taifa wa Mbolea (TFRA), ili kusajili wakulima katika maeneo yote nchini waweze kupata mbolea ya ruzuku.

# TVLA: Matumizi holela dawa za mifugo janga la dunia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Dk. Stella Bitanyi, amesema ifikapo mwaka 2030 watu zaidi ya milioni 10 duniani watakufa kila mwaka kutokana na matumizi holela ya dawa za mifugo ambayo yamekuwa yakisababisha vimelea vya magonjwa kujenga usugu.

Alibainisha hayo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za wakala huo.

Alisema upo umuhimu wa kupima na kujua ugonjwa unaomsumbua mnyama ili kuweza kutoa tiba sahihi.

"Kuna umuhimu mkubwa katika kupima na kujua ugonjwa unaomsumbua mnyama ili kuweza kutoa tiba sahihi. Hii husaidia kuondoa tatizo la kutibu kwa majaribio jambo ambalo kusababisha mfugaji kutumia dawa aina nyingi zinazoweza kusababisha kujenga usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa," alisema.

Aliongeza: "Aidha matumizi ya kiholela ya dawa hasa za antibaiotiki huweza pia kuathiri binadamu kutokana na kula mabaki ya dawa hizo kwenye vyakula vinavyotokana na wanyama.

"Hili ni tatizo kubwa linaloikabiri dunia kwasasa na wafugaji wanapaswa kuzingatia ushauri unaotolewa ili kudhibiti. Inakadiriwa kwamba kufikia mwaka 2030 watu zaidi ya milioni 10 watakufa kila mwaka kutokana na dawa kushindwa kuwatibu kwani vimelea vya magonjwa vitakuwa vimejenga usugu unaotokana na matumizi holela ya dawa kwa binadamu na mifugo," alisema Dk. Bitanyi.

Akielezea kuhusu majukumu ya wakala huo alisema kupitia maabara zake hupokea sampuli za wanyama mbalimbali kwa ajili ya kufanya uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya mifugo.

Alisema njia za uchunguzi zinazotumika ni pamoja na kuchunguza vimelea vya magonjwa kwa kutumia hadubini kuchunguza viashiria vya uwapo wa kinga dhidi ya kimelea kwenye damu kwa kutumia ELISA na kipimo cha juu kabisa cha uchunguzi wa aina ya kimelea kwa kutumia vinasaba yaani PCR.

Kuhusu uzalishaji na usambazaji wa chanjo za mifugo, alisema wakala unatekeleza jukumu hilo kupitia Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI) iliyoko Kibaha mkoani Pwani.

Alisema hivi sasa TVI, Kibaha inazalisha chanjo saba na uzalishaji kwa mwaka 2021/2022 ulifika dozi milioni 65.

Alizitaja chanjo zinazozalishwa na wakala huo kuwa ni chanjo stahimilivu joto ya kukinga kuku dhidi ya ugonjwa wa mdondo, chanjo ya ugonjwa wa kimeta, chanjo ya ugonjwa wa chamavu, chanjo ya homa ya mapafu ya ng'ombe, chanjo ya ugonjwa wa kutupa mimba, chanjo mchanganyiko wa kimeta na chambavu na chanjo ya homa ya mapafu ya mbuzi.

## 'Tuwafundishe watoto utamaduni wa mataifa mbalimbali'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdallah Salim amesema suala la utamaduni ni muhimu hasa kuwafundisha watoto kuanzia ngazi ya elimu ya maandalizi, msingi na sekondari ili wafahamu utamaduni wa mataifa mbalimbali ulimwenguni.

Aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya Siku ya Utamaduni ya Shule ya Feza.

Alisema hivi sasa dunia inapiga hatua katika utandawazi hivyo ni wajibu kwa watoto kufahamishwa tamaduni zilizo bora katika maisha yao.

Salim alisema watoto wengi wanapokuwa shuleni huwa na wigo, hivyo aliupongeza uongozi wa shule hiyo kwa uwamuzi wa kuwa na siku maalum ya utamaduni.

Alisema hatua hiyo ni nzuri kwani inawajenga watoto kuwa wazalendo na utamaduni wao.

Kadhalika alisema wakati umefika kwa shule hiyo na zingine kubuni mipango ya kuonyesha utamaduni wa ngoma na maonyesho ya filamu za maigizo na isiwe utamaduni wa mavazi pekee.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Ibrahim Yunus, alisema lengo la kuanzisha Siku ya Utamaduni ni kuonyesha kwa namna gani wanafunzi wa shule hiyo wanajuwa tamaduni za mataifa mbalimbali.

Alisema licha ya kutoa elimu ya msingi na sekondari lakini shule hiyo pia huwafundisha watoto katika mambo muhimu kwa maisha yao ya baadaye ikiwamo utamaduni wao, uzalendo na heshima katika jamii.

"Licha ya walimu kufanya kazi kubwa ya kuwasomesha watoto katika mambo yanayowahusu pia wanafanya kazi kubwa ya kuwasomesha kuhusiana maadili yao na suala zima la udhalilisha ili kuwajua watu wabaya," alisema.

Katika sherehe hizo wanafunzi wa shule hiyo walionyesha ubunifu wa mavazi ya mataifa mbalimbali ulimwenguni ikiwamo vazi la mswahili.

# Wanafunzi 88,360 Zanzibar kufanya mtihani wa taifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BARAZA la Mitihani Zanzibar limesema limejipanga kuhakikisha mitihani ya taifa kwa wanafunzi 88,360 wa kidato cha pili, darasa la nne na saba itakayoanza wiki hii inafanyika kwa kuzingatia ubora na uadilifu.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mazizini visiwani humo.

Alisema kwa upande wa mitihani ya kidato cha pili wanafunzi 33,119 wanatarajiwa kufanya mitihani hiyo kuanzia Oktoba 27 mwaka huu, kati ya wanafunzi hao wanaume ni 15,570 na wanawake ni 17,549.

"Wanafunzi darasa la saba jumla yao 25,389 watakaofanya mitihani hiyo ikiwamo wanawake 11,713 na wanaume ni 13,676," alisema.

Aidha, alisema kwa upande wa wanafunzi wa darasa la nne jumla ya watahiniwa 58,275 wanatarajiwa kufanya mitihani hiyo ikiwamo wanaume 29,852 na wanawake ni 28,423.

Alisema kwa upande wa watahiniwa wenye mahitaji maalumu wameandaliwa mitihani yao kwa mujibu wa hali ya mahitaji yao ikiwamo wanafunzi wenye uoni hafifu.

Mussa alisema wapo watahiniwa ambao wameandaliwa mtihani maalumu wa nukta nundu, kwa upande wa wanafunzi wa darasa la saba 130, wanafunzi darasa la nne wapo 293 na kidato cha pili 244.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ali Khamis, aliwataka watendaji wote watakaosimamia mitihani kuhakikisha kuwa hawajishughulishi na udanganyifu ambao ni kinyume na sheria na kanuni za mitihani.

Alisema: "Tunawaomba wasimamizi watakaosimamia mitihani hiyo pamoja na wanafunzi kujiepusha na udanganyifu unaoweza kujitokeza ambao ni kinyume na kanuni na sheria za mitihani, watakaobainika watachukuliwa hatua kali ikiwamo kufutiwa matokeo yao".



Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji (kushoto), akizungumza na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani, katika mkutano wa kumuenzi Maalim Seif Sharif Hamad uliofanyika hoteli ya Golden Tulip Mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Naibu Balozi: Uongozi hauhitaji ubaguzi kijinsia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Balozi wa Norway Zanzibar, Kjetil Schie, amesema suala la uongozi halihitaji ubaguzi wa kijinsia, hivyo wanawake wanapaswa kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuzitumia fursa mbalimbali za uongozi.

Aliyasema hayo jana Mjini Zanzibar katika Sherehe ya Maadhimisho Siku ya Mtoto wa Kike Duniani ambayo imeandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Zanzibar.

Alisema matarajio yake ni kuona watoto wa kike wanafanya maamuzi sahihi kwa kuangalia kigezo cha Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ni mwanamke wa kuigwa.

Naibu huyo aliwataka wasichana wa kike kusoma kwa bidii ili kuwa viongozi wazuri wa badaye na kuliongoza taifa.

Hivyo aliwataka wanawake kutoogopa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwa sababu jinsia zote mbili zinahaki sawa katika masuala mbalimbali.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema sauti ya mtoto wa kike bado haijasikika katika masuala mbalimbali muhimu ya nchi, hali inayoathiri mustakabali wa maisha yao.

Alisema TAMWA inaguswa na haki za mtoto wa kike katika maslahi yao ikiwamo kupata viongozi bora wa sasa na baadaye.

Aidha, alizitaka taasisi za serikali na binafsi kuendelea kubuni mikakati ya kuwainua watoto wa kike na vijana ili kuwatengeneza kuwa viongozi bora kwa Taifa.


Dk. Mzuri alisema hivi sasa dunia inazungumzia mtoto wa kike kupata usawa baada ya mapitio na maazimio ya miaka 25 iliyopita yaliyofanyika jijini Beijing, ili kujua nafasi ya mwanamke katika masuala muhimu hasa ya uongozi.

Alisema mifumo ya Zanzibar katika kumwezesha mwanamke haiko vizuri kama ilivyo Tanzania Bara, hivyo aliwataka wasichana kuungana na kupaza sauti zao ili kuepuka vikwazo katika kufikia malengo waliojiwekea.

Alisema TAMWA imeanzisha miradi ya kuwainua wanawake kwenye uongozi kwa lengo la kuwawezesha kushiriki nafasi mbalimbali za uongozi.

Mkurugenzi wa Taasisi ya PEGAO, Hafidh Abdi Said, alisema imefika wakati familia kuacha kumkandamiza mtoto wa kike kwa kuwatumikisha kazi badala yake kuwawezesha katika masomo na mambo muhimu ya maisha yao.

Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Jamila Mahmoud Mohammed, aliushukuru ubalozi wa Norway kwa kusaidia kufanya shughuli mbalimbali Zanzibar ambazo zinalenga kuwasaidia watoto wa kike kupata fursa za kushirikishwa katika ngazi za maamuzi.





# Bashe akunwa ujenzi Bwawa la Majitaka Nzega

**Na Halima Ikunji,**TABORA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amelidhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bwawa la majitaka katika Halmashauri ya Mji wa Nzega mkoani Tabora.

Mradi huo unatekelezwa kwa usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Nzega (NZUWASA) kwa Sh. bilioni mbili.

Bashe alitoa pongezi hizo wakati akizungumza na viongozi wa serikali na wananchi wa Kata ya Uchama wilayani humo. Alisema thamani ya fedha inaonekana kwa asilimia kubwa kulingana na kazi zinazoendelea kufanyika na zile ambazo zimekamilika kwa asilimia 100.

Bashe alisema mradi huo utakuwa na faida kubwa katika kuhifadhi na kutunza mazingira katika Mji wa Nzega, huku wakulima wakitegemea kunufaika kwa kupata mbolea ambayo itazalishwa kutokana na mji taka.

"Nataka kusema mradi huu ni mkubwa sana hapa Nzega na utasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na magonjwa ya mlipuko ambayo yanaweza kusababishwa na mifumo duni ya utunzaji wa maji taka," alisema Bashe.

Alisema baada ya mradi huo kukamilika wataanza maandalizi ya mfumo wa maji taka kutoka majumbani kwenda eneo la bwawa hilo ili kuondoa usumbufu wa kunyonya maji taka kwa kutumia magari.

Mkurugenzi wa NZUWASA, Mhandisi Athumani Kilundumya, alisema fedha za utekelezaji wa mradi huo ni Sh. bilioni mbili.

Alisema mradi huo utatekelezwa kipindi cha miezi 12, ulianza rasmi Aprili mwaka huu na hadi sasa umefikia asimilia 90 ya utekelezaji wake, huku akibainisha kuwa ifikapo Desemba mwaka huu utakuwa umekamilika.

Mhandisi Kilundumya alisema mradi huo utakapokamilika utakuwa ni mradi wa pili katika halmashauri zote nchini kwani halmashauri yenye mfumo wa maji taka kwa sasa ni Halmashauri ya Mji wa Kahama pekee.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Nzega, Maganga Sengerema, alipongeza usimamizi mzuri unaofanywa na Mkurugenzi wa NZUWASA katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji katika Mji wa Nzega.

Alisema endapo wakulima wataanza kunufaika na mbolea itakayozalishwa kutokana na majitaka itapunguza gharama za ulishaji mashambani na kuongeza tija katika kilimo.



Wanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Brilliant, Aziza Hussein (kuli) na Joseph Traimo, wakielezea kuhusu fuvu la binadamu wakati wa mahafali ya 12 ya shule hiyo, Mbezi Kimara kwa Msuguri, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Watoto wenye magonjwa sugu kupewa bima afya bure

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKA la World Vision Tanzania linatarajia kutoa bima za afya kwa watoto 69 wanaotoka katika mazingira magumu na wenye magonjwa sugu.

Bima hizo ni za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwamba zaidi ya Sh. milioni 7.5 zitatumika katika mchakato huo ili ziwasaidia kupata matibabu kwa kipindi cha miaka miwili pekee.

Mratibu wa mradi wa Iyenze- Kilago kutoka shirika hilo, Dominick Mbamba alibainisha hayo wakati akitoa taarifa katika kikao cha majumuisho baada ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ya afya na elimu.

Alisema World Vision Tanzania pia itatoa bima za CHF iliyoboreshwa kwa kaya 300 wanaoishi katika mazingira magumu sawa na wanufaika 1,800 katika kata za Iyenze na Kilago zitakazogharimu Sh. milioni 12 kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kukabiliana na gharama za matibabu bure.

Alisema pia linatarajia kutoa vifaa tiba katika Kituo cha Afya Iyenye na Zahanati ya Kilango vya Sh. milioni 20 ili kuboresha upatikanaji wa vifaa tiba na matibabu kwa wananchi.

Mbamba alisema katika kuwabaini watoto hao wanashirikiana na serikali za vijiji, watendaji wa kata na ustawi wa jamii kupitia mikutano ya hadhara inayofanyika katika vijiji.

Alisema wananchi ndiyo wanaopendekeza majina ya watoto hali ambayo inasaidia kutoibuka malalamiko ya upendeleo.

Diwani wa Kata ya Iyenye, Lucas Makulumo alisema, kata yake ina watoto wengi wenye kuhitaji msaada na kwa msaada wa bima hizo utasaidia kuondoa gharama za matibabu kwa wananchi hususani pale wanapofika katika zahanati na vituo vya afya kupata matibabu.

Alisema vifaa tiba vitasaidia kuondoa adha kwa wananchi kutembea umbali mrefu kutafuta huduma katika Hospitali ya Wilaya kutokana na baadhi ya huduma kutopatikana.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya aliitaka Manispaa ya Kahama kutenga fedha kupitia mapato yake ya ndani za kuiendeleza miradi hiyo.

# Shinyanga yaanza kutekeleza agizo la Waziri Mkuu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MANISPAA ya Shinyanga imeanza kutekeleza agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa la kuongea na wafanyabiashara ili kushusha bei za bidhaa katika mji huo.

Akiwa mkoani Mwanza Majaliwa aliwaagiza wakurugenzi na wakuu wa wilaya kuongea na wafanyabiashara kushusha bidhaa hususani zinazozalishwa ndani.

Imeelezwa kuwa mfumko wa bei za bidhaa katika Manispaa ya Shinyanga umeidumaza manispaa hiyo kimaendeleo, kusababisha wananchi wengi kukimbilia maeneo mengine kupata mahitaji yao ikiwamo wilayani Kahama.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, alibainisha hayo juzi kwenye kikao na wafanyabiashara wa manispaa hiyo kilichohusu kujadili namna ya kukuza mzunguko wa fedha.

Alisema Wilaya ya Kahama imekuwa kwa kasi kimaendeleo kutokana na kuwapo kwa mzunguko mkubwa wa fedha, sababu watu zaidi ya milioni mbili wanaingia kila siku na kutoka kwenda kupata mahitaji yao ambapo bei za bidhaa zao zipo chini.

"Mji huu wa Shinyanga ambao ndiyo makao makuu ya Mkoa tunaujua sisi wenyewe kimaendeleo, naombeni wafanyabiashara punguzeni bei za bidhaa zenu ili tuongeze mzunguko wa kifedha, watu wetu hapa wasikimbilie tena Kahama wala Mwanza kupata huduma bali watimize mahitaji yao hapa hapa,"alisema Satura.

Alisema licha ya kuboresha miundombinu ya kibiashara, pia wanatarajia kupandisha hadhi vyuo vya kati vilivyoko Manispaa ya Shinyanga ili viwe vyuo vikuu, kikiwamo Chuo cha Ushirika Moshi na Afya Kolandoto, ambavyo vitaongeza idadi ya watu kuwa wengi na kusababisha mzunguko mkubwa wa fedha.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara Mkoa wa Shinyanga Dk. Kulwa Meshack, alisema maendeleo ya eneo husika yanaletwa na wananchi wenyewe, kutoa wito kwa wafanyabiashara hasa wa vifaa vya ujenzi kupunguza bei ya bidhaa zao.

Mmoja wa wafanyabiashara ambao walihudhulia kikao hicho, Joyce Yegina, alisema tatizo la mfumuko wa bei za bidhaa katika Manispaa ya Shinyanga linasababishwa na baadhi ya wafanyabiashara kufanya biashara kimazoea pamoja na kukosa uzalendo.

## Ebola yaingia Kampala visa vitatu

**KAMPALA,** Uganda

WAZIRI wa Afya wa Uganda, Jane Ruth Aceng, amesema watu watatu waliokuwa wametengwa katika Hospitali kuu ya Mulago jijini Kampala wameambukizwa ugonjwa wa ebola.

Kwa mujibu wa waziri wa afya watu hao watahamishiwa katika kitengo cha matibabu mjini Entebbe. Visa hivyo vilivyothibitishwa ni vya kwanza kujulikana katika mji mkuu wa Kampala.

Hapo awali wizara ya habari ilisema kwamba mlipuko wa ebola nchini humo unadhibitiwa na unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwaka.

Taarifa ya serikali iliyotolewa Ijumaa jioni ilisema watu 65 wameambukizwa ugonjwa huo na vifo vilikuwa 27. Haikuwa wazi ikiwa idadi hiyo inajumuisha maambukizi mapya ya watu watatu wa mjini Kampala.

Serikali imetangaza hatua za kukabiliana na maambukizi ya ebola kwa wiki tatu karibu na wilaya za Mubende na Kassanda katikati mwa Uganda. **DW**

## Johnson, Sunak wazungumzia uwaziri mkuu wa Uingereza

**LONDON,** Uingereza

RIPOTI mbalimbali za vyombo vya habari nchini Uingereza zimeeleza kwamba waziri mkuu wa zamani Boris Johnson amefanya mazungumzo ya ana kwa ana na Rishi Sunak.

Wanasiasa hao wanaripotiwa kujiweka tayari kuzindua kampeni za kuwania uongozi wa Chama cha Conservative na hatimaye uwaziri mkuu. Johnson na Sunak ambaye ni waziri wake wa zamani wa fedha bado hawajatangaza rasmi azma ya kumrithi Liz Truss ambaye alijiuzulu hivi karibuni.

Jonhson amekatisha likizo na kurejea nchini humo juzi akikusudia kutangaza nia ya kuomba muhula wa pili kama waziri mkuu.

Kinyang'anyiro hicho huenda kikamkutanisha na Sunak ambaye kujiuzulu kwake Julai kama waziri wa fedha kulichochea Johnson kuachia madaraka.

Wagombea wanaotaka kumrithi Truss wanatumia mwisho wa juma kutafuta uungwaji mkono wa kutosha kabla ya muda wa mwisho leo. **DW**



# Russia yazidi kulipua mitambo ya umeme

• Ukraine yahofia kukumbwa na janga baya

**KYIV,** Ukraine

RUSSIA imeendelea kuishambulia vikali Ukraine, ikilenga mitambo na gridi ya nishati ya umeme na kusababisha hofu ya kuwepo janga la kibinadamu.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, alisema mashambulio hayo yalikuwa katika kiwango cha juu sana yakipiga mikoa ya magharibi, katikati, kusini na mashariki.

Kutokana na mashambulizi hayo ya makombora, karibu kaya milioni 1.5 hazikuwa na umeme katika mji mkuu wa Kyiv.

Kiongozi huyo alisema makombora mengi na ndege zisizo na rubani zilikuwa zikidunguliwa na alisisitiza mashambulio kama hayo hayatazuia harakati za kijeshi za nchi yake.

"Kwa kweli, bado hatuna uwezo wa kiufundi wa kutungua asilimia 100 ya makombora ya Russia na ndege zisizo na rubani. Hatua kwa hatua tutafikia kwa msaada wa washirika wetu, nina uhakika na hili," kiongozi huyo alisema katika ujumbe wake kwenye video uliotolewa jana.

Takriban theluthi moja ya vituo vya umeme vya Ukraine na vituo vingine vya kuzalisha nishati vimeharibiwa katika wimbi la mashambulizi ya anga tangu Jumatatu wiki iliyopita.

Maeneo yanayolengwa na mashambulizi ya hivi sasa ni pamoja na eneo la Cherkasy, Kusini-Mashariki mwa mji mkuu Kyiv, na mji wa Khmelnytskyi ulioko magharibi.

> **Mipango hiyo inatoa sababu ya kufikiria kwamba Russia inaweka fedha nyingi katika maandalizi ya ulinzi kwenye kuelekea maeneo ya vitani kwa sasa, pengine kwa lengo la kukomesha mashambulizi ya haraka ya Ukraine.**

Mashambulizi ya anga na ukatikaji wa umeme pia viliripotiwa kutoka Odesa kusini hadi Rivne na Lutsk Kaskazini-Magharibi.

Opereta wa kitaifa wa umeme, Ukrenergo, alisema mashambulizi hayo yanaweza kusababisha uharibifu zaidi kuliko mashambulizi makali ya mabomu mapema mwezi huu.

Rais Zelensky alisema kuwa roketi 36 zilirushwa jana pekee na mengi kati yao zilitunguliwa.

Alisisitiza katika hotuba yake kuwa maofisa walifanikiwa kurejesha umeme katika mikoa mingi ya nchi hiyo.

**WARUSSIA WAJENGA MIUNDO YA ULINZI**

Ujasusi wa Uingereza katika ripoti fupi ya asubuhi ya jana juu ya vita, ilitoa maoni kuhusu taarifa za mfanyabiashara Yevgeny Prigozhin kuanza ujenzi wa miundo ya ulinzi inayoitwa "Wagner line" katika eneo la Luhansk.

Ikiwa kiwango cha mipango kinalingana na taarifa za Prigozhin, kazi hizi zinaweza kuwa na lengo la kuunganisha Mto wa Donets wa Siversky kwenye eneo la ulinzi, na kurudia mpaka wa 2015, ripoti hiyo ilisema.

"Mipango hiyo inatoa sababu ya kufikiria kwamba Russia inaweka fedha nyingi katika maandalizi ya ulinzi kwenye kuelekea maeneo ya vitani kwa sasa, pengine kwa lengo la kukomesha mashambulizi ya haraka ya Ukraine", wataalamu wanaongeza.

Ni msururu wa vizuizi vya kuzuia makombora iliyojengwa hivi karibuni ambayo huanza kutoka mpaka wa Russia mashariki mwa Luhansk na kisha kuelekea kaskazini-magharibi hadi Kremia ambapo inageuka kwenda kusini.

Eneo hilo hutenganisha sehemu ya kawaida ya kaskazini ya mkoa wa Luhansk kutoka sehemu ya kusini.

Hapo awali katika mitandao ya kijamii, wataalamu na wanablogu wa kijeshi walipendekeza kuwa vikosi vya wanajeshi vya Ukraine vinaweza kutaka kujitenga na kisha kukomboa eneo la kaskazini mwa mkoa wa Luhansk. **BBC**



Moto ukiteketeza mtambo wa kuzalisha umeme baada ya kulengwa na makombora ya Russia juzi usiku. **PICHA: REUTERS**

# Xi Jinping achaguliwa tena kuiongoza China

**BEIJING,** CHINA

RAIS wa China, Xi Jinping amechaguliwa tena kuwa katibu wa chama kwa muhula wa tatu mfululizo.

Xi Jinping amehutubia vyombo vya habari, akisema kwamba chama kilimaliza kwa mafanikio kongamano lake, kwa kushikilia bendera yetu, kuunganisha nguvu zetu na kusonga mbele kwa umoja.

Pia alibainisha kuwa jumuiya ya kimataifa imekuwa ikifuatilia kongamano hilo kwa shauku kubwa na wakuu wa nchi wametuma salamu za pongezi na barua na aliwashukuru wote.

Kisha akatambulisha safu yake mpya katika kamati ya kudumu ya chama na kuongeza wote wanajulikana kwa wanachama.

Xi, mwenye miaka 69, ndiye kiongozi wa chama mwenye nguvu zaidi tangu kiongozi wa kwanza wa zama za kikomunisti Mao Zedong aliyefariki mwaka 1976.

Aidha, kiongozi huyo alitangazwa kuwa ataendelea kuwa Mwenyekiti wa Tume Kuu ya Kijeshi, ikimaanisha kuwa yeye ndiye kamanda anayesimamia Jeshi la Ukombozi la Watu wa China.

Hiyo ina maana kwamba Xi ni katibu wa chama, kamanda wa kijeshi na kwa hakika atakuwa pia rais wa China ambaye anahitaji tu uthibitisho wa kiufundi katika kura ya wabunge mapema mwaka ujao. **DW**

# Uhuru wa vyombo vya habari ni msingi kukuza demokrasia

**Na Jenifer Gilla**

BALOZI wa Uholanzi nchini Tanzania, Dk. Wiebe De Boer, amesema uhuru wa habari ni msingi katika kukuza demokrasia nchini kwa kuwa hutoa nafasi ya kuibua mijadala, kutoa miongozo ya utungwaji wa sheria zinaloteta mwelekeo chanya kwa taifa.

Dk. Wiebe aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati akifungua semina ya mabadiliko ya Sheria ya Habari iliyoandaliwa na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

"Chombo cha habari kikiwa huru kinaweza kuwa ni mkono wa nne wa uongozi katika nchi. Nasema uongozi na sio serikali. Kwahiyo majadiliano kuhusu Sheria ya Vyombo vya Habari kwa namna ambayo waandishi wa habari watafanya kazi zao kwa uhuru, ina maslahi makubwa sana," alisema.

Alisema nchi hiyo ipo tayari kuisaidia TEF katika mipango yake kwa kuwa inaamini kuwa uhuru wa vyombo vya habari ni msingi wa ukuaji wa demokrasia unaosaidia kuwapo na uamuzi mzuri na kuboresha maisha ya wananchi.

Naye Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema kuwa baadhi ya sheria za habari zinawabana waandishi wa habari na kusababisha kushidwa kufanya kazi kwa weledi na kutetea haki na maslahi yao.

Aidha, alisema sheria hizo hazifundishwi kwa kina shuleni na kusababisha waandishi wengi kutozifahamu vizuri na kushindwa kueleza matatizo wanayokutana nayo katika kazi zao.

Alisema kwa kushirikiana na wadau wa habari nchini ikiwamo Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, tawi la Tanzania (MISA-Tan), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) na Baraza la Habari Tanzania (MCT), wapo katika mchakato wa kuwaomba watunga sera kuvifanyia marekebisho baadhi ya vifungu vya sheria ya habari vinavyoonekana na kuwa kikwazo kwa kazi za wanahabari.

Mmoja wa waandishi wa habari waliohudhuria semina hiyo, Veronica Mrema, alisema mafunzo hayo yamemwongezea uwelewa kuhusu Sheria ya Vyombo vya Habari kwa sababu amefahamu vizuri baadhi ya vifungu vya sheria ya habari ambavyo hakuvijua.




Mkuu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Prof. Hozen Mayaya, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za chuo hicho na mwelekeo wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Chumvi nyingi chanzo magonjwa ya moyo

**Na Shaban Njia, BUKOMBE**

MATUMIZI ya chumvi nyingi katika chakula yametajwa kuwa miongoni mwa visababishi vya magonjwa ya moyo kwa watu wengi katika jamii na kuhatarisha maisha yao.

Hayo yamebainishwa na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa Hospitali ya Rufani Kanda Bugando, Prof. William Mahalu, wakati akitoa huduma ya matibabu ya moyo bila malipo katika Kliniki ya Baraka Charles Kulwa Memorial Hospitali wilayani Bukombe mkoani Geita.

Alisema kuna aina mbili za magonjwa ya moyo, wa kuzaliwa nao na mtu anaopata katika matumizi ya vyakula mbalimbali, ikiwa ni pamoja na chumvi nyingi.

Alieleza pamoja na sababu hiyo mtu anaweza kupata ugonjwa wa moyo kutokana na matumizi ya sigara, kutokujishughulisha na kazi mbalimbali pamoja na vyakula vyenye mafuta mengi.

Prof. Mahalu alisema Siku ya Moyo Duniani, wanaifanya kwa kuwafikia wananchi na kuwapatia elimu ya ugonjwa huo na dalili zake ili kufahamu chanzo chake na jinsi ya kujikinga.

"Magonjwa mengi yanayowakabili binadamu ni endelevu na ndio maana tunashauri watu wanapobaini kupata dalili ndani ya mwili ambazo sio nzuri kufika katika vituo vya afya kupata matibabu," alisema Prof. Mahalu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Hospitali ya Charles Kulwa Memorial Baraka, Charles Kulwa, alisema wamekuwa wakishirikiana na madaktari bingwa kutoa huduma mara kwa mara kwa wananchi, kwa wiki wanatoa mara moja bila malipo.

Mmoja wa wakazi wa Bukombe, Swaum Ibrahimu, alisema awali alikuwa hafahamu kama chumvi inaweza kuwa chanzo kikubwa cha kupata ugonjwa wa moyo na atahakikisha anaitumia kwa makini ili kumletea shida na kushindwa kutimiza ndoto zake za kimaisha.

Naye Nicodemas Lucas aliomba elimu hiyo itolewe katika vituo vya afya hususan kliniki ili wajawazito wanapofika kujua maendeleo ya mtoto tumboni wafahamu kuwa chumvi ni chanzo cha kupata ugonjwa huo.

## Washerehekea kuzaliwa Mtume Muhammad (SAW)

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA jamii ya Bohora wameungana na wenzao duniani kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume Mohammed (SAW) na kiongozi wao Dk. Syedna AliQadr Mufaddal Saifuddin TUS.

Sherehe hizo jijini Dar es Salaam zilifanyika juzi katika Masjid za mitaa ya Zanaki na Upanga na barabara ya Alykhan kwa waumini hao waliovalia mavazi ya kitamaduni kuandamana.

Maandamano hayo yalipambwa kwa magari, baiskeli, farasi, bendi ya Magereza, Raj Band na Skauti.

Vishada vyenye jumbe mbalimbali kutoka kwa mtakatifu wa Bohora na Rais Samia Suluhu Hassan vilirushwa angani vikielezea umuhimu wa kudumisha amani na upendo.

Ujumbe kutoka kiongozi wa Bohora, uliwataka waumini wa Kiislamu kufuata misingi ya dini na kuwa waaminifu na kuombea nchi amani na utulivu.

## Chuo cha Mipango kuongeza udahili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHUO cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) katika mwaka huu wa fedha kimepanga kuongeza udahili na usajili wa wanafunzi kutoka 14,417 mpaka kufikia wanafunzi 16,663.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Hozen Mayaya, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya utekelezaji wa vipaumbele vya bajeti katika chuo hicho katika mwaka wa fedha 2022/23.

Prof. Mayaya alisema chuo hicho kinaendelea kupitia mitaala ya mafunzo ya muda mrefu na kuandaa mitaala ya kozi mpya na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga miundombinu ya kufundishia.

Alitaja vipaumbele vya mwaka huu wa fedha kuwa ni kuendelea kuajiri watumishi wapya, kulipa stahili mbalimbali, kupandisha vyeo watumishi waliokidhi vigezo pamoja na kuboresha huduma za ustawi na kuongeza uwezo wa kielimu na kiutendaji kwa watumishi 396.

"Tumejipanga kufanya ukarabati mkubwa na mdogo wa nyumba 13 za watumishi, kulipa madeni ya watumishi na watoa huduma, kutekeleza shughuli ambazo hazikutekelezwa katika Mpango Mkakati wa mwaka 2016/17-2020/21 pamoja na uendelezaji wa maeneo ya Miyuji Kaskazini, Chigongwe na Kiseke," alisema.

Kuhusu utekelezaji wa majukumu ya chuo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22 Prof. Mayaya alieleza kuwa hadi kufikia Juni 2022, jumla ya watumishi 351 walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 50 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi.

# Esma atafuta mchumba

**Na Mwandishi Wetu**

DADA wa msanii namba moja Ukanda wa Afrika Mashariki, Diamond Platnumz, Esma Khan ama Esma Platnumz, ameibuka na kusema anatafuta mchumba.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Esma Platnumz alipakia picha ya ndugu yake Diamond Platnumz ambaye ni mdogo wake na kusema kwamba anatafuta mchumba mwenye macho mazuri kama ya ndugu yake huyo.

"Nyie natafuta mchumba mwenye macho mazuri kama ya mdogo wangu Naseeb. Mawifi zangu wana haki ya kulialia pamoja na kuimbiwa nyimbo za uongo na kweli, aliandika Esma.

Esma ndoa yake ilisambaratika na baadaye uhusiano wake mwingine tena ukavunjika. Ni kama sasa hivi tena amepona na yupo sokoni anataka kujaribu bahati tena.

Watumizi wa mtandao wa Instagram walitolea maoni yao tofauti tofauti kauli hiyo, huku wengine wakisema Diamond hawezi kosa mwanamke wa kumuoa hata kama atajua anamwimbia uongo kwani ni pesa na umaarufu tu wanatafuta kwa sababu macho tangu zamani msanii huyo anayo.




# ZUCHU ADAIWA KUIBA WIMBO



**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva, Zuhuru Othman maarufu Zuchu, huenda akakamuliwa Sh. milioni 500 kwa kudaiwa kuiba wimbo wa msanii wa Injili, Enock Jonas.

Katika malalamiko hayo, Jonas amedai Zuchu amechukua sehemu ya kibwagizo na staili ya kucheza katika wimbo wake wa 'Wema wa Mungu' ambao ulitoka mwaka 2012, lakini ulijulikana zaidi kwa jina la 'Zunguka'.

Taarifa za madai hayo zilianza kusambaa mitandaoni kupitia barua iliyoandikwa na Kampuni ya Wanasheria ya Gerpat Solution, ambapo mmoja wa wake, Gerlad Magubuka, amesema Oktoba 22 mteja wao alikwenda kuwalalamikia Zuchu kutumia kionjo cha wimbo wake huo.

Magabuka amesema tayari wameshawapelekea wahusika barua ya madai hayo na nakala nyingine wamepeleka Taasisi ya Hakimiliki nchini (Cosota) na Shirikisho la Wanamuziki Tanzania (Shimuta).

Kwa upande wake, Enock amesema amelazimika kuchukua hatua hiyo baada ya mazungumzo na upande wa Zuchu kushindikana kwa kumwambia kuwa katika madai hayo hawezi kumlipa hata Sh. milioni mbili.

Alisema majibu hayo alipewa na mmoja wa mameneja katika Lebo ya Wasafi, Khamis Taletale (Babu Tale), baada ya kuzungumza naye kwa njia ya simu Jumanne.

Kwa upande wa Cosota kupitia Katibu Mtendaji wake, Doreen Sinare, amekiri suala hilo kutua mezani kwake na kueleza kilichofanyika ni wasanii wenyewe kuandikiana barua na wao wamepelekewa kama taarifa, hivyo hawawezi kusema lolote kwa sasa wameacha wasanii wenyewe ndio wawasiliane kwanza na baadaye wao watakuja kuichambua na kuitolea tamko.

# *Wizkid aweka rekodi Spotify*

**LAGOS,** Nigeria

MUIMBAJI na mtunzi wa nyimbo kutoka nchini Nigeria, Ayodeji Balogun, maarufu Wizkid, amepiga hatua nyingine kwa kuweka rekodi kwenye mtandao wa nyimbo wa kimataifa, Spotify.

Wizkid ameweka historia Spotify kwa kuwa msanii wa kwanza Afrika kufikisha 'streams' bilioni tano.

Wizkid ametangazwa kuwa msanii wa kwanza katika Bara la Afrika na kupitia album yake ya 'Made in Lagos' kutazamwa zaidi kwenye mtandao huo wa Spotify.

Kulingana na data ya chati kupitia Spotify, mwimbaji huyo amefanikiwa kufikisha Stream zaidi ya bilioni tano kwenye Spotify.



HABARI MICHEZO

# CRDB, SANLAM ZAMWAGA MAMILIONI TAIFA CUP 2022

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB na Kampuni ya Bima ya Sanlam Life Assurance, zimetangaza udhamini wa Sh. milioni 350 kwa Ligi ya Mpira wa Kikapu ya Taifa 2022, ijulikanayo kama "CRDB Bank Taifa Cup".

**Mashindano hayo yaliyopewa kaulimbiu ya 'Ni zaidi ya Game Ni Maisha', yatafanyika jijini Tanga kuanzia Novemba 4 na kufikia kilele chake Novemba 12, mwaka huu.**

Akizungumza katika hafla ya kutangaza udhamini huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema benki hiyo imeendelea na uamuzi wake wa kudhamini ligi hiyo ya taifa ya mpira wa kikapu kwa mara ya tatu mfululizo ikiwa ni sehemu ya jitihada za benki hiyo kuwawezesha vijana wa Kitanzania kupitia michezo.

Alisema kuwa Benki ya CRDB kupitia Sera yake ya Uwekezaji katika Jamii (CSI Policy), imekuwa ikiwekeza katika michezo ya vijana kwa kuamini kuwa inasaidia kuongeza ushiriki wao katika shughuli mbalimbali za maendeleo katika jamii.

Nsekela alisema benki hiyo kwa kushirikiana na Sanlam wameamua kuongeza udhamini mwaka huu kulinganisha na Sh. milioni 300 za mwaka jana kutokana na mafanikio ambayo CRDB Bank Taifa Cup imekuwa ikiyapata katika miaka miwili iliyopita ambapo vijana zaidi ya 3,000 wameweza kufikiwa.

"Kupitia mashindano haya mbali na kuonyesha vipaji vyao, pia wamekuwa wakipata scholarship za masomo na kupata mafunzo mbalimbali ambayo yanasaidia kuwajengea kujiamini, kujisimamia na kuzifuata ndoto zao," alisema Nsekela huku akiishukuru Kampuni ya Sanlam kwa kuendelea kuunga mkono mashindano hayo.

Akitangaza zawadi zitakazotolewa kwa washindi wa CRDB Bank Taifa Cup 2022, Nsekela alisema mshindi wa kwanza kwa timu za wanawake na wanaume watakaondoka na kitita cha Sh. milioni 10 kila mmoja na washindi wa pili wataondoka na kitita cha Sh. milioni tano.

"Pamoja na zawadi hizi za timu kutakuwa na zawadi kwa wachezaji bora wa maeneo mbalimbali na makocha. Jumla ya zawadi zote za fedha taslimu zilizotengwa mwaka huu ni Sh. milioni 32. Lakini hapo baadaye tutakwenda kutangaza zawadi nyingine za ufadhili wa masomo kwa wachezaji watakaofanya vizuri na mwaka huu tutaboresha zaidi," aliongezea.

Mgeni rasmi katika hafla ya uzinduzi huo, Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mchezaji wa Mpira wa Kikapu, Esther Matiko, alipongeza Benki ya CRDB kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kusaidia jitihada za serikali kuendeleza michezo nchini.

Matiko alisema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imeweka kipaumbele kikubwa katika michezo kwa kutambua fursa za kiuchumi zinazotokana na sekta hiyo.

Kwa upande wa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF), Michael Kadebe, aliishukuru Benki ya CRDB na Sanlam kwa kuendelea na udhamini wa ligi hiyo huku akibainisha kuwa udhamini wa taasisi hizo kubwa hapa nchini, umesaidia kuongeza hamasa na mapenzi ya mpira wa kikapu kwa vijana kama ilivyo kwa mpira wa miguu na michezo mingine.

Kadebe alimueleza Mheshimiwa Matiko kuwa mbali na udhamini unaotolewa na Benki ya CRDB, benki hiyo imekuwa ikishiriki katika kila hatua kuhakikisha mashindano hayo yanafikiwa ikiwamo na kusaidia kushawi taasisi nyingine kushiriki kufanikisha mashindano hayo.

Mashindano ya CRDB Bank Taifa Cup mwaka 2021, yalifanyika jijini Dodoma katika viwanja vya Chinangali na Uwanja wa Jamhuri ambapo vijana 1,000 kutoka kutoka mikoa yote Tanzania bara na visiwani walishiriki. Katika mashindano hayo timu za mpira wa kikapu za mkoa wa Dar es Salaam ziliibuka washindi katika michuano hiyo kwa upande wa wanawake na wanaume.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (katikati), akirusha mpira kuashiria kuanza kwa mchezo maalumu uliowakutanisha wachezaji waliokuwa bora kwenye 'CRDB Bank Taifa Cup 2020 na 2021' (MVPs), uliochezwa jana katika viwanja vya Don Bosco Oysterbay, Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya ufunguzi wa msimu wa tatu wa 'CRDB Bank Taifa Cup 2022'. Mashindano hayo kwa mwaka huu yatafanyika jijini Tanga kuanzia Novemba 4 - 12, yakishirikisha timu 16 za wanaume na 16 za wanawake. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Hitimana aanika 'gonjwa' la Azam FC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa KMC, Thierry Hitimana, amesema Azam FC bado wameathirika kisaikolojia kutokana na kuondolewa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, hivyo wao wameichukulia faida hiyo kuwaadhibu.

Hitimana ambaye alikuwa akizungumzia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Ijumaa iliyopita Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na KMC kuichabanga Azam mabao 2-1, alisema wachezaji wake wanamiliki mpira dakika 15 za mwanzo bila kutoa fursa ya wao kucheza, hivyo ikazidi kuwaondoa mchezoni na mbinu hiyo ikafanikiwa.

"Nilioongea na wachezaji, unajua wametoka kufungwa kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho kwa hiyo tukiwapa nafasi ya kuchezea mpira watatuadhibu, lakini kama tukiwanyima kwa dakika 15 mpaka 20 wataanza kuwa na maswali mengi kichwani, unajua tayari wameshaathirika kisaikolojia kwa hiyo tukifanya hivyo tutazidi kuwachanganya, na kweli mbinu hiyo imetumiwa na wachezaji wangu tukashinda," alisema kocha huyo.



Alisema kuwa bado Azam ni timu nzuri na itakaa sawa, lakini wao kama KMC wamepata ushindi kutokana na mikakati ya ufundi, pamoja na kutumia mwanya wa kutokuwa kwao sawa kisaikolojia.

Kwa matokeo hayo, KMC imefikisha pointi 13 ambazo Simba na Yanga zilikuwa nazo kabla ya mechi yao ya jana.

Timu hiyo inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni inashika nafasi ya tatu mpaka sasa, huku Azam ikiporomoka hadi nafasi ya sita ikisalia na pointi zake 11.

# *JKT Tanzania yaja juu Ligi ya Championship*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya JKT Tanzania imetangaza hali ya hatari kwa timu zilizo juu ya msimamo wa Ligi ya Championship baada ya kuichapa Ndanda mabao 2-0 na kufikisha jumla ya pointi 15, sawa na Mbuni FC pamoja na Fountain Gate.

Maafande hao ambao ilibaki kidogo wapande Ligi Kuu msimu unaondelea kama si kuzuiwa na Prisons kwenye mechi ya mchujo, walipata ushindi huo ugenini kwenye mechi iliyochezwa juzi Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi ikiweka hai matumaini yake ya msimu ujao kurudi kwenye Ligi Kuu kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Ushindi huo umeifanya timu hiyo kuwa kwenye nafasi ya tatu ya msimamo ikizidiwa mabao tu ya kufunga na timu za Mbuni FC inayoongoza ligi hiyo na Fountain Gate.

Mbuni FC ambayo mechi iliyopita ilipata kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya African Sports kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, ilisawazisha makosa yake juzi iliposhinda bao 1-0 dhidi ya Copco kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, ushindi ambao umeifanya kuendelea kuongoza kwa idadi kubwa ya mabao ya kufunga, ikiwa imeshatupia 14 mpaka sasa.

Fountain Gate ilifungwa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania wiki iliyopita, lakini juzi ilizinduka na kuachia kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Green Warriors kwenye Uwanja wa CCM Gairo na kuifanya kung'ang'ania nafasi ya pili kwa pointi hizo, lakini ikiwa imefunga mabao nane, huku JKT ikiwa na mabao saba.

Ligi hiyo imeingia kwenye raundi ya sita, huku timu ya Copco ndiyo inayoburuza mkia mpaka sasa ikiwa na pointi moja tu.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DALOT ATAKIWA MADRID

MLINZI wa kulia wa Manchester United, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 23, analengwa na Real Madrid. ***(Mirror)***

### RONALDO KUTUA CHELSEA

CHELSEA wanania ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, ambaye yuko tayari kupunguziwa mshahara ili kuondoka Old Trafford. ***(Sunday World)***

### UNITED HAIJAPATA OFA

KLABU ya Manchester United haijapokea maombi yoyote ya kumuuza Crisriano Ronaldo licha ya kuanika kwamba anapatikana kwa uhamisho wa bila malipo. ***(ESPN)***

### GERRARD APIGIWA CHAPUO

MSHAMBULIAJI wa zamani wa England, Darren Bent amesema Steven Gerrard anaweza kuwa mshindani wa kuwa kocha ajaye wa Timu ya Taifa ya England baada ya kutimuliwa na Aston Villa. ***(TalkSPORT)***

### ROSENIOR ATAJWA DERBY

KLABU ya West Brom imefanya mazungumzo na kocha wa zamani wa Derby County, Liam Rosenior, kuhusu kumpa nafasi ya ukocha. ***(Sun)***

### TROSSARD AWINDWA

KLABU ya Newcastle iko tayari kutumia pauni milioni 25 kumsajili mshambuliaji wa Brighton na Ubelgiji, Leandro Trossard mwenye umri wa miaka 27. ***(Talking Transfers, via Express)***

### KEANE AMTETEA RONALDO

NAHODHA wa zamani wa Manchester United, Roy Keane, amesema "wachezaji wameonyesha mchezo mbaya zaidi" katika klabu hiyo huku akimtetea Cristiano Ronaldo kwa kukataa kuingia kama mchezaji wa akiba dhidi ya Tottenham Jumatano iliyopita. ***(Sky Sports, via Sun)***

### BASTONI AWANIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kuwa tayari kutoa ofa ya pauni milioni 43 kumnunua beki wa Inter Milan mwenye umri wa miaka 23, Alessandro Bastoni. ***(Inter Live, via HITC)***

### VATA AIVUTIA ARSENAL

ARSENAL, Manchester City, Juventus, Roma na AC Milan wanavutiwa na kiungo wa kati wa Celtic na Jamhuri ya Ireland mwenye umri wa miaka 17, Rocco Vata. ***(Tuttomercatoweb)***

### KVARATSKHELIA ANYATIWA

REAL Madrid, Paris St-Germain na Manchester City zimetuma maskauti kumtazama winga wa Napoli na Georgia, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 21. ***(90min)***

### LOBOTKA LULU SOKONI

KIUNGO wa Slovakia, Stanislav Lobotka mwenye umri wa miaka 27, anatarajiwa kusaini mkataba mpya na Napoli, licha ya kunyatiwa na Arsenal, Liverpool na Tottenham. ***(90min)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA ATAKA ZAIDI KUTOKA KWA DE BRUYNE

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anataka zaidi kutoka kwa Kevin De Bruyne ambaye amesema hachezi katika kiwango chake cha juu licha ya kufunga bao zuri kwenye ushindi wa 3-1 dhidi ya Brighton and Hove Albion, Jumamosi.

**Mchezaji huyo Bora wa Ligi Kuu England mara mbili, aliifungia City bao la tatu kwa shuti kali la mguu wa kulia kutoka nje ya eneo la hatari dakika ya 75.**

Tangu De Bruyne acheze kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu akiwa na City Septemba 2015, amefunga mabao mengi (24) kutoka nje ya eneo la hatari kuliko mchezaji mwingine yeyote.

Bao hilo lilikuwa la pili kwa Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 31, katika msimu huu wa Ligi Kuu England huku pia akichangia pasi tisa za mabao, lakini Guardiola anatarajia zaidi.

> Kafunga bao zuri, lakini hachezi kwa ubora zaidi, si lazima nimwambie, nguvu yake bado si...

"Anaweza kuwa bora zaidi. Bado hachezi katika kiwango chake cha juu," alisema Guardiola akiwaambia wanahabari.

"Alifunga bao zuri, lakini hachezi kwa ubora zaidi. Si lazima nimwambie. Nguvu yake bado si kamilifu, anajua hilo. Nilizungumza naye.

Erling Haaland aliendeleza kiwango chake cha kushangaza kwa kufunga mara mbili kipindi cha kwanza, kumaanisha kuwa alikuwa mchezaji wa kwanza wa City kufunga katika mechi saba mfululizo za nyumbani kwenye mashindano yote tangu Sergio Aguero, Februari 2018.

Raia huyo wa Norway alionyesha kasi yake na umbo lake na kuanza kufunga dakika ya 22, kabla ya kufunga penalti dakika ya 43.

"Ningesema kwamba (Haaland) ana ubora katika nafasi kubwa, anaweza kuifanya na katika nafasi ndogo anaweza kuifanya," alisema Guardiola.

Bao la Haaland ambalo lilifanya matokeo kuwa 2-0 lilikuwa la 600 kwa City kwenye Ligi Kuu chini ya Guardiola, na kumfanya kuwa kocha wa tatu kufikia mafanikio hayo nyuma ya Sir Alex Ferguson na Arsene Wenger.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 382

MECHI KALI
WEST HAM
VERSUS
BOURNEMOUTH
1 | 1.52
X | 3.95
2 | 5.92

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP AZIDI KULIA NA KIWANGO LIVERPOOL



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amekiri kuwa haelewi jinsi timu yake ilivyoshindwa kuifunga Nottingham Forest, Jumamosi.

Wakiwa na mchezo dhidi ya Manchester City wikendi iliyopita na West Ham katikati ya wiki, Liverpool waliambulia kipigo baada ya kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa waliokuwa mkiani mwa Ligi Kuu England, Forest.

Akizungumza na BT Sport, Klopp alikubali Liverpool 'haikufanya mambo sahihi'.

"Hatukuwa kwenye ubora, tulicheza vibaya na sijawahi kuona mchezo mbaya kama huu," alisema.

"Nafasi zote tulizozipata tulishindwa kuzitumia, lakini wao walipata nafasi na kuzitumia.

"Sifa kwa Nottingham, lakini ilikuwa sisi dhidi ya golikipa, sisi dhidi yetu wenyewe na sio sisi dhidi ya Nottingham Forest."



## Ancelotti: Madrid hii ni bora zaid

**MADRID,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, anaamini kuwa kikosi cha sasa cha Real Madrid kinaweza kuwa bora zaidi kuwahi kufundisha.

Lucas Vazquez na Federico Valverde walifunga katika dakika 15 za mwisho na kuiwawezesha 'Los Blancos' hao kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Sevilla juzi, hivyo kuwafanya waongoze kwenye msimamo kwa pointi sita dhidi ya Barcelona.

Ushindi huo wa pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu ulikuwa wa tisa kwa Madrid katika mechi 10 za LaLiga msimu huu, huku kikosi hicho cha Ancelotti kikiwa bado hakijaonja kipigo katika mashindano yote.

Ancelotti, ambaye ameshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa vipindi viwili tofauti akiwa na klabu hiyo, amesema wachezaji wa sasa wanaweza kuwa bora zaidi kuwahi kuwaongoza katika maisha yake ya soka.

"Sijui kama ni timu inayotegemewa zaidi katika
maisha yangu ya ukoch
lakini ni timu ninay
penda kufundisha
alisema katika mkutan
na waandishi wa haba
baada ya mechi.

"Ni timu ambayo hain
pi matatizo, ambayo ni y
heshima. Na kama ubor
ni mojawapo ya bora zai
ambayo nimewahi kuw
nayo."

"Hizi ni rasilimali amb
zo tunazo kwenye bench
Kikosi kiko na afya nzu
wakati wale wanaochez
kidogo wanaingia uwa
jani na kufanya vizu
sana," aliongeza.

2,731,410

JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/10/22 | 22:00 | RB Leipzig vs Real Madrid | 2.87 | 3.42 | 2.28 |
| 02. 26/10/22 | 02:00 | CA Platense vs Lanus | 2.30 | 3.13 | 3.38 |
| 03. 26/10/22 | 22:00 | Eintracht Frankfurt vs Marseille | 2.29 | 3.26 | 2.97 |
| 04. 26/10/22 | 22:00 | Barcelona vs Bayern Munchen | 2.38 | 3.53 | 2.66 |
| 05. 27/10/22 | 01:00 | Botafogo RJ vs Bragantino SP | 2.43 | 3.11 | 2.72 |
| 06. 27/10/22 | 03:45 | Goias vs America Mineiro MG | 2.68 | 3.02 | 2.53 |
| 07. 27/10/22 | 19:45 | Ludogorets Razgrad vs Betis | 2.95 | 3.45 | 2.26 |
| 08. 27/10/22 | 19:45 | Fenerbahce vs Rennes | 2.59 | 3.19 | 2.69 |
| 09. 27/10/22 | 19:45 | AEK Larnaca vs Dynamo Kiev | 3.25 | 3.40 | 2.18 |
| 10. 27/10/22 | 19:45 | Austria Vienna vs Lech Poznan | 2.59 | 3.34 | 2.59 |
| 11. 27/10/22 | 19:45 | PSV Eindhoven vs Arsenal | 2.68 | 3.51 | 2.42 |
| 12. 27/10/22 | 22:00 | Nantes vs Karabakh | 2.42 | 3.40 | 2.75 |
| 13. 27/10/22 | 22:00 | Sivasspor vs CFR Cluj | 2.26 | 3.24 | 3.24 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 24/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2026 | Hawassa Kenema SC vs Dire Dawa Kenema FC | 2.36 | 2.95 | 3.25 |
| 14:00 | 1288 | Aksu vs Ordabasy | 2.45 | 3.28 | 2.59 |
| 14:30 | 2310 | Shandong Luneng vs Guangzhou Evergrande | 1.18 | 6.00 | 11.61 |
| 15:00 | 1417 | FK Radnicki Beograd vs Indjija | 11.60 | 5.03 | 1.23 |
| 15:00 | 1861 | Tianjin Teda vs Wuhan Zall | 1.44 | 4.18 | 6.03 |
| 15:00 | 2299 | Yenisey Kr vs Ufa | 1.99 | 3.17 | 3.56 |
| 15:00 | 4922 | FK Novi Sad vs FC Rad | 2.72 | 2.91 | 2.57 |
| 15:00 | 5113 | Shenzhen vs Hebei Zhongji | 1.15 | 6.26 | 13.68 |
| 15:30 | 5817 | Gomel vs Isloch | 2.81 | 3.20 | 2.32 |
| 15:45 | 1687 | AL Ain vs Hajer Club | 2.59 | 2.78 | 2.83 |
| 16:00 | 1510 | Ghazl EL Mahallah vs Ismaily SC | 2.54 | 2.79 | 3.09 |
| 16:00 | 2446 | Singida BS FC vs Ihefu FC | 1.97 | 3.05 | 4.30 |
| 16:00 | 5209 | Aktobe vs FK Arys | 1.40 | 4.50 | 7.40 |
| 17:30 | 4567 | Ural Yekaterinburg vs Kryliya Sovetov | 2.63 | 3.28 | 2.53 |
| 18:00 | 1774 | Levadiakos vs AEK Athens | 7.59 | 4.20 | 1.42 |
| 18:15 | 4001 | Petrolul Ploiesti vs Argesul Pitesti | 2.43 | 3.07 | 2.92 |
| 18:30 | 1527 | Bassam vs Sporting Gagnoa | 4.76 | 3.21 | 1.73 |
| 18:30 | 2237 | NK Radomlje vs Luka Koper | 3.26 | 3.40 | 2.00 |
| 19:00 | 1247 | Flora II vs Paide Linnameeskond | 1.70 | 5.00 | 3.55 |
| 19:00 | 1494 | AS Ashdod vs Hapoel Kfar Saba | 3.04 | 3.04 | 2.42 |
| 19:00 | 2306 | Maccabi Petach Tikva vs Maccabi Jaffa | 1.57 | 3.79 | 5.98 |
| 19:00 | 4977 | Viimsi JK vs FC Elva | 2.36 | 3.71 | 2.66 |
| 19:00 | 5319 | Hapoel Acre vs Bnei Yehuda | 2.41 | 3.00 | 3.10 |
| 19:00 | 5594 | AEL Limassol vs Nea Salamis | 1.91 | 3.45 | 3.90 |
| 19:30 | 1420 | Cremonese vs Sampdoria | 2.38 | 3.27 | 2.83 |
| 20:00 | 1497 | Hatayspor vs Besiktas | 4.67 | 3.87 | 1.66 |
| 20:00 | 1915 | Adanaspor vs Genclerbirligi | 2.07 | 3.22 | 3.27 |
| 20:00 | 2410 | Coca Cola vs Arab Contractors | 2.06 | 3.04 | 3.84 |
| 20:00 | 2589 | OFI Crete vs Lamia | 2.17 | 3.14 | 3.39 |
| 20:00 | 4577 | Leixoes vs Tondela | 2.35 | 3.21 | 2.87 |
| 20:00 | 4953 | Zenit St Petersburg vs Sochi | 1.27 | 5.75 | 8.52 |
| 20:00 | 5141 | Aalborg vs Viborg FF | 2.94 | 3.34 | 2.30 |
| 20:30 | 4635 | Maccabi Tel Aviv vs Maccabi Netanya | 1.43 | 4.39 | 5.86 |
| 21:00 | 1013 | Jong Utrecht vs PEC Zwolle | 4.64 | 4.15 | 1.59 |
| 21:00 | 1415 | Jong PSV vs Helmond Sport | 2.01 | 3.45 | 3.35 |
| 21:00 | 1866 | Jong AZ Alkmaar vs Telstar | 2.33 | 3.40 | 2.76 |
| 21:00 | 3113 | Sepsi Osk vs Steaua Bucuresti | 2.45 | 3.22 | 2.77 |
| 21:00 | 3591 | Jong Ajax vs VVV Venlo | 1.67 | 3.94 | 4.34 |
| 21:00 | 5380 | FK Napredak vs Vojvodina | 2.47 | 3.05 | 2.72 |
| 21:15 | 5697 | Debreceni VSC vs Kisvarda FC | 2.63 | 3.22 | 2.44 |
| 21:30 | 5662 | Ascoli vs Cagliari | 2.87 | 3.07 | 2.46 |
| 21:30 | 5716 | GKS Katowice vs ZKS Stal Rzeszow | 2.12 | 3.36 | 3.02 |
| 21:45 | 4050 | Sassuolo vs Verona | 1.92 | 3.52 | 3.62 |
| 21:45 | 5057 | Le Havre vs Metz | 1.98 | 3.32 | 3.66 |
| 21:45 | 5409 | Shelbourne vs UCD Dublin | 1.44 | 4.01 | 6.45 |
| 21:45 | 5689 | Sligo Rovers vs Derry City | 3.97 | 3.44 | 1.79 |
| 22:00 | 2375 | Celta Vigo vs Getafe | 1.74 | 3.41 | 4.91 |
| 22:00 | 5064 | Real Oviedo vs Malaga | 2.11 | 3.01 | 3.66 |
| 22:00 | 5440 | West Ham vs Bournemouth | 1.52 | 3.95 | 5.92 |
| 22:15 | 4372 | Rio Ave vs Portimonense | 2.44 | 3.08 | 2.93 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MABONDIA NYOTA AFRIKA, MAREKANI KUZICHAPA SUPER DOME BOXING DAR

**Na Mwandishi Wetu**

MABONDIA nyota wa Afrika na Marekani watashiriki katika mapambano ya Super Dome Boxing yaliyopangwa kufanyika Novemba 4, mwaka huu kwenye ukumbi mpya wa kisasa wa Super Dome Arena.

**Mapambano hayo yameandaliwa kwa ushirikiano wa kampuni yenye uzoefu mkubwa wa kuandaa ngumi za kulipwa duniani, Global Boxing Stars kwa ushirikiano na Kampuni ya Tanzania, LP Sport chini ya udhamini wa Azam TV kupitia usiku wa vitasa.**

Mabondia ambao watashiriki katika uzinduzi wa Super Dome Boxing ni Nasibu Ramadhani ambaye atazichapa na bondia Toto Helebe wa Afrika Kusini katika uzito wa feather. Pambano hilo limeandaliwa kwa ajili ya kumpromoti bondia Ramadhan kwa mujibu wa Promota, Levis Paul wa LP Sports.

Paul anaamini kuwa Ramadhan bado ana kipaji cha hali ya juu licha ya hivi karibuni kutokuwa katika chati ya ngumi hizo kutokana na kukosa mapambano.

"Ramadhan ni bondia mwenye kipaji cha hali ya juu tofauti na rekodi zake. Ni bondia ambaye ameweza kupigana katika nchi nyingi duniani na mwenye uzoefu mkubwa. Lengo letu ni kumrejesha kwenye chati ya hali ya juu na kuwania ubingwa wa kimataifa mwakani," alisema Levis.

Pambano lingine litakuwa baina ya bondia Shaaban Jongo dhidi ya Mganda, Musa Ntege la kuwania ubingwa wa uzito wa cruiser wa Afrika (ABU) kwa nchi za Afrika Mashariki. Jongo akishinda pambano hilo atapata fursa ya kuwania ubingwa wa Afrika dhidi ya bondia Olanweragu Doradola na kuingizwa katika renki za WBC.

Paul alisema pambano lingine litakuwa la uzito wa juu kati ya bondia Mtanzania anayeishi Sweden, Tamim Awadh dhidi ya bondia kutoka Marekani, Jarrel Miller ambaye mpaka sasa hajapoteza hata pambano moja kati ya 25 aliyocheza huku 21 akiwa ameshinda kwa KO na kutoka sare moja. Tamim ameshinda mapambano 15 ambapo kati ya hayo, 10 ni kwa KO na kupoteza matano.

Bondia huyo kwa sasa ni bingwa wa uzito wa juu wa kimataifa wa chama cha World Boxing Foundation (WBF) baada ya kumchapa bondia wa Kosovo, Shkelqim Ademaj katika raundi ya tisa katika mji wa Eissporthalle Essen, Ujerumani Juni 11, mwaka huu.

Mabondia wengine watakaopanda jukwaani siku hiyo ni Mghana, Manyo Plange na Mnigeria Solomon Adebayo, ambaye atapambana na Hamis Palasungulu katika uzito wa juu.

## MITINDO...



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Brilliant iliyoko Mbezi Kimara kwa Msuguri, Dar es Salaam, wakionyesha umahiri wa mitindo ya mavazi wakati wa mahafali ya 12 ya shule hiyo yaliyofanyika shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# *Okrah, Aziz Ki wafalme Simba, Yanga*

INATOKA UKURASA 32

52, Fiston Mayele alipowaruka juu zaidi ya mabeki Josh Onyango na Henock Inonga kuunanisha mpira wa krosi ya Jesus Moloko, lakini mpira ukapaa juu ya lango.

Timu zote zilifanya mabadiliko, Simba ikiwatoa Pape Sakho, Okrah, Israel Mwenda na kuwaingiza Habib Kyombo, Erasto Nyoni, na Denis Kibu, huku Yanga ikiwapeleka nje, Kisinda, Moloko na nafasi zao zikichukuliwa na Farid Mussa na Gael Bigirimana.

Kabla ya kutoka, Okrah aliikosesha Simba mabao mawili ya wazi dakika ya 63 na 68, ambapo pia kama Phiri angekuwa makini angeweza kufunga bao dakika saba kabla ya mechi kumalizika.

**KABLA YA MECHI**

Hadi saa 10:30, mashabiki wa Simba walivunja rekodi yake baada ya kujaza eneo lao rasmi la kukaa ambalo huku nafasi eneo la mzunguko la Yanga kukiwa na nafasi za wazi.

Katika hatua nyingine wachezaji wawili wa klabu hizo kongwe Yanga, Aziz Ki na Clatous Chama walifanya kituko baada ya wawili hao kutegeana kuingia ndani ya uwanja wakati timu ikiwa tayari kwa ajili ya kupiga picha.

Ilichukuwa dakika moja kwa nyota hao kutegeana na baadaye Aziz Ki aliamua kuingia uwanjani Chama akafuata kwa ajili ya kukaguliwa na kuanza kwa mechi.

Michezo
Jumatatu Oktoba 24, 2022
Nipashe



Klopp azidi kulia na kiwango Liver UKURASA 30



Mashabiki wa Simba na Yanga wakifuatilia mechi ya Ligi Kuu wakati timu zao zikitoka sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana, **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ni Okrah, Aziz Ki

## Wamaliza ubishi nani zaidi Simba, Yanga kwa Mkapa, Wekundu wa Msimbazi watesa kileleni, lakini...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WACHEZAJI wawili kutoka Afrika Magharibi, Mghana Augustine Okrah na Stephane Aziz Ki, jana walimaliza ubishi wa nani zaidi katika 'Dabi' ya Simba na Yanga baada ya kuzifungia timu zao zikitoka sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Okrah alianza kuifungia Simba bao dakika ya 14, kabla ya Aziz Ki kusawazisha sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko.**

Ilikuwa ni mechi ya mzunguko wa kwanza Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.


Hata hivyo, Simba imeonekana kuwa na ugumu kuifunga Yanga kwenye Ligi Kuu, kwani mara ya mwisho ilikuwa ni Februari 16, 2019 kwa bao la Meddie Kagere.

Matokeo hayo yanazifanya timu zote zifikishe pointi 14 kila moja, Simba ikiendelea kukaa kileleni kwa idadi ya mabao ya kufunga.

Simba iliianza mechi hiyo kwa kasi na kama wachezaji wake wangetulia wangeweza kuandika bao sekunde ya 34 tu, baada ya Mohamed Hussein 'Tshabalala' kuambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto, akapiga krosi iliyowapita mabeki watatu wa Yanga, lakini Moses Phiri alichelewa kuunganisha mpira huo, naye ukampita na kutoka nje.

Yanga ilijibu shambulio hilo dakika ya 11, baada ya Tuisila Kisinda kumtoka Tshabalala na kupiga krosi ambayo ilizua kizaazaa kwenye lango la Simba, kabla ya kufagiliwa na Joash Onyango kabla ya kuvuka msitari wa goli.

Alikuwa ni Okrah, aliyeipatia Simba bao la kwanza dakika ya 14, baada ya kupenyezewa pasi mzunguko kutoka kwa Clatous Chama.



Kiungo mkabaji wa Simba, Jonas Mkude (kushoto), akiwania mshambuliaji wa Yanga, Aziz Ki kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

Baada ya bao hilo Simba walionekana kutawala mechi ikipiga pasi fupi fupi na kuwapa wakati mgumu viungo pamoja na mabeki wao.

Hata hivyo, wachezaji wa Simba walionekana kufurahia kuuchezea zaidi mpira kuliko kusaka bao la pili.

Kosa lililofanywa na Mzamiru Yassin kumchezea madhambi Khalid Aucho liliifanya Yanga kurudisha bao dakika moja ya nyongeza, wakati zikiwa zimeonyeshwa dakika mbili za ziada kabla ya mapumziko.

Aziz Ki, aliachia fataki kali lililokwenda juu pembeni kona ya lango, kulia kwa kipa Aishi Manula na kujaa wavuni.

**KIPINDI CHA PILI**

Kama kawaida ya Yanga iliingia kwa kasi na kufanya mashambulizi kwenye lango la Simba ambapo nusura ipate bao dakika ya

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042